Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**BUNGE LA TANZANIA**

____________

**MAJADILIANO YA BUNGE**

____________

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 14 Juni, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):**

Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2012/2013.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):**

Taarifa ya Sera ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni Viongozi Waandamizi wa Chama chetu tulifanya ziara katika Majimbo ya Mtwara Mjini, Mtwara Vijini, Tandahimba, Newala, Lulindi, Masasi na Nanyumbu katika Mkoa wa Mtwara na vilevile Jimbo la Lindi Mjini, Mtama, Mchinga na Ruangwa katika Mkoa wa Lindi. Kuna kilio kikubwa sana cha wananchi kuhusiana na utaratibu mzima wa zao la korosho hususan katika maeneo ya malipo yaliyocheleweshwa, upatikanaji hafifu na usio sahihi wa pembejeo na wakulima kucheleweshwa kulipwa malipo yao kwa kiwango ambacho kinatishia uendelevu wa zao hili la korosho.

Je, Serikali yako inazo taarifa hizo na kama inazo na kwa sababu kilio hicho kipo kwenye Kata zote ambazo tulizitembelea; mna mkakati gani wa makusudi wa ziada wa kurekebisha hali hiyo? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba niungane na Watanzania wenzangu, kutoa pole kwa Familia ya Mzee Bob Makani. Upande wa CHADEMA najua wamempoteza Kiongozi ambaye alikuwa anawasaidia kwenye Chama chao; kwa hiyo, tunasema pole kwa wote kwa jambo hili, lakini Mwenyezi Mungu alipenda hivyo hatuna budi kuheshimu kauli yake.

Kuhusu swali la Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, kwanza, namshukuru kwa taarifa lakini hakuikamilisha, alitakiwa aseme vilevile kwamba, wakati wameenda wamekuta tatizo hili la zao la korosho limekwisha. *(Makofi)*

Limekwisha kwa maana kwamba, korosho ambazo zilikuwa zimerundikana katika maghala ambayo ndiyo tulikuwa tunajaribu kuhangaika kujaribu kuhakikisha zinanunuliwa zilikwishanunuliwa. Kwa upande mwingine, tulikuwa na tatizo vilevile la malipo ya awamu ya pili kwa wakulima ambao walikuwa hawajalipwa. Sasa kiasi cha fedha ambacho kilipatikana ndiyo hicho ambacho kimeanza kutatua tatizo la kuwalipa wakulima wote ambao walikuwa bado

hawajakamilisha zoezi. Wakati huo huo tulikuwa tunaendelea na zoezi la kupata fedha kutoka Benki ya Biashara, ambayo kwa kweli tulichotaka sisi ni dhamana ili kuwezesha Vyama vya Ushirika viweze navyo kukamilisha zoezi hilo kuhakikisha kwamba madai yote yanakamilishwa, ndiyo maana nimesema kwamba kwa sehemu kubwa tatizo lile limeshashughulikiwa na imani yangu ni kwamba muda si mrefu hakuna tatizo ambalo litabaki linazungumzwa kuhusiana na zao hilo.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, sisi tumetembelea Wilaya anazozizungumzia, tumewasikiliza wananchi na malalamiko haya ninayowasilisha hapa ni dhahiri na Mheshimiwa Waziri Mkuu amejibu hoja moja tu hapa ya malipo lakini katika swali langu la msingi liliuliza mambo matatu; malipo, pembejeo na soko.

Kitu kinachojidhihirisha kwa dhahiri hapa kuna utawala mbovu ambao unazingira kilimo chote cha korosho. Bodi ya Korosho haiwezi kukwepa lawama hizo na kwa bahati mbaya zaidi, Mwenyekiti wa Bodi ya Korosho ni Mbunge mwenzetu na baadhi ya Wajumbe ni Wabunge wenzetu wanaotoka maeneo hayo hayo ambao tungetegemea wawatetee wananchi hao. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi nilichokueleza ni hali halisi tuliyoikuta katika mkoa.

**SPIKA:** Muwe na utulivu.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, unalizungumziaje tatizo la pembejeo na tatizo la malipo kwa wananchi ambayo yanapingana kutoka eneo moja kwenda lingine? Je, huoni sasa kuna ulazima wa kutoingiza Wabunge katika Bodi za Mazao kwa sababu Bodi hizi zinatakiwa ziwasimamie wahusika na siyo zihusike kwa sababu kunakuwa kuna *double interest* ama *conflict of interest?*

**WAZIRI MKUU:** Soko la korosho kwa sasa kwa sehemu kubwa ni nje ya Tanzania na hasa India. Soko hili la korosho linatawaliwa na bei ambazo zinatokana na bei za Kimataifa huko nje na hili ndiyo tatizo ambalo tunalo kwenye pamba na ndiyo tatizo tulilonalo kwenye mazao mengine. Tatizo linaanza pale inapotokea kwamba bei ya zao katika ya haya mazao ambayo yanategemea masoko ya nje inaposhuka ghafla katika masoko ya dunia na kuwa lina tatizo ndani nchi ambayo ndiyo wauzaji kama sisi Tanzania. Kwa hiyo, korosho ndiyo kilichotokea, kwa sehemu kubwa walidhamiria kuuza korosho kwa bei ambayo ilikuwa ni nzuri, zaidi ya shilingi 1000, ghafla bei ikashuka ikawa sasa haina tija kwa mtu ambaye alitaka kuuza korosho hizo nje na ikaleta tatizo. Nimesema hatimaye jambo hili lilikuja kutatuliwa, mnunuzi alipatikana na korosho zikaweza kuuzwa. *(Makofi)*

Tatizo la soko hatuwezi kusema litatatuliwa na sisi moja kwa moja, ni lazima tukubali kwamba kwa mazao ambayo kwa sehemu kubwa yanatawaliwa na soko la nje, lazima tuendelee kulitazama jambo hili kama changamoto kwa Taifa letu. Sisi tunadhani njia rahisi ni kuimarisha viwanda vyetu vya ndani ili tuwe na soko la ndani la uhakika na ndiyo maana msisitizo mkubwa sasa ni kwenye viwanda. Kwa hiyo, kwa maana hiyo hata viwanda vya masoko ni lazima tuvijenge, tuviimarishe ili tuweze kuwapa Watanzania uhakika wa soko lao. Kwa hiyo, nadhani hili ni jambo moja.

La pili, ni hili ambalo umegusia juu ya pembejeo; pembejeo nazo ni suala ambalo linasimamiwa moja kwa moja na vyombo ambavyo vimepewa dhamana hiyo na hasa kwa sehemu kubwa Ushirika na Bodi. Sasa ni kweli kumekuwa na matatizo kidogo juu ya uagizaji na tatizo la kiuendeshaji ambalo nalo likisimamiwa vizuri linaweza kumalizika kama tukidhamiria wote kwa pamoja. Kwa hiyo, imani yangu ni kwamba, tutajitahidi tuweze kufanya vizuri zaidi katika eneo hilo.

Umeongelea juu ya Wabunge; mimi nadhani hilo ni suala letu na tunaweza tukalizungumza Bungeni likaisha, lakini isiwe kwamba sasa kwa sababu tatizo limetokea basi mzigo unambebesha Mwenyekiti wa Bodi na Mbunge ambaye ni Mjumbe wa Bodi, hapana. Mimi sidhani kama hiyo ni sahihi sana, lakini tunachoweza kusema tu kwamba tatizo likitokea suluhu ni kupata ufumbuzi wa tatizo. Sasa kama suala la Bodi ni tatizo, bahati nzuri wote tupo hapa hakuna tatizo tunaweza tukakubaliana tukaondoa hilo taratibu halafu likamalizika, lakini hata ukifanya

hivyo siyo kwamba itakuwa ndiyo ufumbuzi wa tatizo unalolizungumza leo hata kidogo, bado tutaendelea kufanya kazi kwa ushirikiano kutatua matatizo ya wakulima.

**MHE. RAJABU MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa hivi karibuni Zanzibar kulitokea machafuko na vurugu iliyopelekea baadhi ya watu kuumia na mali zao kuharibiwa; na kwa kuwa Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kimataifa tulishapata amani na utulivu; na kwa kuwa Zanzibar wapo watu takriban asilimia 33 ambao waliikataa au hawakuikubali Serikali ya Umoja wa Kitaifa na inasadikika kwamba hadi leo bado watu hawa hawajaridhika nayo; hivi sasa kuna baadhi ya lugha ambazo zinahusisha vurugu zile na baadhi ya makundi na vyama vya siasa:-

Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Zanzibar itakuwa tayari kuunda Tume Huru kuweza kuchunguza kadhia hii iliyowakuta Wazanzibari ili wale waliohusika waweze kuchukuliwa hatua za kisheria? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed kwamba, hivi karibuni tulipata tatizo hilo la uvunjifu wa amani kule Zanzibar, tarehe 26 Mei, 2012. Vurugu hizo ziliendelea mpaka tarehe 27 kabla hazijatulizwa.

Taarifa nilizonazo ni kwamba, chimbuko la tatizo hili ni Shirika moja lisilo la Kiserikali ambalo limeandikishwa Zanzibar kwa mujibu wa Sheria mwaka 2001 linaloitwa Jumuiya ya Mihadhara ya Kiislamu, maarufu sana kwa jina Uamsho. *NGO* hii malengo yake ukiyasoma ni mazuri sana, sehemu kubwa ni kuendeleza Dini na imani ya Kiislamu, kujenga upendo na amani miongoni mwa waislamu na kufanya matendo mengine yoyote ambayo lengo lake ni kumwendeleza Mwislamu na kuendeleza Dini ya Kiislamu. Awali inaonekana walitekeleza jukumu hili vizuri, lakini hapa katikati kukaanza kujitokeza hali ambayo iliashiria kwanza kuondoka kwenye mwelekeo wa mambo yake ya msingi na hasa pale juhudi za Umoja wa Serikali ya Kitaifa pale Zanzibar ulipoanza kuzungumzwa. Tukaanza kuona dalili za chokochoko, kuonekana kutokuridhika na hali hiyo na mambo mengine kama hayo, lakini hatimaye baada ya umoja kuundwa ikaonekana hali imetulia.

Tulipoanza mchakato huu wa Katiba, Uamsho nao wakaanza. Sasa kusingekuwa na tatizo kama dhamira ingekuwa ni kuendeleza jambo hili kwa nia njema, lakini kilichojitokeza kwa taarifa za kiusalama ni kwamba, ilikuwa kupinga kitu kinachoitwa Muungano na tarehe 26 Mei, 2012 hawa watu walikuwa wamepewa kibali cha kwenda kufanya mkutano. Katika mkutano ule wamezungumza waliyoyazungumza na kwa sehemu kubwa ilikuwa ni haya ya kujaribu kukataa kitu kinachoitwa Muungano. Baada ya pale wakaamua kufanya maandamano ambayo polisi hawakuwa na taarifa nayo, kwa hiyo, ikabidi polisi waingilie kati. Kilichofuatia baada ya pale, Rais alijaribu kukieleza vizuri sana kwenye hotuba yake ya mwisho wa mwezi lakini hata kabla yake, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi naye alikuwa amelizungumza vizuri sana kwenye vyombo vya habari.

Pengine bila kuendelea sana kwenye historia, kimoja ambacho na mimi nakubaliana na wewe kabisa ni kwamba ni vizuri jambo hili likadhibitiwa, lisiachwe kuendelezwa na hasa kwa sababu fursa ipo katika mwelekeo wa sasa wa kuandika Katiba upya. Moja ya jambo ambalo Serikali imekuwa wazi ni kwamba, suala hili la kuzungumza juu ya Muungano, kutafuta namna ya kuboresha, kuona namna gani tuendeleze ni kitu ambacho kipo wazi; kwa nini tuingize choko choko ambazo hazina tija!

Waliohusika walikamatwa pamoja na Sheikh ambaye alikuwa ni mmojawapo katika wale waliokuwa wameongoza maandamano yale, Sheikh Juma Issa. Ni dhahiri kabisa kwamba, ndani ya vuguvugu hili la Uamsho, taarifa za kiusalama zinasema vilevile inawezekana wapo watu kama unavyowasema na inawezekana Viongozi wa Kisiasa vilevile wamo na watu wengine ambao pengine hawautakii Muungano mambo mema; kwa hiyo ni kweli lazima wote tuendelee kulitazama kwa macho makali. *(Makofi)*

Umetoa rai kwamba pengine kungeundwa Tume Huru ili itazame jambo hili kwa upana wake tuone ni mambo gani pengine tunaweza kuyafanya kuweza kukabiliana na jambo hili. Mimi

nadhani rai ni nzuri, lakini siwezi nikalitolea maamuzi moja kwa moja; tunaweza bado tukalifikisha kwenye Serikali ya Mapinduzi Zanzibar waone kwanza kama ni jambo ambalo linastahiki, maana inawezekana hatua ambazo wamezichukua pengine wanaona zinatosha au vinginevyo. Vinginevyo, kama rai, nadhani ni nzuri sana ili wote tuweze kujua mustakabali wa nchi yetu utakuwaje kutokana na hizo purukushani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rajab, naomba uulize kwa kifupi kwa sababu maelezo yamekuwa marefu.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina swali moja.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu umetaja suala la vyombo vya habari; na kwa kuwa wakati kadhia hii inatokea vyombo vya habari vilitoa taarifa nyingi hususan kuhusiana na kuchomwa kwa makanisa lakini wakasahau kwamba kuna baadhi ya misikiti na kuna baadhi ya vyombo vya watu wa kawaida viliharibiwa; na kwa kuwa moja kati ya tatizo lililowakumba wenzetu Kenya ni vyombo vya habari kupotosha habari au kutoa habari za upande mmoja:-

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu una tamko gani juu ya vyombo vya habari kuhusiana na kutoa taarifa kama hizi kwa upande mmoja tu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari ndiyo vimeandika hivyo, lakini rai yako nadhani ni nzuri, kuviomba vyombo vya habari wanapotoa taarifa hizi ni lazima uliweke kwenye mizania vizuri kwa sababu kama unachosema ndicho kilichotokea na mkaacha kusema juu ya upande mwingine, hisia zinazojengeka zinaweza zikaonekana kama vile jambo hili limeegemea makanisa tu na kumbe kwenye purukushani ile ipo pia misikiti ambayo inawezekana vilevile kwamba iliharibiwa. Kwa hiyo, ni suala tu la uandishi, ni suala la watu wanaohusika na vyombo hivyo kuweza kutoa taarifa sahihi.

Niseme tu kwamba, kwa namna jambo hili lilivyofanyika ni dhahiri kabisa kwamba, purukushani ile unaweza ukaitafsiri kwa maana nyingi sana, maana unapoingia sasa unachoma makanisa, unakwenda unaparamia *guest house* unachoma, unakwenda unachoma msikiti, inaweza kuwa ni vurugu za jumla lakini ndani yake kila mmoja atataka kuelekeza nguvu kule anakoona yeye kunamfaa. Sasa kikubwa ni kudhibiti chanzo, ndiyo maana mimi nakubaliana na wewe kwamba hili jambo lazima tutafute suluhu ya kudumu.

Kwa sasa niseme kama walivyosema Viongozi wa Kitaifa, kwanza ni kushukuru Polisi ambao waliharakisha kuchukua hatua katika kusimamia jambo hili haraka ili wasiendelee kuharibu mali za watu. Kwa hiyo, nadhani tutawasihi waendelee na vyombo vya usalama viendelee kufuatilia jambo hili kwa ukaribu sana na vyombo vya sheria navyo viharakishe kesi ambazo zinahusu wale wote ambao wameshakamatwa na mkondo ule uweze kwenda haraka zaidi.

**SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Murtaza Mangungu.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Wananchi wa Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Mbeya, Iringa na Rukwa katika kipindi cha mwaka 1905 - 1907 walipigana Vita ya Majimaji. Je, ni lini Serikali itafikiria kudai fidia ya udhalilishaji na unyama huu kwa wananchi ndani ya nchi yao?

**SPIKA:** Amdai nani? Adaiwe nani?

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Wadaiwe Wajerumani ambao tulipigana nao. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Haki ya Mungu! Haya Waziri Mkuu labda unaiweza hiyo. *(Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naona Mheshimiwa Mangungu leo kaniamkia vibaya. *(Kicheko)*

Sina hakika kama tunachoweza kusema ni kwamba tudai fidia maana mimi kwangu nimekuwa nawachukua wahanga hawa kama watu ambao unaweza ukasema ni mashujaa waliopambana na mkoloni; mtu ambaye alitaka kutugandamiza wakampiga na wakamfukuza. Nilikuwa naichukulia kwamba ni mashujaa ambao wanastahili kwa sehemu kubwa kupewa heshima na sifa na Watanzania kwa kazi waliyoifanya.

Sasa sina hakika kama hiyo hoja inatekelezeka lakini nadhani kubwa kama Taifa, hebu tuwe na kiburi na faraja kuona kwamba tulikuwa na watu hata enzi hizo ambao waliukataa ukoloni kwa asilimia mia moja.

Sasa hoja yake inaweza pengine ikatazamwa katika nyakati tofauti kama itaonekana ni nzito zaidi, lakini kwangu mimi zaidi ni kuwatambua na kuwaenzi sana wale wote ambao walishiriki katika Vita ya Majimaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mangungu bado kweli unauliza; maana hata wakidaiwa wakifaidika na mimi nitafaidika kwa sababu ni mtoto wa Chifu. (*Makofi*)

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nakubaliana na yeye ni kweli wanaenziwa na sisi Wamatumbi na Wangindo tumejengewa mnara katika eneo la Nandete kama kumbukumbu ya ushujaa ule.

La msingi ni kwamba kuna baadhi ya nchi zimedai fidia na utaratibu wa kuwafidia wananchi wale unaendelea. Sisi ndiyo waanzilishi wa vuguvugu lile katika Ukanda mzima wa Kusini mwa Afrika. Kwa nini hatujafikiria kudai fidia hii wananchi wetu wamedhalilishwa, kunyanyaswa na kuuawa katika unyama ambao umepitiliza kabisa?

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi sina kumbukumbu ya nchi ambazo zimefanya hivyo, kama zipo tutatazama mifano yao tuone walikuwa na misingi ipi.

Pengine kama ni kusaidia nadhani hoja isingekuwa hivyo, hoja ingekuwa basi tudai fidia kwa wakoloni ambao walitutawala wakatudhalilisha, wakatunyonya, badala tu ya kuchukua eneo moja kwa sababu ukoloni ni ukoloni tu, ile ilikuwa ni dalili ya kukataa kwetu kama Taifa lakini nadhani hoja ingekuwa pana zaidi. Mimi nipo tayari kama atanipa mifano ya nchi hizo tuone kama inafanana na hali ya Tanzania.

**SPIKA:** Tunaendelea na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na tatizo kubwa sana la uhusiano kati ya wananchi wanaoishi kandokando ya hifadhi, mapori ya akiba na WMA na wahifadhi. Mheshimiwa Waziri Mkuu utakumbuka pale ulipotembelea Wilaya ya Meatu tarehe 22 Februari 2012 ulijionea malalamiko makubwa dhidi ya wananchi hasa kuhusu mpaka, kuhusu wananchi kupigwa na kuuawa, kuhusu kutozwa faini kiholela tena porini na wakati mwingine Maaskari wa *Game Reserve* wanajigeuza kuwa Mahakama wanahukumu huko huko porini na kero nyingine nyingi ambazo ulizishuhudia zikiwepo za rushwa kubwa na wahifadhi nao walikuwa na malalamiko yao.

Katika kusikiliza malalamiko haya uliamua Tume Huru iundwe na ichunguze ukweli wa mambo hayo na kisha iweze kuishauri Serikali ili kutafuta ufumbuzi wa kudumu kuhusu malalamiko hayo na matatizo hayo.

**SPIKA:** Swali sasa!

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Je, Tume hiyo itaundwa lini kwa kuwa mpaka sasa sina taarifa za kuundwa kwake wala sijaiona Jimboni?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli anavyosema Mheshimiwa Mpina; nilipopita wakati wa ziara ya Mkoa wa Simiyu nilikutana na malalamiko hayo Meatu na niliwaahidi kwamba kama bado inaonekana ni jambo la busara kuwa na Tume kuja kutazama tatizo hili, basi nitakwenda kufikiria niweze kuona uwezekano wa kuunda hiyo Tume.

Baada ya ziara ile nilichofanya ni kuagiza Mkoa uchukue hatua stahiki kuhakikisha kwamba wanashirikiana na vyombo vinavyohusika ili kurejesha hali ya amani na utulivu katika maeneo yanayohusika. Vilevile niliwaagiza kwamba, katika jitihada hizo ni lazima waendelee kutoa elimu kwa wananchi ili wasiwe wanaondoka katika maeneo yao kwenda kulisha mifugo katika maeneo ya hifadhi, kwa sababu kwa kufanya hivyo ndiyo matatizo yanapoanzia. Sasa, nimekuwa nafuatilia jambo hili kwa sehemu kubwa na ninaona jitihada hizo zinaendelea vizuri.

Hili la Tume sijafikia hatua ya mwisho ya kuamua kama tuunde au tusiunde, kwa sababu baada ya hapo nimeshauriana na Wizara zinazohusika na kujaribu kuona historia ya namna tulivyoshughulikia jambo hili na nikawaahidi kwamba, basi wanipe muda ili niweze kuona kama kuna haja au hatua zilizokwishachukuliwa zinatosheleza. Kwa hiyo, baada ya muda mfupi nitatoa taarifa kwa Wakuu wa Mikoa wanaohusika.

**SPIKA:** Ahsante. Naomba tuendelee na Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema.

**MHE. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni ulipanga ziara kuja kwenye Jimbo langu la Vunjo lakini kwa bahati mbaya ukatingwa na kazi nyingine na kazi moja ambayo ...

**SPIKA:** Linatakiwa liwe ni swali la Kitaifa.

**MHE. AUGUSTINE L. MREMA:** Haya. Mheshimiwa Waziri Mkuu; hivi karibuni ulikuwa umepanga kufanya ziara kuja kwenye Jimbo langu la Vunjo na Wananchi wa Jimbo la Vunjo wakakutarajia kufika na wakakungojea kwa hamu. Sasa naomba kujua kama utapata nafasi unaweza kuja lini ili uwafafanulie ile Sera yako nzuri ya Soko la Kimataifa ambalo litakuwa na vitu vingi vya kusaidia ajira katika Jimbo la Vunjo?

Mheshimiwa Spika, ni hivyo tu.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Waziri Mkuu, sema tafadhali na mengine utayajibu huko huko.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema Mzee Mrema, nilikuwa nimeamua kwenda kufanya ziara fupi katika Mkoa wa Kilimanjaro. Nilitaka kwenda kutembelea Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro pale Moshi kwa lengo la kujua matumizi ya ule uwanja kwa sasa na kama yanajitosheleza tuone ni namna gani tunaweza tukautumia Uwanja ule kwa njia ambayo ina tija zaidi. Niliahidi kwenda kutembelea Soko la Himo na kwenda kutembelea umwagiliaji katika Wilaya ya Mwanga.

Kwa bahati mbaya sana, wakati nimepanga kuja, Rais akaniagiza niende kumwakilisha Angola, kwa hiyo, nikalazimika kuvunja ile ziara nikaenda Angola. Kwa hiyo, naomba radhi, nilimwambia Mkuu wa Mkoa aniombee radhi lakini sijafuta ile ziara hata kidogo, nikipata mwanya wowote ule nitakuja kuifanya hiyo ziara kama nilivyoahidi. Najua una shauku kubwa sana na Himo kwenye Soko lako la Kimataifa na mimi nilitaka kuja kuona kazi inayoendelea ili tuweze kuiendeleza vizuri zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mrema, ngoja atakapokuja. Sasa nimwite msemaji wa mwisho ambaye ni Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar.

**MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR:** Mheshimiwa Spika, naomba radhi kwa sababu swali langu limejibiwa kwa hiyo naomba kulifuta.

**SPIKA:** Limefanana na lingine, ahsante. Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Waziri Mkuu; mchakato wa kutoa maoni kwa ajili ya Katiba Mpya unakaribia kuanza na Serikali iliahidi kutoa nakala milioni nne za Katiba. Je, Serikali itaanza lini kutoa nakala hizo za Katiba kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania waweze kutoa maoni yao vizuri?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahadi tuliyoitoa ilikuwa ni ya nakala 500,000 za Katiba lakini rai iliyotoka ikawa ni kwamba mbona ni kidogo, ni vizuri zikaongezwa kwa kadiri itakavyowezekana ili ziweze kuwafikia watu wengi zaidi. Kwa hiyo, zoezi hili tunaendelea nalo na kwa sasa nafikiri tumeshafikisha nakala kama 200,000 lakini uchapishaji unaendelea.

Nilipokutana na Mwenyekiti wa Tume, Mzee Joseph Warioba, wakati tulipokwenda kutembelea ofisi yao na hata alipokuja kwenye Mkutano wa Wakuu wa Mikoa hapa Dodoma, kwa ajili ya kuwasilisha mada juu ya mchakato unavyoendelea. Moja ya jambo ambalo Tume imeamua kufanya ambalo nadhani ni zuri sana ilikuwa ni kuandaa makala kwa muhtasari yanayoonesha maudhui ya Katiba ya nchi kama ilivyo sasa kwa sababu ukienda kusoma kile kitabu au ile Katiba yenyewe kidogo lugha yake ya kisheriasheria mambo mengine hayakukaa vizuri sana. Kwa hiyo, wao wameamua kushughulikia na maudhui katika maeneo yake mbalimbali ili msomaji aweze kujua kwa ujumla Katiba ina mambo gani, lengo la maeneo hayo ni kitu gani, kwa lugha nyepesi inayoweza kueleweka na Mtanzania katika mazingira tuliyonayo hivi sasa. Nadhani na ile taarifa nayo itasaidia sana katika kurahisisha uelewa juu ya suala hili la Katiba.

Kwa hiyo, tunaendelea na huo mchakato na ahadi ya Serikali bado ipo palepale na tunashirikiana na Tume kuona kazi hiyo inafanyika vizuri.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha na Mheshimiwa Waziri Mkuu tunapenda kukushukuru sana kwa kujibu maswali mazito na kwa sababu yalikuwa mazito sana walioomba walikuwa tisa, nimefanikiwa kuwapa nafasi watano tu basi.

## MASWALI YA KAWAIDA

**SPIKA:** Maswali ya kawaida, tunaanza na Mheshimiwa Azza Hillal Hamad atauliza swali la kwanza.

Na. 21

### Kuwasaidia Kielimu Watoto Wanaoishi Kwenye Mazingira Magumu

**MHE. AZZA HILLAL HAMAD** aliuliza:-

Mpango wa Serikali wa kusaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu umekuwa ukisuasua kwa muda mrefu:-

Je, Serikali inawasaidiaje watoto wanaofaulu kuingia Elimu ya Sekondari ili kuhakikisha wanamaliza elimu yao hiyo na hata wanapofanikiwa kuendelea zaidi?

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la watoto wanaoishi katika mazingira magumu ni suala mtambuka, linalohitaji ushiriki mkubwa wa jamii yenyewe na Wizara mbalimbali zikiwemo Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaaa.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Serikali wa kugharimia Elimu ya Sekondari kwa watoto wanaotoka katika mazingira magumu ulianza kutekelezwa mwaka 2003 kwa lengo la kuwapa fursa sawa ya Elimu ya Sekondari watoto wote nchini. Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ilikuwa ikiwasomesha watoto hawa kwa kuzingatia mahitaji yaliyoainishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kugatua usimamizi wa uendeshaji wa Shule za Sekondari kuhamishiwa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Halmashauri ziliagizwa kwamba, kuanzia tarehe 1 Julai, 2009, ziendeshe zoezi la kuwabaini watoto wote wanaoishi katika mazingira magumu na kuandaa gharama za kuwasomesha kisha kuzijumuisha katika Bajeti ya Mwaka ya Ruzuku ya Matumizi Mengineyo (*OC*).

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Mkoa wa Shinyanga umetenga katika bajeti yake shilingi 67,250,000.00 kwa ajili ya kusomesha watoto wanaoishi katika mazingira magumu 2,579 kwa mchanganuo ufuatao:-

| HALMASHAURI | IDADI YA WATOTO | KIASI KILICHOTENGWA |
|---|---|---|
| Kahama | 1655 | 35,950,000/= |
| Kishapu | 170 | 5,200,000/= |
| Shinyanga Manispaa | 221 | 10,100,000/= |
| Shinyanga Vijijini | 533 | 16,000,000/= |
| Jumla | 2,579 | 67,250,000/= |

Mheshimiwa Spika, bajeti inakidhi baadhi ya mahitaji ya msingi ya watoto; hivyo, tunahamasisha jamii kwa ujumla kushiriki kikamilifu kuwapatia mahitaji muhimu ili kupunguza ugumu wa maisha kwa watoto hao.

Mheshimiwa Spika, ni jukumu la Serikali kuwahudumia wananchi wake wakiwemo watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Serikali inawahimiza wazazi na jamii kwa ujumla, kuwapenda na kuwapa huduma muhimu watoto ili wasitoroke kuingia mitaani. Pia, inaendelea kuzihimiza Halmashauri kufanya sensa kila mwaka ya kuwatambua watoto hao ili kuwa na takwimu sahihi zitakazorahisisha mchakato wa bajeti.

**MHE. AZZA HILLAL HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimwulize maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa watoto hawa wamekuwa wakirudishwa mara kwa mara nyumbani kwa kukosa kulipiwa ada; je, Serikali inatoa tamko gani kwa Halmashauri zinazoshindwa kutimiza wajibu wake kwa watoto hawa na kupelekea kukata tamaa ya kuendelea na masomo yao?

(ii) Kwa kuwa utaratibu mzima wa upatikanaji wa fedha hizi unaonekana kuchelewa; je, ni lini Serikali itafanya utaratibu mwingine mzuri ili malipo haya yaweze kuwafikia kwa wakati?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka nikiri hapa kwamba, jambo ambalo Mheshimiwa Mbunge analileta hapa ni la msingi sana, ni jambo ambalo tunajua kabisa kwamba ni tatizo. Sasa jambo hili kama tulivyoeleza hapa, linatuhusu sisi wote tunaozungumza hapa. Kama Halmashauri inataka kuhalalisha matumizi ya pesa zinazopelekwa kule, moja ya eneo ambalo tunatakiwa kuliangalia ni hili linalozungumzwa hapa la watoto ambao wako mitaani. *Justification* hiyo ni ya hali ya juu sana, kama watoto hao unawaacha wanazagaa pale hawana baba wala mama, mama na baba wamekufa kwa UKIMWI, mama yake na baba yake atakuwa ni Halmashauri na Serikali na Serikali itakapofanya hivyo ndiyo heshima yake inaongezeka.

Tunawaomba sasa hili jambo ni la kwetu sisi wote, yaani Wabunge, Madiwani na wote tunaohusika. Maelekezo yalikwishatolewa kwamba kila Halmashauri ihakikishe inatenga fedha kwa ajili watoto hawa. Kwa hiyo, unapokaa katika Kikao cha Baraza la Madiwani, ukiona watoto

hawa hawakutengewa fedha, useme sipitishi bajeti hii mpaka nione *item* ambayo ina-*deal* na hawa watoto.

Mheshimiwa Spika, maelezo haya niliyoyatoa na ninaposisitizia jambo huwa sauti inapanda, unisamehe mama yangu hapa. Tulikwenda Lushoto pale tukazungumzia jambo hili tukakubaliana na ni la kwetu sote Waheshimiwa Wabunge, tunawaombeni msimamie kule mliko mhakikishe fedha hizi zinatengwa.

Leo nimezungumza na *RAS* anaondoka anakwenda Kahama nikamwambia fedha hizi watakwenda kunibana. Ukiangalia katika *public expenditure*, ukurasa wa 177, *Volume III, Item 20071100,* zimewekwa kule, lakini zimeingizwa katika kifungu cha *OC*. Kuhusu kwamba fedha hizi zinachelewa, dada yangu Mheshimiwa Azza nenda kafuatilie jambo hili, kamkamate Katibu Tawala, mwambie nimeambiwa fedha hizi zipo hapa na wale wote niliowasomea nendeni mkaangalie, mkikuta hazipo njooni.

**SPIKA:** Jihadhari usiende kumkaba utakabwa wewe. *(Makofi)*

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa suala la kuishi katika mazingira magumu ni suala mtambuka lakini katika ufanyaji wa *implementation* ya zoezi hili imeonekana likiwasahau watoto wenye mtindio wa ubongo na pia walemavu wanakuwa sehemu ya mpango huu. Je, Serikali inasema nini juu ya kuwapatia kundi hili huduma za afya na elimu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hivi sasa tumeanzisha utaratibu katika Halmashauri unaoitwa *Community Health Fund (CHF).* Zipo Halmashauri sasa hivi tunavyozungumza ambazo tayari zimeanza kuwaingiza watoto hawa katika Bima za Afya za *Community*. Hawa watoto wanaozungumzwa hapa ni watoto ambao wana hali mbaya sana, wenye mtindio wa ubongo, ambao wanaonekana kwamba wameathirika na watoto wengine wa namna ile. Zipo Halmashauri ambazo zimeamua kuwaingiza kule ili wakienda hospitali waweze kupata huduma kama watoto wengine. Utaratibu huu upo katika Halmashauri na kama nilivyosisitiza hapa ni wajibu wetu sisi Wabunge na Madiwani na wale wote tulioko katika Halmashauri, kuhakikisha kwamba hawa nao tunawaangalia.

Mheshimiwa Spika, watu wananiangalia, najua wanashangaa huyu jamaa anazungumza nini! Ninazungumzia utaratibu ambao upo kule, unatekelezwa au hautekelezwi sasa hiki ni kitu kingine ambacho sisi wote tunawajibika katika hili.

Naona rafiki yangu Mheshimiwa Moses Machali ananiangalia, anafikiri nataka kutengeneza jukwaa hapa; nasema twendeni tukafuatilie utaratibu huu hata watoto wanaoingia darasa la saba na wanaokwenda Kidato cha Kwanza wote tuwapangie utaratibu katika vijiji kuwatambua na kujua majina yao ili waweze kusaidiwa.

Na. 22

**Kutunga Sheria ya *National Policy For Consultancy Industry***

**MHE. TUNDU A. M. LISSU (K.n.y. MHE. PHILEMON K. NDESAMBURO)** aliuliza:-

Mnamo mwaka 2005 aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Ubinafsishaji), Mheshimiwa Dkt. Abdallah O. Kigoda (Mb.), alianzisha mchakato wa kutunga Sheria ya *National Policy for the Consultancy Industry in Tanzania* ambayo ingeliwezesha Taifa kupata mwelekeo mzuri katika kuleta maendeleo katika uchumi wa nchi kwa kupata ushauri mzuri kutoka kwa wataalam:-

(a) Je, Serikali imefuta utaratibu huo mzuri ambao ungeliletea Taifa faida kubwa?

(b) Kama bado mpango huo upo; je, ni lini Muswada huo utaletwa hapa Bungeni?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Kiwelu Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianza kuandaa mchakato wa Sera ya *National Policy for the Consultancy Industry in Tanzania* ili kuwawezesha Wataalam Waelekezi kuweza kuishauri Serikali kuhusu masuala ya kiuchumi na kijamii. Muswada wa Sera ya Taifa ya Utaalam Elekezi Tanzania ulijadiliwa na wadau katika hatua mbalimbali na kukubaliwa, uliandaliwa na kupelekwa katika Baraza la Mawaziri na ushauri kadhaa ulitolewa kwamba iwepo Sera na ianze kabla ya Sheria. Katika kutekeleza Sera hii, kianzishwe Chama cha Wataalam Waelekezi ili kitumike kama Sekretarieti ya Baraza la Taifa la Wataalam Elekezi. Baraza la Taifa la Wataalam Elekezi lichukue jukumu la kuratibu kwa sababu wakati huu kuna Sera nyingi za Kisekta na Taasisi ambazo zinafanya kazi kisheria. Baraza la Taifa la Wataalam Elekezi lihakikishe Sera na Mikakati inayofuata inaendana na ile ya makubaliano ya Kimataifa ya Biashara *(International Trade Agreement)* na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwezeshaji wakati ule ichukue jukumu la kuandaa Mpango Mkakati wa Sera haraka iwezekanavyo na kuhakikisha kuwa inatekelezwa kwa faida ya Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wake, Serikali ilikamilisha uundaji wa Sera ya Taifa na Huduma za Ushauri Mwaka 2005 na Mkakati wa Utekelezaji kwa kipindi cha mwaka 2005/2010, chini ya utaratibu wa iliyokuwa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Aidha, kutokana na mabadiliko ya Muundo wa Serikali, uliotangazwa Februari mwaka 2008, baadhi ya majukumu yaliyokuwa Wizara hiyo yaliyokasimiwa kutekelezwa na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, yalihamishiwa Wizara mbalimbali. Miongoni mwa majukumu hayo ni Kuraribu Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma za Ushauri *(National Policy for the Consultancy Industry in Tanzania)* ilihamishiwa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana mwaka 2009 ambayo sasa ni Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa utekelezaji wa Sera hii unaenda sambamba na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ajira ya Mwaka 2008 kwa kuhusisha vyombo vya utatu kama vile Baraza la Ushauri na Masuala ya Kazi, Uchumi na Jamii *(LESCO)*. Aidha, mchakato wa kuandaa Rasimu ya Sheria ya Uanzishaji wa Baraza la Kitaifa la Huduma na Ushauri unafanyiwa kazi hivi sasa ikiwa ni pamoja na kupata maoni ya wadau mbalimbali chini ya utaratibu wa Wizara ya Kazi na Ajira. Kwa kuzingatia maoni hayo ya wadau na vilevile tija katika Taifa, Serikali itatathmini namna nzuri zaidi ya kuendelea na utekelezaji wa Sera hii kwa kushirikiana na wadau.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Je, Muswada wa Sheria iliyoulizwa na Mheshimiwa Ndesamburo utaletwa lini Bungeni kama upo?

(ii) Kazi ya ushauri elekezi kwa utaratibu uliopo sasa ipo kwa mujibu wa sheria katika vyombo vya taaluma husika kama sheria, uhandisi na udaktari. Swali langu ni kwamba; kwa vile vyombo vya taaluma hizi tayari vinashughulikia masuala ya Washauri Waelekezi katika taaluma zinazohusika; je, hili Baraza la Kitaifa la Huduma na Ushauri litafanya kazi gani ambayo haifanywi na vyombo vya taaluma hizi kwa sasa? Nashukuru.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi, Muswada ule sasa unashughulikiwa na Wizara ya Kazi na Ajira, utakapokuwa tayari utauletwa Bungeni ili Bunge hili liweze kuujadili.

Swali la pili, ni kweli kwamba katika jibu la msingi nimesema katika kukubaliana na hii Sera, pamoja na kutafuta uwezekano wa kuweka Sheria, tulisema jambo hili lifanywe kwa uangalifu mkubwa kwa sababu zipo taaluma ambazo tayari zinafanya kazi hii. Kwa hiyo, Baraza hili linaweza kuwa lina-*coordinate* kazi zote zinazofanywa za ushauri badala ya kuwa na chombo

kimoja kimoja. Kwa hiyo, kazi yake itakuwa ni ya ushauri zaidi, lakini haitaingilia kazi za kitaaluma ambazo zinafanywa na *institutions* zilizopo kwa hivi sasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani, swali lingine la nyongeza lakini liwe fupi.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Huu Mpango ni mzuri sana kama utatekelezwa kikamilifu. Kwa kutoa ushauri tu nchi ya India katika kipindi cha miaka kama 70 iliyopita, ilianza Mpango kama huu ambapo walitengeneza *"A National Comprehensive Consultancy Board"* ambayo iliweza kufanya uchanganuzi na ushauri yakinifu katika masuala ya uwekezaji katika viwanda vidogo na viwanda vya kati, jambo ambalo lilisaidia sana *industrialisation process* ya China.

Mheshimiwa Spika, kwa nchi yetu ingekuwa ni jambo la msingi sana kama Serikali ingesaidia kutoa huduma hii kwa sababu wapo Watanzania wengi wenye mitaji midogo midogo, lakini wanakosa *access* ya *information* hasa *technical information* ambazo zingewasaidia kuwekeza katika viwanda vidogo vidogo hasa katika *agro processing.*

Je, Mheshimiwa Waziri atakubali kupata ushauri kutoka kwetu tuweze kumshauri zaidi ili aweze kuishauri Wizara inayohusika namna bora ya kutengeneza Mpango huu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, Serikali wakati wowote inapokea ushauri na hakuna hata mara moja inaweza ikasema hatupokei ushauri. Masuala yanayohusiana na uchumi yanasimamiwa na sera zake na Tume ya Mipango na Tume ya Mipango inashirikisha mawazo kutoka Wizara mbalimbali na wadau. Kwa hiyo kama Mheshimiwa Mbowe anao ushauri namshauri haupeleke kwenye Tume ya Mipango na katika Wizara ya Kazi ambayo inashughulikia masuala hayo.

Na. 23

**Ubora wa Shule Binafsi**

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA** aliuliza:-

Hivi sasa kuna mfumko mkubwa wa Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Watu Binafsi:-

(a) Je, wakati Shule na Vyuo vya Serikali havina Walimu wa kutosha Shule za Watu Binafsi zinapataje Walimu?

(b) Je, kuna Idara mahususi inayosimamia Shule na Vyuo vya Watu Binafsi katika uendeshaji na kukagua vyeti vinavyotolewa, ada na michango inayotozwa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 1995, inafafanua wazi kuwa utoaji wa elimu nchini utakuwa kwa ushirikiano wa Serikali na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, Shule zisizo za Serikali zinapata Walimu kwa kutangaza ajira kupitia matangazo ya shule husika kutoka kwenye vyanzo vifuatavyo: Wahitimu kutoka vyuoni, Walimu kutoka nje ya nchi baada ya kutimiza masharti ya ajira yanayotolewa na Serikali na Walimu wa Kujitolea (*Volunteers).* Vile vile baada ya kufungua milango ya ajira kwa Nchi za Afrika Mashariki,

Walimu kutoka nchi jirani wanapata ajira katika Shule zisizo za Serikali. Hali hii ndiyo inasababisha Shule zisizo za Serikali kupata Walimu.

Mheshimiwa Spika, utoaji na ukaguzi wa elimu katika Shule na Vyuo vya Serikali na Visivyo vya Serikali unasimamiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kupitia Idara na Taasisi zake zikiwemo Idara ya Ukaguzi wa Shule, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* na Tume ya Vyuo Vikuu *(TCU)*. Aidha, masuala ya ada na michango kwa Shule na Vyuo vya Ualimu hushughulikiwa na Ofisi ya Kamishna wa Elimu.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(i) Mheshimiwa Spika, katika Shule zetu za Msingi na Shule za Sekondari za Kata na katika Vyuo mbalimbali, tunao upungufu wa Walimu, lakini kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Walimu wanasomeshwa na Serikali. Sasa napenda kuuliza; je, hakuna utaratibu wowote wa kuhakikisha kwamba Walimu hawa kwanza wanajaza nafasi katika Shule za Msingi za Serikali na Shule za Sekondari za Kata kwa kuhakikisha kwamba wale Walimu hawatoki vyuoni moja kwa moja wakaenda kuajiriwa katika Shule Binafsi kabla hawajafundisha katika Shule za Serikali?

(ii) Kwa kuwa ameeleza kwamba Idara ya Ukaguzi na Ofisi ya Kamishna inasimamia masuala yote yanayohusu Shule za Binafsi na Vyuo, lakini tunavyojua ni kwamba hii Idara ya Ukaguzi sasa hivi haifanyi kazi kama inavyotakiwa; shule hazikaguliwi na imeelemewa sana hii Idara ya Ukaguzi. Je, pamoja na juhudi nyingine zinazofanywa kuna mpango gani mkakati mkubwa wa kuhakikisha kwamba Idara ya Ukaguzi inapatiwa nyenzo na watumishi wa kutosha ili shule zote ziweze kukaguliwa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali kuweka utaratibu wa mikataba kwa Walimu wanapomaliza vyuoni kwamba wakae Serikalini kwanza halafu ndipo wapate uhuru wa kufundisha Shule za Binafsi, suala hili linaweza likaendelea kuzungumzwa. Tufahamu tu kwamba, hizi Shule Binafsi kwa Sera ya Elimu ya Mwaka 1995, Serikali ilipokuwa inaruhusu kuweka mpango wa watu binafsi, Mashirika ya Dini na kadhalika kuwa na shule, maana yake wanahitaji Walimu na wale Walimu wanafundisha watoto wetu wa Kitanzania kwa pamoja; na ndiyo maana tunasema tuna ushirikiano wa Shule Binafsi na Shule za Serikali. Shule hizi zimetusaidia sana kutoa elimu bora hapa nchini, lakini suala hili linaweza likazungumzwa tuone namna gani ya kuweka utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu Idara ya Ukaguzi; ni kweli kabisa Idara ya Ukaguzi hata tulipokuwa tunapitisha bajeti mwaka jana hapa ilipata fedha kidogo, lakini tunashukuru mwaka huu kama Mheshimiwa Spika wa Bunge utatupitishia bajeti yetu, tumeiongezea fedha Idara hii ili iweze kufanya kazi vizuri.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona.

Shule nyingi za Kata na Shule za Msingi hazitimizi vigezo na huwa zinapewa vibali. Kwa mfano, unakuta shule nyingi hazina matundu ya kutosha ya vyoo, Walimu wa kutosha na hata madarasa na maabara za kutosha. Kwa nini Serikali inawapa vibali vya kufungua shule zile na hatimaye Wakaguzi wakipita wanazifunga tena; je, hawaoni kuwa huu ni usumbufu?

**SPIKA:** Shule za Msingi au za Sekondari?

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Zote za Msingi na za Sekondari.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo sote tumekuwa tukishuhudia kwamba toka mwaka 2006 Serikali imeweka mkakati wa kuhakikisha angalau kila Kata kuna shule moja ya sekondari ili kuweza kuwasaidia watoto wetu walioko huko vijijini; hili linaendelea kufanyika na Serikali inaendelea kupeleka ruzuku kwenye Halmashauri ili shule hizi ziweze kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, baadhi ya Shule za Kata zinakuwa na upungufu wa vyoo, vitabu na kadhalika, lakini Serikali inaendelea kuweka bajeti. Mwaka jana tumeweka bajeti na shule hizo zimepelekewa fedha. Mwaka huu tumeongeza bajeti kwenye Wizara, shule hizo zitaendelea kuboreka ili angalau kuweza kutoa elimu bora nchini.

**SPIKA:** Kwa sababu ya muda tunaendelea.

Na. 24

**Majengo ya Vituo vya Polisi – Konde na Mtangatuani**

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO** aliuliza:-

Majengo ya Vituo vya Polisi Konde na Matangatuani yamechakaa sana kufikia hatua isiyofaa kwa chombo kuwepo kwenye majengo hayo na hata banda lililojengwa ukamilishaji wake bado unasuasua:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga Jengo la Matangatuani, ambalo lilitaifishwa na kuharibikia mikononi mwa aliyelitaifisha?

(b) Je, utaifishaji wa aina hii umeleta manufaa gani kwa Taifa?

(c) Je, ni lini majengo ya Polisi na Nyumba za Makazi ya Askari wa vituo hivyo yatakarabatiwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Mgogoni, lenye sehemu (a), (b) na (c), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jengo la Matangatuani lilitaifishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kukabidhiwa kwa Jeshi la Polisi mara tu baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya Mwaka 1964. Utaifishaji huo umekuwa na mafanikio makubwa kwa Taifa kwani awali Jengo hilo lilitumiwa na Askari wa FFU wa Mikoa ya Kaskazini na Kusini Pemba.

Mheshimiwa Spika, mpango wa sasa ni kulifanya liwe Kituo cha Polisi cha Daraja C. Serikali imeanza ukarabati wa Jengo la Matangatuani kwa kupaua paa jipya na ukarabati unaendelea. Kwa upande wa Kituo cha Polisi na Nyumba za kuishi Askari Konde, juhudi zinaendelea kufanyika kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali ili kuyafanyia ukarabati majengo hayo.

**MHE. KOMBO HAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

(i) Kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri hayakufanyiwa utafiti; na kwa kuwa kilichotendeka ni ukarabati wa karo ya choo kilichokuwa kimefurika na ambacho walitafuta usaidizi kutoka kwa Kampuni ya MECCO na kwa Mheshimiwa Khatib Said Haji; na kwa kuwa ofisi na nyumba za makazi hazijafanyiwa matengenezo au ukarabati hadi leo hii; ni lini sasa Serikali itafanyia ukarabati nyumba za makazi za polisi ambazo vigae vyake vimeshaanza kuanguka na kuhatarisha hali ya maisha ya wakazi wa pale?

(ii) Kwa kuwa askari waliopo katika Kisiwa cha Konde walijitolea kujenga nyumba kwa kutumia mishahara yao binafsi; na kwa kuwa wameshindwa kuendeleza jengo lile hali ya kuwa limeshafikia kwenye linta; je, Serikali ipo tayari kulimaliza jengo hilo ambalo walinzi wameshafika kwenye linta na wameonesha moyo wa kuisaidia Serikali kwa wao kuweza kujijengea nyumba yao ya kuishi kwa kutumia nguvu zao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kombo, kama ifuatavyo:-

Kwanza, inawezekana kwamba kuna marekebisho ya karo la nyumba wanazokaa askari. Nilichosema kimeanza kufanyika ni kupaua Jengo la Mtangatuani na siyo ukarabati wa jengo ambalo wanakaa askari.

Lini tutatushughulikia? Naomba kumhakikishia Mheshimiwa kuwa, tayari tumefanya makisio ya gharama ambazo zinatakiwa za majengo yote; kituo cha polisi na nyumba wanazokaa askari. Pia nimhakikishie kwamba, mara tukipata fedha kutoka kwenye bajeti, kazi hii itafanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la utayari wa kumaliza jengo ambalo askari wamejitolea, kwanza, naomba nichukue fursa hii kuwapongeza kwa moyo wa uzalendo na Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ipo tayari kulimalizia Jengo hili.

**SPIKA:** Kwa kuwa swali linahusu Mtangatuani, mitamwita Mheshimiwa Mussa Haji Kombo aulize swali la nyongeza. Kuna wengine mtauliza ya kwenu huko wakati hayapo hapa.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja dogo sana.

Naomba kujua thamani ambayo Serikali yetu ya Mapinduzi walitaifisha nyumba hizi kuzitoa kwa watu na leo zikaachwa zinakufa. Je, huku si kututia aibu na uhasama sisi watoto wa Kimapinduzi?

**SPIKA:** Hivi nyumba huwa zinakufa? Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, malengo ya kutaifisha Jengo hili yalikuwa ni mazuri kama yalivyotaifishwa majengo mengine popote nchini. Mara baada ya kutaifishwa Jengo hili, lilitumika vizuri kwa manufaa ya nchi hii kama nilivyosema kwenye jibu la msingi. Kilichotokea ni kwamba, kulifanyika uamuzi wa kuhamisha FFU ambao walikuwa pale na kuwajengea maeneo ya Finya ambako sasa wanakaa. Hata hivyo, ukarabati ambao unafanyika sasa utalirejesha Jengo hili katika hali nzuri, litimize madhumuni ya kutaifishwa kwake na Mapinduzi Matukufu ya Mwaka 1964.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Kwanza, muda umekwisha, tumalize kwanza kazi zilizoko kwenye ratiba yetu.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwakumbusha kwamba, wale wanaotaka wageni wao watambuliwe ni vizuri wakawa wanapeleka kunakohusika. Wakileta vikaratasi wakati mwingine Spika hawezi kutafsiri miandiko yenu halafu pia msome Kanuni inayohusika wageni gani wanatakiwa kutambuliwa hapa.

Wageni walioko Ukumbini leo; kwanza, kuna Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Dkt. Philip Mpango; maana hapa lazima utulie kidogo utofautishe kati ya jina na cheo. Karibu sana.

Yeye ameambatana na Naibu Makatibu Watendaji watano ambao ni Dkt. Longinus Rutasitara, ambaye ni Naibu Katibu Mtendaji – Uchumi Jumla; Eng. Happiness Mgalula ni Naibu Katibu Mtendaji Miundombinu; Ndugu Maduka Kessy, Naibu Katibu Mtendaji Sekta za Uzalishaji;

Ndugu Florence Mwanri, Naibu Katibu Mtendaji Huduma za Jamii; na Ndugu Cliford Tandari, yeye ni Naibu Katibu Mtendaji Biashara za Kimataifa. Kwa hiyo, timu yake Dkt. Mpango imekamilika.

Tunaye pia Mwakilishi Mkazi wa *IMF* hapa Nchini, Ndugu Thomas Baunsgaard; nadhani tutamtambulisha jioni.

Yupo Dkt. Natu Mwamba, Naibu Gavana wa Benki Kuu. Kumbe Wanawake wanaweza hapo.

Yupo Mwenyekiti wa Chama cha *CUF* Taifa, Prof. Ibrahim Lipumba; karibuni sana. *(Makofi*)

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo; wapo wanafunzi 88 kutoka Chuo Kikuu cha *UDOM* wanaotokea Jimbo la Hanang, Mkoa wa Manyara; wasimame walipo. Sasa ninyi wote kama mnatoka Jimbo la Hanang basi mmeshapiga hatua. *(Makofi)*

Kuna wanafunzi wengine kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Jimbo la Misungwi, Mwanza na wao wasimame walipo. Kama wamekosa nafasi basi watapata badaye nafikiri nafasi ipo.

Kuna wanachuo wengine 86 kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo. Hawa ni wageni Mheshimiwa Kilufi, maana Kilufi ni mwanafunzi wa Hombolo siku hizi. Wasimame walipo. Nasikia kati yenu mlitaka kuwa na *appointment* na Waziri wa TAMISEMI, mtafanya *appointment* Waziri akimaliza mambo ya Bajeti hapa, vinginevyo wana kazi za kutosha.

Wapo wanafunzi 52 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaosoma mwaka wa tatu. Haya, tunawatakieni mafanikio mema, mhakikishe mnamaliza vizuri kuja kulitumikia Taifa kwa namna yoyote ile. Ajira hazipo, fikirieni namna ya kujiajiri. Ndiyo ukweli wenyewe, kusoma siyo lazima uajiriwe, unatakiwa ujiajiri mwenyewe.

Tuna wageni watano kutoka Shirikisho la CCM Vyuo Vikuu Morogoro wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Mwashibanda Shibanda. Wako wapi hao? Kama wamekosa nafasi basi baadaye watapata.

Tuna Wabunge wapya wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki waliochaguliwa juzi. Yupo Mheshimiwa Bernard Murunya, Mheshimiwa Twaha Taslima na Mheshimiwa Shy-Rose Bhanji. Ahsanteni sana. Tunarudia tena kuwapongeza kwa uchaguzi wenu na kuapishwa kwenu, huko mlikokwenda bado Taifa linawategemea. *(Makofi*)

Kuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Augustine Mrema ambao ni Sister Inviolata Kessy, Mama Mkuu Shirika la Holy Spirit Sisters Ramulya Moshi; yule pale. Yupo na Sister Yusta Mboya. Hawa wamekuja kututembelea hapa.

Pia kuna Katibu wa Mbunge katika Jimbo la Muleba Kusini, Mheshimiwa Prof. Anna Tibaijuka, anaitwa Denis Charles. Kwa ujumla, wale ambao sijawatambulisha naomba mjisikie mpo nyumbani, huu Ukumbi ni kwa ajili ya wananchi wote wanaopata nafasi kuhudhuria humu ndani. Ni suala la nafasi tu, lakini watu wote wanakaribishwa kuhudhuria.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa John Andrew Chenge, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, wanatakiwa kukutana katika Jengo namba 227, Jengo la Utawala. Sijaona muda, nadhani baada ya Hotuba ya Mipango kusomwa.

Katibu wa Kamati ya Wabunge wa CCM, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM kuwa, kesho tarehe 15, saa tisa alasiri, kutakuwa na kikao kitakachofanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, Mheshimiwa David Silinde, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wa CHADEMA kuwa, leo tarehe 14, saa saba mchana, kutakuwa na kikao kwenye Ofisi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Jengo la Utawala.

Mwenyekiti wa *APNAC*, Mheshimiwa dkt. Mary Mwanjelwa, anaomba niwatangazie Wanachama hai wa *APNAC*; *APNAC* ni *Africa Parliamentarians Network Against Corruption* kuwa, kesho tarehe 15, saa tatu asubuhi, kutakuwa na mafunzo juu ya rushwa, yatakayofanyika katika Ukumbi wa New Dodoma Hotel. Wanachama hai tu ndiyo wanaoalikwa kuhudhuria mafunzo hayo. Aidha, Kamati Tendaji ya *APNAC* inaombwa kukutana leo tarehe 14 katika Ukumbi Namba 231, Ghorofa ya Pili, Jengo la Utawala, mara baada ya Serikali kusoma Bajeti yake jioni.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mawili; tumekubaliana katika Kamati ya Uongozi, tutakapoanza mjadala wa Bajeti hizi, hakuna nafasi ya Wabunge kwenda kukaa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu pale kuongea. Ninamaanisha hapa ndani ya Bunge. Sababu kubwa ya kufanya hivyo ni kwamba, Waziri Mkuu anatakiwa asikilize yale mnayoyasema hapa kama Serikali ikibidi iyachukulie hatua. Sasa wengine wanaenda kukaa pale *half an hour* wanaendelea kuongea. Jamani hapa siyo nafasi ya kuongea, mkitaka fanyeni *appointment* ana ofisi hapa. Mawaziri ni wale ambao wana suala ambalo linataka *consultation* mara moja.

Mawaziri nao pia hawaruhusuwi. Mimi nadhani kama ni *consultation* huwezi kutumia *more than 30 minutes.* Kama unataka *30 minutes* kamtafute ofisini. Kwa sababu hii si tabia njema, Waziri Mkuu anakaa humu kusikiliza yale mnayoongea halafu Serikali ikayafanyie maamuzi. Naomba hilo mlizingatie.

Wiki hii tumekuwa na uchaguzi wa viti mbalimbali. Waheshimiwa Wabunge kama mnavyofahamu, kutokana na uteuzi wa Wabunge na baadhi ya Mawaziri wapya uliofanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mujibu wa Masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 66 (1) (a), baadhi ya waliokuwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu waliteuliwa kuwa Mawaziri. Hivyo, ili kujaza nafasi hizo, Kamati zilfuatazo zilifanya Uchaguzi wa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti kwa mujibu wa Fasili ya Kumi ya Kanuni ya 113 ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Waliochaguliwa ni Mheshimiwa John Andrew Chenge, alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi alijiuzulu mwenyewe.

Mheshimiwa Sylvester Mabumba, alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo na Mheshimiwa Philipa Geofrey Mturano, alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Selemani Zedi, alichaguliwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa John Paul Lwanji, alichaguliwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Kutokana na Uchaguzi wa Wenyeviti hao kukamilika kwa mujibu wa Kanuni ya 11 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Uongozi hapo itajumuisha Wenyeviti na Makamu Wenyeviti, inatarajia kukutana leo tarehe 14 Juni, 2012 mara baada ya Hotuba ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika Ukumbi wa Spika kupendekeza jina la Mwenyekiti wa Bunge ili tuweze kujaza nafasi iliyoachwa wazi na Mheshimiwa George Simbachawene, ambaye aliteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

Nimeletewa ki-*note* hapa kwamba, lile tangazo lingine niliambiwa Kamati ya Wabunge wa CCM ni saa tisa na huyu mwingine anasema ni kesho saa tano, kwa hiyo, mabadiliko hayo naomba myazingatie.

Waheshimiwa Wabunge, nimemaliza matangazo, tunaendelea na shughuli zingine. Katibu, hatua inayofuata.

## MWONGOZO WA SPIKA

**SPIKA:** Kulikuwa na mwongozo wa Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuomba mwongozo wa Kiti chako. Ninaomba mwongozo juu ya jambo lililotokea wakati wa Kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu. Kanuni ya 1(2)(6) ya Kanuni za Bunge hili inayohusu utaratibu wa maswali kwa Waziri Mkuu, inaelekeza kwamba maswali atakayoulizwa Waziri Mkuu, yatakuwa ni yale yanayohusu Sera za Serikali au jambo lolote lenye manufaa na maslahi kwa jamii na Taifa lililo chini ya madaraka na mamlaka ya kazi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu, ameulizwa ni lini ataanza kugawa nakala milioni nne za Katiba na ameulizwa lini ataenda Jimbo la Vunjo.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wa Kiti chako kama maswali haya yanakidhi matakwa ya Kanuni ya Kwanza, Kanuni Ndogo ya Pili ya Nyongeza ya Sita na kama haya si matumizi mabaya ya muda wa maswali kwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, mimi naona yanakidhi kwa sababu mbili; ziara ya Vunjo ilikuwa ya wananchi wa kule na bahati nzuri Waziri Mkuu anaifahamu, maana kuna wakati unaenda kuuliza swali ambalo *seriously* ni la Sekta fulani, *you do not expect* kwamba, *Prime Minister* anakuwa anajua; lakini hili alikuwa anajua na Wananchi wa Vunjo nao siyo wachache ni wengi.

Nakala za Katiba hiyo ndiyo kabisa ya nchi nzima ni ya Kitaifa kabisa. Kwa hiyo, nafikiri yanakidhi. Kuhusu usambazaji wa Katiba ni lazima Waziri Mkuu afahamu, hili ni suala la Kitaifa na linaendelea hivi sasa, ndiyo maana tukaruhusu haya maswali yajibiwe kwa sababu nilijua kabisa atakuwa na taarifa ya aina fulani; kwa hiyo yanakidhi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Aah! Hatuwezi kuendelea na mchezo wa mwongozo, hapana tunaendelea na kazi. Katibu, hatua inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2012/2013

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likae kama Kamati kwa ajili ya kupokea na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2011 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2012/13. Taarifa hizi ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao ulipitishwa na Bunge hili mwezi Juni, 2011.

Pamoja na hotuba hii, nawasilisha Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2011 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2012/13.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutumia nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii ya kuwasilisha taarifa hizi. Vilevile, napenda kumpongeza Mheshimiwa Andrew John Chenge, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Kamati imetupatia maoni na ushauri ambao umesaidia kuboresha taarifa hizi ninazoziwasilisha. Tunaahidi kuipatia Kamati ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, Serikali itaendelea kuzingatia maoni na maelekezo yanayotolewa na Kamati pamoja na Bunge hili katika hatua mbalimbali za uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Wabunge wapya walioteuliwa na Rais hivi karibuni. Waheshimiwa hao ni pamoja na Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omari Kigoda - Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Balozi Khamis Sued Kagasheki - Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mhandisi Christopher Kajoro Chiza - Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe - Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Fenella Ephraim Mukangara - Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa - Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Prof. Sospeter Muhongo - Mbunge wa Kuteuliwa na Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa January Yusuf Makamba - Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Dkt. Seif Seleman Rashid - Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Stephen Julius Maselle na Mheshimiwa George Boniface Simbachawene - Naibu Mawaziri wa Nishati na Madini.

Wengine ni Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba - Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Binilith Satano Mahenge - Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Angela Kairuki - Naibu Waziri wa Sheria na Katiba, Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla - Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Saada Omari Mkuya na Mheshimiwa Janeth Mbene - Wabunge wa Kuteuliwa na Naibu Mawaziri wa Fedha. Aidha, nampongeza Mheshimiwa James Mbatia, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge. Ninaamini uteuzi wao umezingatia umahiri na umakini katika utendaji kazi ndani na nje ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa, kwa ushirikiano aliotoa katika kuandaa na kufikisha hatua hii ya Hotuba. Aidha, nawashukuru Wataalam kutoka Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango chini ya Uongozi wa Ndugu Ramadhani Khijjah - Katibu Mkuu Hazina na Dkt. Philip Mpango - Katibu Mtendaji Tume ya Mipango. Vilevile napenda niwashukuru Wafanyakazi wote wa Taasisi mbili hizi pamoja na Idara na Taasisi zilizo chini yao kwa kufanikisha uandaaji wa Hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno ya shukrani, naomba sasa nielezee kwa muhtasari Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika kipindi cha mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Shirika la Fedha Duniani, Uchumi wa Dunia ulikua kwa asilimia 3.9 mwaka 2011 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.3 mwaka 2010. Kiwango kidogo cha ukuaji wa uchumi kilitokana na mtikisiko wa uchumi katika nchi za Ulaya uliosababishwa na miundo tete ya kifedha *(financial fragilities),* hususan hasara katika Sekta ya Kibenki, kuongezeka kwa nakisi ya bajeti kwa nchi nyingi za Ulaya na kukosekana kwa hali ya utulivu katika nchi za Kiarabu.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ukuaji wa uchumi katika Bara la Afrika kilipungua na kuwa asilimia 2.7 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 4.6 mwaka 2010 kutokana na hali mbaya ya kisiasa iliyojitokeza katika nchi za Kaskazini mwa Afrika. Kiwango cha ukuaji wa uchumi wa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara nacho kilipungua na kuwa asilimia 5.1 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, ukuaji halisi wa Pato la Taifa ulikuwa asilimia 6.4 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2010. Kushuka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kulitokana hasa na hali mbaya ya ukame iliyojitokeza katika baadhi ya maeneo nchini ambapo Sekta ya Kilimo iliathirika zaidi. Aidha, upungufu wa umeme ulichangia kushuka kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani na shughuli nyingine zinazohitaji umeme. Pamoja na kushuka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi, Sekta za Mawasiliano, Huduma za Fedha, Ujenzi na Elimu zilikuwa na ukuaji wa viwango vya juu kati ya asilimia 6 hadi asilimia 19.

Mheshimiwa Spika, pamoja na baadhi ya sekta kukua kwa viwango vya juu, ukuaji huu wa uchumi haukupunguza umaskini kwa kiwango kikubwa kama ilivyotarajiwa kwa sababu sekta zilizokua haraka hazitoi ajira kwa wananchi wengi hasa waliopo vijijini ambao wanategemea kilimo. Kasi ya ukuaji katika Sekta ya Kilimo ambayo inaajiri takriban asilimia 75 ya nguvukazi nchini ilipungua kutoka asilimia 4.2 mwaka 2010 hadi 3.6 mwaka 2011 wakati kasi ya ongezeko la watu imeendelea kuwa juu (asilimia 2.9).

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011, Pato la Taifa lilikuwa shilingi trilioni 37.5 kwa bei za mwaka 2011. Kutokana na idadi ya watu Tanzania Bara kukadiriwa kuwa watu milioni 43.2 mwaka 2010 na watu milioni 44.5 mwaka 2011, pato la wastani la kila mtu lilikuwa shilingi 869,436.3 mwaka 2011 ikilinganishwa na shilingi 770,464.3 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 12.8.

Mheshimiwa Spika, wastani wa mfumko wa bei kwa mwaka 2011 uliongezeka hadi asilimia 12.7 kutoka asilimia 5.5 mwaka 2010. Kuongezeka kwa kasi ya upandaji bei kulichangiwa na kuendelea kupanda kwa wastani wa bei za mafuta ya petroli katika Soko la Dunia; upungufu wa mvua za vuli katika robo ya nne ya mwaka 2010 ambao ulipunguza mavuno; kupanda kwa bei ya umeme, gesi, mafuta ya kupikia, mchele na sukari; upungufu wa nishati ya umeme; kuporomoka kwa thamani ya shilingi; na upungufu wa chakula katika Kanda ya Afrika Mashariki kutokana na hali ya ukame. Mahitaji ya chakula katika nchi za jirani za Kenya, Uganda, Somalia na Sudani ya Kusini yameongeza kasi ya upandaji wa bei za chakula na sukari hapa nchini. Hadi Aprili 2012, mfumko wa bei ulikuwa asilimia 18.7 ikilinganishwa na asilimia 8.6 Aprili 2011.

Mheshimiwa Spika, mfumko wa bei ambao haujumuishi chakula na nishati, kwa mwaka ulioishia Aprili 2012 uliongezeka hadi asilimia 9.0 kutoka asilimia 5.7 Aprili 2011. Hii ilitokana na kuongezeka kwa bei za mafuta, gharama za usafirishaji na kuongezaka kwa mfumko wa bei katika nchi zinazofanya biashara na Tanzania hususan China na India *(imported inflation*). Mfumko wa bei ya chakula uliongezeka na kufikia asilimia 24.7 Aprili 2012 kutoka asilimia 9.2 Aprili 2011. Mfumko wa bei ya nishati uliongezeka hadi asilimia 24.9 Aprili 2012 kutoka asilimia 22.1 kwa mwaka ulioishia Aprili 2011.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na mfumko wa bei, Serikali ilichukua hatua zifuatazo: Kuhakikisha usambazaji wa chakula katika maeneo yenye uhaba wa chakula; kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula; kuendelea kuimarisha hifadhi ya chakula kwa kuongeza ununuzi wa mazao ya chakula; kuongeza uzalishaji wa umeme wa megawati 342 chini ya Mpango wa Dharura; kupandisha kiwango cha riba ya Benki Kuu inayotozwa kwa taasisi za fedha kutoka asilimia 7.58 hadi asilimia 12.58; na kupandisha kiwango cha amana ambacho Benki za Biashara zinapaswa kuhifadhi Benki Kuu kutoka asilimia 20 hadi asilimia 30. Hatua hizo zimeweza kupunguza kasi ya upandaji bei kutoka asilimia 19.8 Desemba 2011 hadi asilimia 18.7 Aprili 2012.

Mheshimiwa Spika, kufikia Desemba 2011, ujazi wa fedha na karadha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni 2,008.7 sawa na asilimia 18.2, ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 2,232.4 Desemba 2010. Hadi kufikia Machi 2012, ukuaji wa M3 uliongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni 1,767.6 sawa na asilimia 15.7. Ukuaji huu wa M3 ulikuwa chini ya lengo la ukuaji wa asilimia 21.3 Desemba 2011 na asilimia 23.8 Machi 2012. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa asilimia 15.0 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 1,205.8 Desemba 2011 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 1,438.7 Desemba 2010. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa asilimia 14.8 Machi 2012 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 1,211.8. Kasi ndogo ya ukuaji wa ujazi wa fedha ilitokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa rasilimali katika fedha za kigeni kwenye benki ikilinganishwa na ongezeko la ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi 2012, kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kwa asilimia 21.9 ikilinganishwa na asilimia 23.3 Machi 2011. Ongezeko hili liliendа sambamba na kuongezeka kwa rasilimali za fedha za ndani *(net domestic assets*) kwenye benki pamoja na kupungua kwa ukuaji wa rasilimali za fedha za kigeni *(net foreign assets*) kwenye benki. Sehemu kubwa ya mikopo hii ilielekezwa katika shughuli binafsi asilimia 21.9; biashara asilimia 19.9; uzalishaji bidhaa viwandani asilimia 11.9; kilimo asilimia 11.8; na usafiri na mawasiliano asilimia 7.9.

Mheshimiwa Spika, wastani wa viwango vya riba za mikopo katika benki za biashara ulipungua kidogo hadi asilimia 14.21 Desemba 2011 kutoka asilimia 14.92 Desemba 2010. Vile vile, wastani wa riba za kukopa kwa muda mfupi (hadi mwaka mmoja) ulipungua kutoka asilimia 14.37 Desemba 2010 hadi asilimia 13.73 Desemba 2011. Aidha, wastani wa jumla wa riba za amana za akiba uliongezeka kutoka asilimia 6.09 Desemba 2010 hadi asilimia 7.12 Desemba 2011. Vile vile, wastani wa riba za amana za akiba za muda maalum (miezi 12) uliongezeka hadi asilimia 9.99 Desemba 2011 kutoka asilimia 8.45 Desemba 2010.

Kutokana na mwelekeo huo wa riba, tofauti baina ya viwango vya riba za amana na mikopo (mwaka mmoja) ilipungua kutoka asilimia 7.26 Desemba 2010 hadi asilimia 4.59 Desemba 2011. Tofauti hiyo inatokana na kuongezeka kwa ushindani kwa mabenki katika utoaji wa huduma. Aidha, wastani wa riba za amana za akiba uliongezeka na kufikia asilimia 2.90 Desemba 2011 kutoka asilimia 2.43 Desemba 2010.

Mheshimiwa Spika, thamani ya Shilingi ya Tanzania kwa mwaka 2011 ilishuka kwa asilimia 10.3 hadi wastani wa shilingi 1,579.5 kwa dola moja ya Kimarekani ikilinganishwa na wastani wa shilingi 1,432.3 mwaka 2010. Mwishoni mwa Desemba 2011, bei ya Dola ya Kimarekani ilikuwa na thamani ya shilingi 1,587.6 ikilinganishwa na shilingi 1,469.9 mwishoni mwa Desemba 2010. Kushuka kwa thamani ya shilingi kulitokana na kushuka kwa mauzo nje ikilinganishwa na uagizaji nje; tofauti ya mfumko wa bei kati Tanzania na nchi inazofanyanazo biashara; ulanguzi au kuotea katika soko la fedha za kigeni *(market speculation);* na kuimarika kwa Dola ya Kimarekani dhidi ya Sarafu za Mataifa mengine. Hadi Machi, 2012 thamani ya shilingi ilikuwa wastani wa shilingi 1,588 kwa Dola moja ya Kimarekani.

Mheshimiwa Spika, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje iliongezeka kwa asilimia 17.1 mwaka 2011 na kufikia dola milioni 6,796.3 kutoka dola milioni 5,805.0 mwaka 2010. Ongezeko la mauzo nje lilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa asilia (Kahawa, Tumbaku, Karafuu na Korosho) na bidhaa zisizo asilia hasa madini na mapato yatokanayo na huduma za utalii na usafirishaji. Uagizaji wa bidhaa na huduma uliongezeka kwa asilimia 33.0 kutoka Dola za Kimarekani milioni 9,017.9 mwaka 2010 hadi dola milioni 11,992.3 mwaka 2011. Ongezeko hilo lilitokana hasa na uagizaji wa mafuta na mitambo kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la umeme.

Mheshimiwa Spika, hadi Desemba 2011, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 3,761.2 ikilinganishwa na dola milioni 3,948.0 Desemba 2010, sawa na upungufu wa asilimia 4.7. Kiasi hiki cha akiba ya fedha za kigeni kwa mwaka 2011 kilikuwa na uwezo wa kuagiza bidhaa na huduma kwa miezi 3.8 ikilinganishwa na miezi 5.3 iliyofikiwa mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011, thamani ya mitaji ya kigeni ya moja kwa moja iliongezeka kwa asilimia 97 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 854.2 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 433.9 mwaka 2010. Ongezeko hili kubwa lilitokana na uwekezaji mkubwa wa utafiti wa gesi katika Mikoa ya Mtwara na Pwani ambao uligharimu zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 300. Sekta zilizoongoza katika kupokea idadi kubwa ya miradi kutoka nje ni uzalishaji wa bidhaa viwandani, utalii, majengo ya biashara na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012, mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri, yalifikia shilingi bilioni 5,180.6, sawa na asilimia 98 ya makisio ya kukusanya shilingi bilioni 5,217.2. Kati ya makusanyo hayo, mapato ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 4,765.5, sawa na asilimia 104 ya makadirio ya shilingi bilioni 4,585.5. Ongezeko hili lilitokana na hatua za kiutawala zilizochukuliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mapato yasiyo ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 272.1, sawa na asilimia 57 ya lengo la shilingi bilioni 473.5. Mapato ya Halmashauri yalikuwa shilingi bilioni 143 sawa na asilimia 60 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 237.8. Ukusanyaji huo mdogo wa mapato yasiyo ya kodi ulitokana na kushindwa kwa Mashirika na Taasisi kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kama ilivyotarajiwa. Serikali inakusudia kufanya tathmini ya mifumo ya ukusanyaji mapato yasiyo ya kodi kwenye Wizara zenye utaratibu wa kukusanya maduhuli kwa lengo la kuiboresha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, matumizi ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 9,439.4, sawa na asilimia 87.0 ya makadirio. Matumizi halisi kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012 yalikuwa shilingi bilioni 8,676.8, sawa na asilimia 97.5 ya makadirio ya shilingi bilioni 8,895.8.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012, Serikali ilipokea misaada na mikopo ya kibajeti ya jumla ya shilingi bilioni 735 ambazo ni asilimia 85 ya makadirio ya shilingi bilioni 869.4 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, deni la Taifa limeongezeka kufikia shilingi bilioni 20,276.6 katika kipindi kilichoishia Machi 2012 kutoka shilingi bilioni 17,578.9 Machi 2011, sawa na ongezeko la asilimia 15.4. Kati ya fedha hizo, shilingi 15,306.9 bilioni ni deni la nje ambapo shilingi bilioni 12,342.5 ni deni la umma na kiasi kilichosalia ni deni la sekta binafsi. Hadi Machi 2012, deni la ndani lilifikia shilingi bilioni 4,969.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 4,496.5 Machi 2011, sawa na ongezeko la asilimia 10.5.

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali itakayosomwa leo jioni itabainisha kwa kina mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2011/12 na makadirio ya mwaka 2012/13.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa Kiuchumi Kikanda na Kimataifa, uliendelea kuimarika na hivyo kuendelea kulijengea Taifa mazingira mazuri ya shughuli za kiuchumi na kijamii. Katika mwaka 2011, Miradi mbalimbali ya Maendeleo ya Kikanda iliendelea kutekelezwa ikiwemo ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*), ambayo ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 90; ujenzi wa Barabara ya Arusha - Namanga - *Athi River* umefikia asilimia 90: na Tanga - Horohoro asilimia 67.5; na hati ya makubaliano *(MoU)* ya Mradi wa Kufua Umeme ulioko Murongo/Kikagati imesainiwa kati ya Tanzania na Uganda.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa biashara baina ya Tanzania na nchi za Kikanda umezidi kuimarika ambapo mauzo nje yaliongezeka kwa asilimia 75.3 kufikia Dola za Kimarekani milioni 1,222.4 kwa nchi za SADC na asilimia 12.8 kufikia Dola za Kimarekani milioni 368.4 kwa nchi za *EAC*. Uagizaji kutoka nchi za *SADC* na *EAC* nao pia uliongezeka kufikia Dola za Kimarekani milioni 1,199.7 na Dola za Kimarekani milioni 385.3, sawa na ongezeko la asilimia 36.6 na asilimia 30.3 kwa mtiririko huo. Bidhaa zilizochangia ongezeko hilo ni pamoja na dhahabu, vyandarua, mchele, saruji, chai na vyombo vya majumbani.

Mheshimiwa Spika, napenda nielezee kwa ufupi ukuaji wa uchumi katika sekta mbalimbali. Mawaziri wa wizara husika wataeleza kwa kina maendeleo katika maeneo yao; hivyo nitatoa tathmini ya kiujumla tu ya maendeleo katika baadhi ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, shughuli za kiuchumi za kilimo zinazojumuisha mazao; mifugo na misitu na uwindaji zilikua kwa kiwango cha asilimia 3.6 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 4.2 mwaka 2010. Upungufu huu ulitokana na kuchelewa kwa mvua za msimu kwa mwaka 2009/10 ambazo ziliathiri uzalishaji wa mazao. Aidha, mchango wa shughuli za kiuchumi za kilimo ulikuwa asilimia 23.7 ya Pato la Taifa mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 24.1 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, shughuli za kiuchumi katika uvuvi zilikua kwa kiwango cha asilimia 1.2 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 1.5 mwaka 2010. Kushuka huku kwa ukuaji katika sekta ndogo ya uvuvi kulitokana na matumizi ya zana duni za uvuvi, uharibifu wa mazalia ya samaki na kuongezeka kwa ushindani katika soko la dunia. Mchango wa shughuli za uvuvi katika Pato la Taifa uliendelea kubakia asilimia 1.4 kama ilivyokuwa mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Viwanda na Ujenzi inajumuisha uzalishaji bidhaa viwandani; umeme na gesi; usambazaji wa maji; madini; uchimbaji wa mawe na ujenzi. Shughuli za kiuchumi katika Sekta ya Viwanda na Ujenzi zilikua kwa kiwango cha asilimia 6.9 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 8.2 mwaka 2010. Kupungua kwa ukuaji kulitokana na ukuaji mdogo katika shughuli ndogo zote. Mchango wa shughuli za kiuchumi za viwanda na ujenzi katika Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 22.4 mwaka 2010 hadi asilimia 22.7 mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani zilikua kwa kiwango cha asilimia 7.8 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 7.9 mwaka 2010. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kulitokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji kutokana na upungufu wa nishati ya umeme na kuongezeka kwa gharama za uagizaji wa malighafi za viwandani hususan mafuta. Aidha, mchango wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani katika Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 9.0 mwaka 2010 hadi asilimia 9.3 mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, sekta ndogo ya umeme na gesi ilikua kwa asilimia 1.5 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 10.2 mwaka 2010. Upungufu huu ulitokana na kupungua kwa kina cha

maji katika mabwawa ya Mtera na Kihansi; uchakavu wa mitambo ya umeme; na ukarabati wa mitambo ya Songas uliosababisha kusimama kwa uzalishaji wa umeme wa gesi kwa muda. Mchango wa shughuli za kiuchumi katika umeme na gesi ulikuwa asilimia 1.8 katika Pato la Taifa mwaka 2011 kama ilivyokuwa mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, sekta ndogo ya ujenzi ilikua kwa kiwango cha asilimia 9.0 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 10.2 mwaka 2010. Ukuaji huo ulichangiwa hasa na kuongezeka kwa shughuli za ujenzi wa: barabara na madaraja; majengo ya kuishi na yasiyo ya kuishi; na upanuzi wa miundombinu ya maji na barabara. Mchango wa shughuli za ujenzi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.0 mwaka 2011 kama ilivyokuwa mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, sekta ndogo ya usambazaji maji ilikua kwa kiwango cha asilimia 4.0 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 6.3 mwaka 2010. Kasi ndogo ya ukuaji ilitokana na ukame uliotokea katika maeneo mengi nchini na uchakavu wa mitambo. Mchango wa shughuli za maji katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 0.3 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 0.4 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, sekta ya utoaji huduma inajumuisha biashara na matengenezo; uchukuzi; mawasiliano; hoteli na migahawa; utawala; elimu; afya; huduma za fedha na bima; na upangishaji wa majengo. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika utoaji huduma kilikuwa asilimia 7.9 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 8.2 mwaka 2010. Mchango wa shughuli za utoaji huduma katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 44.0 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 43.9 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Sekta Ndogo ya Mawasiliano katika mwaka 2011 iliendelea kuwa na kiwango kikubwa zaidi cha ukuaji ikilinganishwa na shughuli nyingine za kiuchumi. Kiwango cha ukuaji katika shughuli za mawasiliano kilikuwa asilimia 19.0 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 22.1 mwaka 2010. Ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa wateja wa huduma za mawasiliano ya simu za mkononi. Mchango wa shughuli za mawasiliano katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 2.2 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 2.1 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, shughuli za biashara na matengenezo zilikua kwa asilimia 8.1 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 8.2 mwaka 2010. Ukuaji huo ulichangiwa na kuimarika kwa biashara ya kikanda. Upungufu wa umeme uliathiri shughuli za biashara na matengenezo na kupunguza kasi ya ukuaji katika sekta. Mchango wa shughuli ndogo za biashara na matengenezo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 12.2 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 12.1 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, viwango vya ukuaji katika shughuli za utoaji huduma za elimu na afya vilikuwa asilimia 7.4 na 5.4 mwaka 2011, ikilinganishwa na asilimia 7.3 na 6.9 mwaka 2010 kwa mtiririko huo. Ukuaji katika shughuli za utoaji huduma za elimu ulitokana na kuendelea kwa utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM II); Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES); na kuongezeka kwa ajira mpya za walimu. Kwa upande wa shughuli za huduma za afya, ukuaji ulichangiwa na utekelezaji wa Programu za Chanjo, Malaria, Kifua Kikuu na VVU/UKIMWI. Mchango wa shughuli za huduma za afya katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.7 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 1.6 mwaka 2010. Aidha, katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo, sekta ndogo ya elimu ilikuwa ikichangia asilimia 1.4 katika Pato la Taifa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2002, inakadiriwa kuwa idadi ya watu Tanzania kwa mwaka 2011 ilikuwa watu milioni 44.5 ikilinganishwa na watu milioni 43.2 mwaka 2010. Kati yao, wanawake walikuwa milioni 22.6, sawa na asilimia 50.7 na wanaume walikuwa milioni 21.9. Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na watu milioni 43.2 sawa na asilimia 97.0 na Tanzania Zanzibar ilikuwa na watu milioni 1.3. Mgawanyo wa watu unaonesha kuwa asilimia 73.3 wanaishi vijijini na asilimia 26.7 wanaishi mijini.

Mheshimiwa Spika, msongamano wa watu kimkoa unaonesha kuwa Mkoa wa Dar es Salaam, una msongamano mkubwa wa watu (2,294) kwa kilometa moja ya mraba, ukifuatiwa na Mwanza watu 186, Kilimanjaro watu 126 na Mara watu 87. Mkoa uliokuwa na kiwango kidogo cha msongamano wa watu ni Lindi yenye watu 14 kwa kilometa ya mraba. Kwa upande wa Tanzania

Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na msongamano mkubwa wa watu 2,152 kwa kilometa ya mraba na Mkoa wa Kusini Unguja ulikuwa na msongamano mdogo wa watu 135 kwa kilometa ya mraba.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI kwa kutoa huduma za tiba na matunzo kwa wagonjwa wa UKIMWI, ushauri nasaha na upimaji wa Virusi vya UKIMWI kwa hiari. Aidha, Serikali iliendelea kuboresha huduma hizi kwa kuhakikisha kuwa dawa za kupunguza makali ya VVU zinapatikana katika vituo vya kutoa huduma. Mwaka 2011, watu milioni 14.9 walipata ushauri nasaha na kupima Virusi vya UKIMWI kwa hiari ikilinganishwa na watu milioni 8.9 mwaka 2010. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa watoa mafunzo mbalimbali na ushauri nasaha na kuongezeka kwa vituo vya kutoa ushauri nasaha na vipimo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011, Serikali iliendelea kuwahimiza wawekezaji kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira katika uwekezaji kwa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kabla na baada ya kutekeleza Miradi yao. Katika kipindi hiki, jumla ya Miradi ya Maendeleo 467 ya uwekezaji ilisajiliwa kwa ajili ya kufanyiwa TAM. Kati ya Miradi hiyo, Miradi 163 ilipata Hati za TAM baada ya kukidhi vigezo ikilinganishwa na Miradi 220 mwaka 2010. Aidha, kati ya Miradi iliyopewa Hati za TAM mwaka 2011, Miradi 44 ilikuwa ya mawasiliano; 36 ya viwanda; 28 ya nishati; 17 ya miundombinu; 16 ya ujenzi na uendelezaji kwenye vivutio vya utalii; 12 maji; 7 ya uchimbaji wa madini; na Miradi mitatu ilikuwa ya misitu na kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Serikali iliandaa Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi. Mkakati huu wa miaka mitano unaweka mikakati ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kusaidia kupunguza gesijoto.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inaendelea kuchukua hatua katika kufikia Malengo ya Milenia ifikapo mwaka 2015, lakini kuna baadhi ya maeneo ambayo uwezekano wa kufikia malengo kwa muda uliobaki ni mdogo hususan katika viashiria vya afya. Vifo vya watoto wachanga na walio na umri wa chini ya miaka mitano viliendelea kupungua japo siyo kwa kasi inayoweza kufikia Malengo ya Milenia.

Serikali inaendelea na jitihada za kuhakikisha kwamba huduma za afya kwa ujumla wake zinaboreshwa. Kuhusiana na hatua za kudhibiti malaria, mwaka 2011, Serikali ilisambaza vyandarua bila malipo katika kaya katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Jumla ya vyandarua vyenye dawa milioni 17.6 viligawiwa katika kampeni hii. Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza dawa za kuharibu mazalia ya mbu wanaoeneza ugonjwa wa malaria kinachojengwa Kibaha katika Mkoa wa Pwani. Hatua hizo, pamoja na punguzo la bei za dawa ya mseto ya kutibu malaria, ziliimarisha udhibiti wa ugonjwa wa malaria.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kilipungua hadi asilimia 2.4 kwa vijana wenye umri kati ya miaka 15 – 24 ikilinganishwa na lengo la mwaka 2015 la asilimia 1.2. Aidha, kulikuwa na maendeleo mazuri katika viashiria vinavyohusiana na usawa wa jinsia na elimu lakini changamoto iliyopo ni utoaji wa elimu bora hususan kuimarisha mazingira ya kujifunza na kufundishia. Changamoto nyingine ni kuongeza kasi ya kupunguza umaskini wa wananchi wanaoishi kwa kiwango cha chini ya dola moja kwa siku. Serikali pia inaendelea kuboresha huduma za upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini na ujenzi wa nyumba bora.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka mmoja wa utekelezaji wa MKUKUTA-II, matokeo kadhaa yamepatikana kutokana na utekelezaji wa programu mbalimbali. MKUKUTA-II kama ulivyokuwa ule wa kwanza unatekelezwa kupitia programu na michakato ya kitaifa, kisekta na ile iliyo chini ya Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na ukuaji wa uchumi, kuongezeka kwa pato la wastani la kila mtu kutoka shilingi 770,464.3 mwaka 2010 hadi kufikia shilingi 869,436.3 mwaka 2011, kuongezeka kwa uwiano wa kujitosheleza kwa chakula kutoka asilimia 102 mwaka 2010 hadi asilimia 112 mwaka 2011, kuongeza uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma katika ngazi zote, kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa na kuboresha sekta za elimu, afya na maji. Kiwango cha ukuaji wa uchumi mwaka 2011 kilikuwa

asilimia 6.4 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2010. Ukuaji huu ni chini ya shabaha ya MKUKUTA-II ya kuwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 8 hadi asilimia 10 ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana, changamoto na mambo yanayohitaji mjadala zaidi na kupewa kipaumbele kwa ajili ya kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika kipindi cha utekekelezaji wa Awamu ya Pili ya MKUKUTA, yamechambuliwa kwa kina katika taarifa ya utekelezaji kwa mwaka 2010/11.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011, Serikali iliendelea na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Kupitia Mifuko yake ya uwezeshaji, iliendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wananchi. Mifuko hii ni pamoja na Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi uliotoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 7.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 4.6 zilizotolewa mwaka 2010, Mfuko wa Rais wa kutoa mikopo kwa wananchi wa kipato cha chini uliotoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 6.8 kwa walengwa 167,372 na Mfuko wa kuwezesha wakulima ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 49.45 kwa wakulima na wasambazaji wa pembejeo za kilimo. Aidha, Serikali kupitia Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 49.23 kwa wajasiriamali 72,912 ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 47.14 iliyotolewa kwa wajasiriamali 72,179 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea mapitio ya hali ya uchumi kwa mwaka 2011, sasa naomba nielezee kwa muhtasari wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2012/13.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kuwa katika Bunge la mwezi Aprili 2012, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, ilileta mapendekezo ya Mfumo wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2012/13. Hotuba hii ninayoiwasilisha inafafanua kwa muhtasari Misingi, Malengo na Miradi ya Maendeleo ambayo Serikali inakusudia kuitekeleza katika mwaka 2012/13 kwa kuzingatia mfumo wa Mpango uliopitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Uchumi Jumla na Maendeleo ya Jamii na Mpango wa Maendeleo katika mwaka 2012/13 yatakuwa yafuatayo:-

(i) Pato halisi la Taifa litakua kwa asilimia 6.8 mwaka 2012 na kuendelea kuongezeka hadi asilimia 8.5 mwaka 2016;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya upandaji bei ili ipungue hadi viwango vya tarakimu moja kutoka asilimia 18.7 Aprili 2012;

(iii) Kuongeza mapato ya ndani yafikie asilimia 16.9 ya Pato la Taifa Juni 2012 na asilimia 18.0 mwaka 2012/13;

(iv) Kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) katika wigo wa asilimia 18.0 mwishoni mwa Juni 2013, utakaowiana na malengo ya ukuaji wa uchumi na kasi ya upandaji bei;

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni itakayoweza kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje kwa kipindi kisichopungua miezi 4.5;

(vi) Kuongeza mauzo ya bidhaa nje kufikia asilimia 23.1 mwaka 2011/12 na asilimia 24.3 mwaka 2012/13;

(vii) Kupunguza tofauti ya viwango vya riba za akiba na zile za kukopa;

(viii) Mikopo kwa sekta binafsi ikue kwa kiwango cha asilimia 20.0 Juni 2013 sambamba na jitihada za kudhibiti mfumko wa bei; na

(ix) Kuimarisha thamani ya shilingi na kuwa na kiwango imara cha ubadilishaji wa fedha kitakachotokana na mwenendo wa soko la fedha.

Mheshimiwa Spika, malengo tuliyokusudia ya uchumi jumla na Mpango katika kipindi cha mwaka 2012/13 yatafikiwa kwa kuzingatia misingi ifuatayo:-

(i) Kuendelea kuimarika kwa amani, utulivu na utengamano;

(ii) Viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya jamii vitaendelea kutengamaa na kuimarika;

(iii) Mapato ya ndani yataongezeka ili kuweza kugharamia utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango;

(iv) Maeneo ya vipaumbele kama yalivyoainishwa katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano yatazingatiwa;

(v) Rasilimali zitaelekezwa kwenye maeneo ya miradi ya kimkakati na miradi muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi kwa haraka zaidi kama yalivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2012/13;

(vi) Kuendelea kutekeleza MKUKUTA II;

(vii) Kuendelea kuimarisha usimamizi wa fedha za umma;

(viii) Kuendelea kuimarisha sera za fedha ili ziendane na sera za bajeti zitakazosaidia kupunguza mfumko wa bei na tofauti ya riba za amana na za mikopo;

(ix) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuvutia ushirikishwaji wa sekta binafsi katika uchumi, hususan katika ugharamiaji wa miradi ya miundombinu; na

(x) Kuendelea kuimarisha mahusiano na Washirika wa Maendeleo na nchi marafiki.

Mheshimiwa Spika, Miradi ambayo Serikali inakusudia kutekeleza katika mwaka 2012/13 imegawanyika katika sehemu kuu mbili: Kwanza ni Miradi ya kitaifa ya Kimkakati ambayo utekelezaji wake utaleta matokeo ya haraka na kuweka msingi thabiti wa kufikia Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Sehemu ya pili ni Miradi mingineyo katika maeneo muhimu ya kiuchumi ambayo utekelezwaji wake unatarajiwa kuwezesha ukuaji wa haraka wa uchumi ambao ni shirikishi na kupunguza kiwango cha umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika kuainisha Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati, mambo muhimu yaliyozingatiwa ni pamoja na Miradi yenye kuleta matokeo ya haraka, hususan katika kuchochea maendeleo ya maeneo mengine *(multiplier effect);* uwezo wa Mradi husika kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi na hivyo kuongeza ajira; kukabiliana na matatizo ya kiuchumi yaliyopo sasa kama vile mfumko wa bei; na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Miradi mikubwa ya kimkakati itakayotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa Kituo cha Biashara na Uwekezaji Kurasini *(Kurasini Logistic/Trade Hub);* uimarishaji wa Reli ya Kati katika maeneo ya Tabora – Kigoma, Isaka – Mwanza; ukarabati wa reli (kilomita 197) katika kiwango cha *80lb/yards;* ununuzi wa vifaa kwa ajili ya ukarabati wa reli (kilomita 197 - *80lbs/yd;* ukarabati na uboreshaji wa njia ya reli katika eneo la Kidete – Gulwe; ujenzi wa Daraja la Bahi – Kintinku; na ukarabati wa injini na mabehewa ya treni. Aidha, fedha zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu wa njia ya reli katika maeneo ya kimkakati, Reli ya Mtwara – Mbamba Bay/Mchuchuma na Liganga; reli kutoka Dar es Salaam – Isaka – Kigali – Keza/Geita – Msongati na Reli ya Tanga (Mwambani) – Arusha – Musoma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nishati ya umeme, fedha zimetengwa kwa ajili ya Miradi ya Ujenzi wa Bomba la Gesi (Mtwara – Dar es Salaam) na mitambo ya kufua umeme Kinyerezi (MW 150 & MW 240). Aidha, kwa upande wa usambazaji; fedha zimetengwa kwa ajili ya Miradi ya ujenzi na uimarishaji wa njia za umeme wa msongo *220kV North – West Grid*; *400 Kv* Iringa

– Shinyanga; na *kV 132* Makambako – Songea. Vile vile, Miradi ya upelekaji umeme vijijini imetengewa fedha kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa nishati hiyo vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Barabara, Miradi iliyopewa kipaumbele ni pamoja na barabara zenye kufungua fursa kiuchumi; zinazounganisha Tanzania na nchi jirani; zinazosaidia kupunguza msongamano mijini pamoja na ujenzi wa madaraja na vivuko.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Kilimo na Viwanda, Miradi itakayotekelezwa inajumuisha ile ya kilimo cha miwa na mpunga katika mabonde makuu ya Wami, Ruvu, Kagera, Kilombero na Malagarasi; Miradi katika Ukanda wa Kilimo Kusini mwa Tanzania *(SAGCOT); ASDP* na Miradi ya Kilimo cha Umwagiliaji. Katika eneo la viwanda Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na ile ya Chuma na Makaa ya Mawe Mchuchuma na Liganga, kukamilisha Kiwanda cha Viuadudu Kibaha; Mradi wa Magadi Soda Bonde la Engaruka; na uwekezaji katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi *(EPZs & SEZs).* Aidha, Serikali italipa fidia katika maeneo maalum *(EPZ)* ya Bagamoyo na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Huduma za Kifedha, Serikali itaongeza mtaji katika Benki ya Wanawake ili kuweza kuhimili ushindani katika soko na kuwa benki ya kibiashara. Aidha, Serikali itawezesha uanzishwaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili kutoa mikopo na huduma za kibenki kwa wakulima na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ambayo Serikali itatekeleza Miradi ya Maendeleo ya Kimkakati yameelezewa kwa kina katika Sura ya Tatu ya Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2012/13.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Miradi ya Kimkakati, Miradi mingine katika maeneo muhimu ya kiuchumi itaendelezwa ili kuwezesha ukuaji wa haraka wa uchumi ambao ni shirikishi. Miradi hii itagharamiwa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo ikiwemo sekta binafsi na washirika wa maendeleo. Miradi hii ilichaguliwa kwa kuzingatia Miradi inayoendelea, Miradi yenye masharti ya kimkataba na Miradi ambayo ina fedha za wahisani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/13, Miradi itakayotekelezwa katika eneo la elimu na mafunzo ya ufundi itajumuisha uendelezaji wa ujenzi wa vyumba vya mihadhara, maktaba, mabweni ya wanafunzi katika Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Sokoine, Dodoma, Mzumbe, Ardhi, Ushirika Moshi, Ualimu Dar es Salaam na Mkwawa; uendelezaji wa vyuo vya ufundi – VETA; ujenzi wa chuo Kikuu cha Muhimbili sehemu ya Mloganzira; kusaidia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES I); ukarabati wa miundombinu katika vyuo vitano vya ualimu; na ujenzi na ukarabati wa Maktaba ya Mkoa, Dodoma. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine, itaweka nguvu kuandaa wataalam katika fani maalum (urani, gesi na mafuta).

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Afya, Programu na Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na Mpango wa Usimamizi wa Sekta ya Afya; kuwezesha programu ya kupunguza vifo vya akina mama wajawazito; kujenga na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya ikiwa ni pamoja na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali ya Magonjwa ya Saratani Ocean Road, Kituo cha Tiba ya Magonjwa ya Moyo kilichopo Hospitali ya Muhimbili na kujenga na kukarabati majengo ya Hospitali za Mikoa ya Mtwara, Mara na Lindi.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi, Programu na Miradi itakayopewa kipaumbele kwa mwaka 2012/13 ni pamoja na kuendelea kutekeleza Programu ya *ASDP* katika Sekta ya Mifugo; kuwezesha mfumo wa utambuaji na ufuatiliaji wa mifugo; na kutekeleza Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Viumbe wa Bahari katika Ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la misitu na wanyamapori, Miradi itakayotekelezwa ni kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za kuongeza thamani ya mazao ya nyuki, wanyamapori na misitu; na kujenga uwezo wa kitaasisi kwa ajili ya usimamizi wa utoaji wa hewa-ukaa.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la nishati na madini, Miradi itakayotekelezwa ni ujenzi wa Ofisi za Madini za Mikoa ya Mtwara, Dodoma, Geita na Arusha; ujenzi wa Ofisi ya Mamlaka ya

Ukaguzi wa Madini na Wakala wa Usambazaji wa Umeme Vijijini; na kuimarisha taasisi zinazoshughulika na tafiti za utafutaji na usimamizi wa madini.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la ardhi, nyumba na makazi, Miradi itakayotekelezwa ni kuanza ujenzi wa mji mpya wa kisasa Kigamboni (*Satellite City*). Aidha, Serikali inatarajia kuanzisha benki-ardhi kwa ajili ya kupata maeneo ya kilimo cha biashara na chakula.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la usafiri wa anga na majini, Miradi itakayotekelezwa ni ukarabati wa Viwanja vya Ndege vya Julius Nyerere, Mwanza, Kigoma, Tabora, Songwe, Mpanda, Arusha na Bukoba; uendelezaji wa Gati Nambari Nane katika Ziwa Tanganyika; na matengenezo ya ndege za Serikali. Aidha, katika eneo la hali ya hewa, shughuli zitakazotekelezwa ni ununuzi wa vifaa na rada kwa ajili ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania; na kuwezesha vituo vya taarifa ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi kuwa na vifaa vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la maendeleo ya teknolojia na ubunifu, Miradi itakayotekelezwa ni kuendeleza ubunifu katika kuzalisha zana za kilimo zinazoendana na teknolojia ya kisasa kwa kuimarisha Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini *(CAMARTEC)*; na kuimarisha taasisi za tathmini na ufuatiliaji wa viwango vya bidhaa vinavyohitajika katika soko hususan chakula kwa kuendeleza Taasisi ya *TIRDO.*

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Utawala Bora, shughuli zitakazotekelezwa ni kuimarisha miundombinu na vitendea kazi kwa ajili ya Sekratarieti ya Maadili ya Viongozi na TAKUKURU; kujenga uwezo wa wataalam katika Sekta ya Sheria na kuongeza vitendea kazi; ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya kuimarisha usalama wa raia na mali zao na wawekezaji; na ujenzi wa miundombinu muhimu katika Sekta ya Sheria na Utoaji Haki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/13, Serikali itaendelea na zoezi la kuandikisha raia ili waweze kupatiwa Vitambulisho vya Taifa. Utambulisho wa Kitaifa unalenga kuwa na mfumo mzuri wa kuwezesha wananchi na mali zao kutambulika rasmi na kuchangia katika shughuli za kiuchumi na maendeleo. Kukamilika kwa mfumo huu kutaongeza tija na ufanisi katika kuwezesha wananchi kupata mikopo, ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kuimarisha ulinzi na usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la kazi na ajira, shughuli zitakazotekelezwa ni kuwezesha Mifuko inayotoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana, wanawake na makundi maalum ili kutoa fursa za kupata mitaji ambayo itawawezesha kujiajiri wenyewe. Aidha, Serikali itaimarisha mifumo ya ukaguzi katika sehemu za kazi, usuluhishi na uamuzi wa migogoro ya kikazi, usimamizi na udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na ukuzaji wa ajira.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012 ni mwaka wa Sensa ya Watu na Makazi ikiwa ni miaka kumi baada ya sensa ya mwisho kufanyika nchini mwaka 2002. Tarehe 26 Agosti, 2012 ni Siku ya Sensa nchini. Kaulimbiu ya mwaka huu ni SENSA KWA MAENDELEO: JIANDAE KUHESABIWA. Maandalizi ya zoezi hili yanaratibiwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Ni matumaini yangu kuwa, Waheshimiwa Wabunge watakuwa mabalozi wazuri katika kuhamasisha na kuwahimiza wananchi wajiandae na washiriki kikamilifu katika kuhesabiwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011, Serikali ilianza mchakato wa uundwaji wa Katiba Mpya. Katika kutekeleza hilo, Serikali imeunda Tume ya Kukusanya Maoni Kuhusu Katiba Mpya. Tume hiyo inaundwa na Wajumbe 30 kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar na inaongozwa na Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba. Tume ilianza kazi rasmi Mei, 2012 na inatarajiwa kukamilisha kazi hii baada ya miezi 18.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango wa mwaka 2012/13, shilingi trilioni 4.527 zimetengwa kwa ajili ya kugharamia Mpango. Kati ya fedha hizo, shilingi 2.213 trilioni ni fedha za ndani na shilingi trilioni 2.314 ni fedha za nje. Katika fedha za ndani, shilingi trilioni 1.135 zimetegwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati na shilingi trilioni 1.078 zimetengwa kwa ajili ya Miradi mingine kwenye maeneo muhimu kwa ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, katika uandaaji wa Mpango, tumezingatia changamoto ambazo zinaweza kujitokeza kama vikwazo wakati wa utekelezaji wa Mpango. Vikwazo ambavyo vinaweza kupunguza kasi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka ni pamoja na upatikanaji na ucheleweshaji wa fedha za misaada na mikopo; upatikanaji na ukamilishaji wa mikataba ya wawekezaji na wabia; na mabadiliko ya tabia-nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na vikwazo mbalimbali vya utekekelezaji wa Mpango, itailazimu Serikali ichukue hatua zifuatazo: :upunguza utegemezi wa mikopo na misaada kwa kuboresha mifumo ya ukusanyaji na usimamiaji wa mapato hususan yasiyo ya kodi, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kurasimisha sekta isiyo rasmi; kuharakisha zoezi la tathmini ya nchi kuweza kukopa katika masoko ya fedha na mitaji kimataifa; na kuimarisha mifumo ya tahadhari na kujikinga na majanga *(disaster preparedness and surveillance).*

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji na tathmini utafuata utaratibu wa kawaida wa utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Miradi. Ufuatiliaji na tathmini wa Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati utafanywa na Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango na taasisi husika. Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) itafanya tathmini na ufuatiliaji wa Miradi katika ngazi za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na taarifa zake kuwasilishwa Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza Hali ya Uchumi wa Taifa, Matarajio, Misingi na Malengo ya Mpango na bajeti kwa kipindi cha mwaka 2011/12 ni wazi kwamba, hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kuimarisha uchumi kwa kiasi kikubwa zimeweza kuzaa matunda yaliyotarajiwa. Katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2012/13, juhudi zitaendelea kuelekezwa katika kuhakikisha ukuaji wa uchumi unaimarika zaidi, kupunguza mfumko wa bei kwa kuongeza uzalishaji wa chakula na kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa kutosha na wa uhakika na kuzalisha ajira hasa kwa vijana, wanawake na makundi maalum.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo imeungwa mkono na tunaishukuru Tume ya Mipango kwa kuwasilisha Hotuba yake kuhusu Hali ya Uchumi wa Nchi katika mwaka tunaoenda nao.

Waheshimiwa Wabunge, kama kawaida yetu, sasa tumesoma Hotuba ya Hali ya Uchumi lakini saa kumi ndiyo tutasoma Bajeti inayohusika. Kwa hiyo, nawaombeni sana muwahi; ni saa kumi kamili siyo saa kumi na moja. Jitahidini kila mtu awe amekaa kwa sababu tutakuwa na wageni wengi sana ambao wanakuja kusikiliza Hotuba hiyo.

Baada ya kusema hivyo, nina tangazo moja kwamba siku ya tarehe 16, yaani kesho kutwa, Jumamosi, kutakuwa na Uzinduzi wa Awamu ya Nne ya Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma *(The Launching of Public Financial Management Reform Programme – Phase IV)* katika Ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa nne asubuhi. Programu hii ni ile ambayo inapitia kwa *CAG* lakini inasaidia Kamati ya *Public Accounts Commitee, Local Government Accounts Commitee, Parastatal Accounts Commitee* na Kamati ya Uchumi na Fedha. Kwa hiyo, wanaingia awamu ya nne, tulikuwa na awamu ya kwanza, ya pili na sasa hii ni ya nne na itaendelea kusaidia kwenye *capacity building* na kuwaonesha watu mifumo mbalimbali ambayo inaweza kutumika katika kuisimamia Serikali.

Baada ya kusema hayo, naomba kusitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi jioni.

*(Saa 5.28 asubuhi Bunge lilifungwa mpaka Saa 10. 00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liweze kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013. Pamoja na Hotuba hii, nimewasilisha Vitabu Vinne vya Bajeti vinavyoelezea takwimu mbalimbali za Bajeti. Kitabu cha Kwanza kinaelezea makisio ya mapato. Kitabu cha Pili kinaelezea makisio ya matumizi ya kawaida kwa Wizara, Idara zinazojitegemea; Taasisi na Wakala wa Serikali. Cha Tatu kinahusu makisio ya matumizi ya kawaida kwa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Cha Nne kinaelezea makadirio ya matumizi ya maendeleo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali; Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, upo Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2012 ambao ni sehemu ya Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati, Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani kubwa aliyonayo kwangu kwa kuniteua kuwa Waziri wa Fedha. Naahidi kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa kwa umakini na uaminifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza wafuatao kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mawaziri kama ifuatavyo: Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mbunge; Mheshimiwa Mhandisi Christopher Kajoro Chiza, Mbunge; Mheshimiwa Dokta Harrison George Mwakyembe Mbunge; Mheshimiwa Dokta Fenella Ephraim Mukangara, Mbunge; Mheshimiwa Balozi Khamis Sued Kagasheki, Mbunge; na Mheshimiwa Dokta Abdallah Omari Kigoda Mbunge. Aidha, napenda kuwapongeza wafuatao kwa kuteuliwa kuwa Naibu Mawaziri katika Wizara mbalimbali; Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mbunge; Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Mbunge; Mheshimiwa Dokta Seif Suleiman Rashid, Mbunge; Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge; Mheshimiwa January Yusuf Makamba, Mbunge; Mheshimiwa Dokta Charles John Tizeba, Mbunge; Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Mbunge; Mheshimiwa Angela Jasmine Kairuki, Mbunge; Mheshimiwa Stephen Julius Maselle, Mbunge; na Mheshimiwa Mhandisi Dokta Binilith Satano Mahenge, Mbunge. Kadhalika, nampongeza Mheshimiwa James Mbatia, Mbunge, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Mheshimiwa Alhaji Adam Kimbisa, Mbunge; Mheshimiwa Shy Rose Banji, Mbunge; Mheshimiwa Abdulah Alli Hassan Mwinyi, Mbunge; Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, Mbunge; Mheshimiwa Dkt. Twaha Issa Taslima, Mbunge; Mheshimiwa Nderkindo Perpetua Kessy, Mbunge; Mheshimiwa Bernard Musomi Murunyana, Mbunge; Mheshimiwa Anjela Charles Kizigha, Mbunge; na Mheshimiwa Maryam Ussi Yahaya, Mbunge, ambao wamechaguliwa kutuwakilisha kwenye Bunge la Afrika Mashariki. Ni matumaini yangu watatuwakilisha vyema kwa maslahi na manufaa ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Bajeti hii yamehusisha wadau na Taasisi mbalimbali. Napenda kuwashukuru walioshiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha matayarisho yake. Kwa namna ya pekee, ninaishukuru Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Mtemi Andrew John Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi, pamoja na Kamati nyingine za Kisekta, kwa ushauri mzuri walioutoa wakati wakichambua mapendekezo ya Bajeti hii. Aidha, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushauri na mapendekezo yao ambayo yamezingatiwa katika Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, Mbunge, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, kwa ushirikiano alionipatia wakati wa maandalizi ya Bajeti. Aidha, nawashukuru Naibu Mawaziri wa Fedha, Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mbunge na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Mbunge. Namshukuru Katibu Mkuu, Ndugu Ramadhani M. Khijjah; Naibu Katibu Wakuu; Ndugu Laston T. Msongole, Dokta Servacius B. Likwelile na Ndugu Elizabeth Nyambibo, kwa mchango wao mkubwa katika matayarisho ya Bajeti. Vilevile,

nawashukuru Prof. Benno Ndulu, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania; Dokta Phillip Mpango, Katibu Mtendaji Ofisi ya Rais (Tume ya Mipango); Ndugu Harry Kitilya, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania; na Dokta Albina Chuwa, Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Takwimu ya Taifa. Nawashukuru wote kwa mchango wao katika maandalizi ya bajeti hii. Naishukuru pia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kutayarisha kwa wakati Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2012 na nyaraka mbalimbali za Sheria ambazo ni sehemu ya Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wakuu wa Idara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha, kwa ushirikiano wao. Aidha, namshukuru Mpigachapa Mkuu wa Serikali, kwa kuchapisha Hotuba hii kwa wakati. Nawashukuru pia Wataalamu na wale wote waliotoa mapendekezo kuhusu Sera, Mikakati na masuala mbalimbali ya kodi ambayo yamezingatiwa katika kuandaa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa Mwenyeji wa Mikutano ya Bodi ya Magavana wa Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa Mwaka 2012 iliyofanyika kuanzia tarehe 28 Mei hadi tarehe 2 Juni 2012 na kufunguliwa rasmi na Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mikutano hii ilifanyika kwa ufanisi mkubwa katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha na kuhudhuriwa na washiriki 2,350 kutoka ndani na nje ya Tanzania. Hii imekuwa ni nafasi ya kipekee kwa Tanzania kutangaza fursa mbalimbali za kiuchumi zilizopo nchini. Aidha, washiriki wa ndani kutoka sekta binafsi walipata nafasi ya kufahamu fursa za mikopo zilizopo katika Benki ya Maendeleo ya Afrika. Napenda kutoa wito kwa sekta binafsi kutumia fursa hizo kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Mwaka 2012/13 imelenga kukabiliana na changamoto zinazokabili uchumi ikiwa ni pamoja na kuongeza fursa za kukuza uchumi, kushughulikia uhaba wa chakula nchini, kupambana na mfumko wa bei, kuendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kusimamia matumizi, kushughulikia suala la ukosefu wa ajira hasa kwa vijana, kuwekeza katika miundombinu ya nishati ya umeme hususan ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam, barabara, bandari na reli ya kati ili kupunguza gharama za kufanya biashara na kuongeza tija katika uzalishaji na kulipa madeni ya ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2011/12. Mfumo wa Bajeti ya Mwaka 2011/12 uliendeleza juhudi za Serikali za kufikia Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Aidha, Bajeti ilizingatia utekelezaji wa vipaumbele vya Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16); Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA II); Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015; Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA); Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010; Mkakati wa Taifa wa Madeni; pamoja na kuimarisha usimamizi wa kodi na matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, misingi na shabaha za bajeti ya mwaka 2011/12, pamoja na mambo mengine, ililenga kukamilisha malengo ya Serikali ya kukabiliana na changamoto za kupunguza makali ya maisha kwa wananchi; kuendelea kuboresha mfumo wa makusanyo ya mapato ya ndani; kuboresha mazingira ya uwekezaji wa ndani na nje; kuendeleza sekta binafsi ili kupanua wigo wa kodi; kukamilisha maandalizi ya Mradi wa Vitambulisho vya Taifa; na kutenga rasilimali na kutekeleza Miradi katika maeneo ya kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yaliyozingatiwa katika misingi na shabaha ya bajeti hiyo yalikuwa ni kutekeleza mipango na mikakati maalum ya kuharakisha ukuaji wa uchumi; kutafuta mikopo ya masharti nafuu na ya kibiashara; kuharakisha utekelezaji wa Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na ya Binafsi ili kupanua fursa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo; Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012; kuhakikisha kwamba maduhuli ya Serikali yanakusanywa ipasavyo na kuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali; pamoja na kulinda na kudumisha mafanikio yaliyopatikana katika Sekta za Huduma za Jamii, hususan elimu na afya ambazo zimekuwa na upanuzi mkubwa wa huduma.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2011/12, Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali kukabiliana na changamoto zinazowakabili wananchi kwa lengo la kupunguza makali ya maisha kunakotokana na kupanda kwa bei za bidhaa na huduma. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kurekebisha namna ya kukokotoa gharama za mafuta na kutangaza bei elekezi kila mwezi na kuanzisha utaratibu wa uagizaji mafuta kwa pamoja *(bulk procurement)*. Hatua hizi zimesaidia kupunguza kasi ya upandaji wa bei ya mafuta hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetumia shilingi bilioni 296 kutekeleza mpango wa dharura wa kukabiliana na tatizo la upungufu wa nishati ya umeme kwa kutumia mitambo ya kukodi. Utekelezaji wa jitihada hizi umeongeza megawati 324 kwenye Gridi ya Taifa. Kadhalika, Serikali ilitumia Dola za Marekani milioni 183 kugharamia ujenzi wa mitambo ya kufua umeme wa megawati 100 kwa Mkoa wa Dar es Salaam, Mradi ambao umekamilika na upo kwenye hatua za majaribio na Megawati 60 kwa Mkoa wa Mwanza ambao bado ujenzi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetumia shilingi bilioni 27 kugharamia ununuzi na usambazaji wa tani 120,000 za mahindi katika masoko kwa lengo la kukabiliana na uhaba wa chakula kwa baadhi ya maeneo. Aidha, Serikali ilitoa vibali vya kuagiza sukari bila kutoza ushuru wa forodha kiasi cha tani 200,000 ili kukabiliana na uhaba na kupanda kwa bei ya sukari. Kadhalika, Serikali ilipandisha kiwango cha riba inayotozwa na Benki Kuu kwa Taasisi za Fedha kutoka asilimia 7.58 hadi asilimia 12.58. Vilevile, Serikali ilipandisha kiwango cha amana ambacho benki za biashara zinapaswa kuhifadhi Benki Kuu kutoka asilimia 20 hadi asilimia 30. Hatua hizi zimesaidia kupunguza kasi ya kupanda kwa bei.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na tatizo la ajira, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuongeza fursa za ajira. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha mazingira ya kisera na kisheria kuwezesha sekta binafsi kukua; kupanua huduma za fedha ikiwa ni pamoja na kuongeza mitaji katika Benki ya Rasilimali, Benki ya Wanawake, Benki ya Posta na Twiga Bancorp na kufanikisha uanzishwaji wa kampuni ya kutoa mikopo ya muda mrefu ya ujenzi wa nyumba na makazi. Hatua nyingine zilizochukuliwa na kuchangia ongezeko la ajira ni pamoja na kujenga miundombinu ya barabara, umeme, kilimo, mawasiliano na kuwezesha wananchi kupitia programu mbalimbali za uwezeshaji. Aidha, kuna Taasisi mbalimbali ambazo zimechangia kutoa ajira kama vile *TASAF, SELF, VETA,* Shirika la Viwanda Vidogovidogo *(SIDO)*, Taasisi ndogondogo za Fedha, *VICOBA*, Benki za Kijamii na Mifuko ya Udhamini ya mikopo inayosimamiwa na Benki Kuu. Katika mwaka 2011/12, Serikali iliajiri Walimu wa Shule za Sekondari na Msingi 25,000, Maafisa Ugani wa Kilimo na Mifugo 4,499 na Watumishi wa Kada ya Afya 6,916.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianza utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji mwaka 2011 kufuatia kuidhinishwa kwake mwaka 2010. Kupitia Mpango huu, taratibu na kanuni za mawasilisho na malipo ya kodi na ushuru yanafanyika kwa njia ya mtandao. Utaratibu huu umeongeza ufanisi kwa kuondoa usumbufu na upotevu wa muda katika ulipaji wa kodi. Hadi sasa, zaidi ya asilimia 75 ya walipa kodi wakubwa na walipa kodi wengine 2,795 wanafanya mawasilisho yao kwa njia ya mtandao. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania ilianzisha mfumo unaounganisha usimamizi wa kodi *(Asycuda, ITAX)* na benki za biashara ili kurahisisha ulipaji wa kodi. Mfumo huu umeunganisha jumla ya benki 25. Kadhalika, Mamlaka inatumia huduma za *M-Pesa (Vodacom)* na *NMB mobile* kwa ajili ya kulipia kodi ya majengo na kodi ya mapato.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea na jitihada za kupunguza urasimu katika utoaji wa mizigo bandarini kwa kuanzisha utaratibu wa kuwasilisha nyaraka kwa njia ya mtandao kabla ya mizigo kuwasili. Utaratibu huu umelenga kupunguza tatizo la mrundikano na upotevu wa nyaraka na kupelekea kupungua kwa muda na gharama za uagizaji na usafirishaji mizigo nje ya nchi. Serikali imepunguza vizuizi vya usafirishaji mizigo ndani ya nchi kutoka 50 vilivyokuwepo kufikia 15, isipokuwa vituo vya mizani na forodha. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za kufanya biashara na usumbufu wanaopata wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/12, Serikali iliendelea kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani yanayotokana na kodi na yasiyo ya kodi kwa kuchukua hatua za kiutawala, kisera pamoja na marekebisho ya viwango vya kodi na sheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148, ili kuboresha uzalishaji katika Sekta za Kilimo, Mifugo, Viwanda, Biashara na Utalii. Marekebisho hayo ni pamoja na kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vipuri vya zana za kilimo; chakula cha kukuzia kuku; nyuzi za kutengenezea nyavu za kuvulia samaki; pamoja na kuanzisha utaratibu wa kuwarejeshea kodi wageni kwa bidhaa walizonunua nchini wakati wanaondoka.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilifuta msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye kuuza na kupangisha majengo ya nyumba za kuishi za Shirika la Nyumba la Taifa - *NHC*; kuondoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali isipokuwa kwenye vifaa vya misaada kwa vituo vya kulelea watoto yatima na shule.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ilifanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332, kwa kufuta Kodi ya Zuio kwa usafirishaji wa samaki nje ya nchi ili kuongeza utoaji wa huduma za usafirishaji wa mazao ya samaki kutokea hapa nchini badala ya kupitia nchi za jirani. Aidha, marekebisho yalifanyika katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147, kwa kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye mafuta mazito ya kuendeshea mitambo ili kupunguza gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Mafuta ya Petroli, Sura ya 220, ilifanyiwa marekebisho kwa kutoa msamaha wa ushuru unaotozwa kwenye mafuta yanayotumika katika kuendesha meli na vifaa vingine vinavyotumika katika utafiti wa mafuta na gesi ili kupunguza gharama. Aidha, marekebisho yalifanyika kwenye Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004 kufuatia kuridhia kwa Mawaziri wa Fedha wa Nchi Wanachama kufanya marekebisho mbalimbali katika kukuza Sekta za Viwanda, Usafirishaji, Mifugo, Biashara na Utalii. Vilevile, marekebisho yalilenga katika kuboresha afya ya jamii na kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na kuhamasisha na kuhakikisha mashine za kielectroniki – *EFD* zinatumika ipasavyo; kuimarisha mfumo wa kusimamia vitalu vya kodi; kuongeza vituo vya kutoa huduma kwa wateja na vya kukusanyia mapato; kuimarisha mifumo ya malipo ya kodi; na kuboresha mfumo wa uthaminishaji kwa kuimarisha ukaguzi wa hesabu za walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumze juu ya mwenendo wa ukusanyaji mapato, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali ilipanga kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 13,525.9 kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali na kutumia kiasi hicho kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Vyanzo vya mapato vilikuwa kama ifuatavyo: mapato ya ndani yalikadiriwa kufikia kiasi cha shilingi bilioni 6,775.9; mapato kutoka Serikali za Mitaa yalikadiriwa kufikia kiasi cha shilingi bilioni 350.5; misaada na mikopo ya kibajeti ilikadiriwa kufikia kiasi cha shilingi bilioni 869.4; misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo na ya kisekta ilikadiriwa kufikia kiasi cha shilingi bilioni 3,054.1; mikopo ya ndani na nje yenye masharti ya kibiashara ilikadiriwa kufikia kiasi cha shilingi bilioni 1,664.9; na mikopo ya kulipia dhamana na hatifungani zinazoiva zilikadiriwa kufikia kiasi cha shilingi bilioni 810.9.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri, hadi Aprili 2012 makusanyo yamefikia jumla shilingi bilioni 5,684.5. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 80 ya makadirio ya kukusanya shilingi bilioni 7,126.4 kwa mwaka 2011/12.

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 5,227.5 ambayo ni sawa na asilimia 84 ya makadirio ya kukusanya shilingi bilioni 6,228.8. Kulingana na mwenendo wa makusanyo ya mapato ya kodi kwa kipindi cha miezi kumi ya mwaka 2011/12, hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 6,307.8 na hivyo kuweza kufikia lengo tulilojiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapato yasiyotokana na kodi yamefikia shilingi bilioni 451.6 ikiwa ni asilimia 83 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 547.1 kwa mwaka. Kutokana na mwenendo huo, Serikali inatarajia hadi Juni 2012 kufikia malengo yao.

Mheshimiwa Spika, mapato ya Serikali za Mitaa yalifikia kiasi cha shilingi bilioni 143, sawa na asilimia 40.8 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 350.5 kwa mwaka. Hadi Juni 2012, Serikali inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 200 kutokana na chanzo hiki ikiwa ni asilimia 57 ya lengo la mwaka. Kutokufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato haya kumechangiwa na kuchelewa kuanza kutekeleza utozaji wa ada za leseni.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie juu ya misaada na mikopo ya masharti mafuu kutoka nje, katika mwaka 2011/2012, Serikali ilikadiria kupata kiasi cha shilingi bilioni 869.4 kama misaada na mikopo ya kibajeti ambayo hadi sasa Serikali imepokea shilingi bilioni 916.3, ikiwa zaidi ya shilingi bilioni 46.9. Ongezeko hili limetokana na baadhi ya wafadhili kutoa fedha zaidi ya kiwango walichoahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo ikijumuisha mifuko ya kisekta, hadi kufikia Aprili 2012 ilifikia shilingi bilioni 1,450.4 sawa na asilimia 47 ya makadirio ya bajeti ya mwaka ya shilingi bilioni 3,054.1. Upungufu huu umesababishwa na kasi ndogo ya utekelezaji wa baadhi ya miradi na kuchelewa kupokea taarifa ya fedha hizi kutoka kwa washirika wa maendeleo na Wizara na Taasisi zinazotekeleza miradi husika.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya ndani, katika kipindi cha Julai 2011 hadi Aprili 2012, Serikali imekopa kiasi cha shilingi bilioni 526 kwa ajili ya kulipia dhamana za Serikali zilizoiva ikiwa ni asilimia 64 ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 819.1. Aidha, Serikali ilipanga kukopa shilingi bilioni 393.4 sawa na asilimia moja ya Pato la Taifa kwa ajili ya kugharamia matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2012, Serikali ilikuwa imekopa shilingi bilioni 232.6 sawa na asilimia 59 ya makadirio ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara, mwaka 2011/2012, Serikali ilikadiria kukopa kiasi cha Dola za Marekani milioni 822, sawa na shilingi bilioni 1,271.6 kama mikopo ya kibiashara. Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Aprili 2012, Serikali ilisaini Mkataba wa mkopo wa kiasi cha Dola za Marekani milioni 310 na Benki ya *Standard* ya Afrika Kusini. Hadi kufikia Aprili 2012, jumla ya Dola za Marekani milioni 229 ambazo zilitumika kulipia madeni ya barabara ya mwaka 2010/2011ndizo zilizotumika.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali ilisaini mkataba wa mkopo wa Euro milioni 61 na Benki ya *HSBC*. Mkopo huu umeelekezwa kugharamia ujenzi wa mtambo wa kufua umeme wa megawati 60 Nyakato Mwanza. Serikali pia imesaini mkataba wa mkopo wa Dola za Marekani milioni 350 kutoka Benki ya *Credit Suisse* ya Uingereza ambapo Dola za Marekani milioni 200 zimepokelewa mwanzoni mwa mwezi huu Juni 2012. Kiasi kilichobaki cha Dola za Marekani milioni 150 kitapatikana na kutumika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepata Mshauri Mwelekezi ambaye ataishauri Serikali katika zoezi la kujiandaa kufanyiwa tathmini ya uwezo wa kukopa na kulipa madeni *(Sovereign Credit Rating).* Maandalizi haya yataiwezesha nchi kufanyiwa tathmini yanatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2013. Kukamilika kwa zoezi hilo kutawapatia wakopeshaji imani na hivyo kuiwezesha Serikali kupata mikopo yenye masharti nafuu ya kibiashara kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sera za Matumizi, katika mwaka 2011/2012, Serikali iliendelea kutekeleza sera za matumizi kulingana na upatikanaji wa mapato ya ndani, misaada pamoja na mikopo ya ndani na ile ya nje. Aidha, Serikali iliendelea kuboresha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma, ikijumuisha udhibiti wa ulipaji wa mishahara, matumizi katika miradi ya maendeleo, ruzuku ya pembejeo, ununuzi wa umma na kuendelea kudhibiti malimbikizo ya madeni. Serikali imeandaa mkakati wa kulipa na kudhibiti madeni yatokanayo na malimbikizo ya madai ya watumishi; wakandarasi; wazabuni; na madeni mengineyo. Madeni hayo yatalipwa baada ya kuhakikiwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma. Katika jitihada za kuimarisha usimamizi wa fedha za umma, Serikali imeendelea kutekeleza programu ya maboresho ya usimamizi wa fedha za umma katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Katika

utekelezaji wa programu hiyo, Serikali imeweka mtandao wa *IFMS* katika Halmashauri 133. Aidha, Serikali imetoa mafunzo ya ulipaji kwa mfumo wa malipo ya kibenki - *TISS* kwa watumishi wa kada ya Uhasibu katika Mikoa 20, Hazina ndogo zote, Ofisi ya Bunge, TAMISEMI na Ofisi ya Mrajisi wa Vyama vya Ushirika. Vilevile, Serikali imetoa mafunzo kwa Wahasibu wa Wizara, Idara, Mikoa na Balozi zetu 32 katika kuandaa Hesabu za Serikali kwa viwango vya Kimataifa (*IPSAS – Accruals basis*).

Mheshimiwa Spika, kutokana na maboresho hayo, usimamizi wa fedha katika Wizara, Idara, Taasisi, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa unaendelea kuimarika. Hali hii inajidhihirisha katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2010/2011 ambapo Hati Safi za ukaguzi kwa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa zimeongezeka kutoka asilimia 71 hadi asilimia 85. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Hati zenye Shaka zimepungua kutoka asilimia 26 mwaka wa fedha 2009/2010 hadi asilimia 15 kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na hapakuwepo na Hati zisizoridhisha ikilinganishwa na mwaka 2009/2010 ambapo Hati hizo zilitolewa kwa Taasisi mbili.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Balozi zetu, Hati Safi zimeongezeka kutoka asilimia 71 mwaka 2009/2010 na kufikia asilimia 85 mwaka 2010/2011 na hapakuwepo na Hati zisizoridhisha katika mwaka 2010/2011. Aidha, kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, Hati safi zimeongezeka kutoka asilimia 49 mwaka wa fedha 2009/2010 hadi asilimia 54 mwaka 2010/2011 na hivi Hati zenye Shaka zimepungua kutoka asilimia 64 mwaka 2009/2010 na kufikia asilimia 56 mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali imefungua akaunti sita kwa kila Halmashauri kwa ajili ya uendeshaji wa majukumu yao. Akaunti hizo ni za Mapato; Amana; Matumizi ya kawaida; Mishahara; Maendeleo; na Mfuko wa Barabara. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uendeshaji, urasimu wa matumizi, ugumu wa kutoa taarifa za matumizi, ulimbikizaji wa fedha kwenye akaunti bila kutumika kwa muda mrefu na kudhibiti fedha zisitumike katika shughuli ambazo hazikuidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa matumizi. Kwa upande wa matumizi, Serikali ilikadiria kutumia kiasi cha shilingi bilioni 13,525.9 katika mwaka wa fedha wa 2011/2012. Mgawanyo wa matumizi ya Serikali katika kipindi hiki ulikuwa kama ifuatavyo; kiasi cha shilingi bilioni 8,600.3 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 4,925.6 zilikadiriwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida. Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Aprili 2012 matumizi ya kawaida yamefikia shilingi bilioni 7,349.8 sawa na asilimia 85.5 ya makadirio ya mwaka kama ilivyo katika ridhaa ya matumizi. Kati ya kiasi hicho, malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma yalikuwa shilingi bilioni 2,760.5 sawa na asilimia 84.4 ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 3,270.3. Malipo ya riba kwa mikopo ya ndani na nje yalikuwa shilingi bilioni 316.1 sawa na asilimia 102.4 ya makadirio ya shilingi bilioni 308.7 kwa mwaka. Malipo ya mikopo ya nje yalikuwa shilingi bilioni 57.3 sawa na asilimia 85.7 ya makadirio kwa mwaka. Serikali ilitumia shilingi bilioni 526 kwa ajili ya kulipia dhamana za Serikali za muda mfupi na Hatifungani za Serikali zilizoiva. Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika kulipa madeni kwa wakati ili kuepuka malimbikizo ya riba.

Mheshimiwa Spika, matumizi mengineyo katika Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 2,384.9 ikiwa ni asilimia 72.8 ya makadirio ya shilingi bilioni 3,275.1 kwa mwaka. Kati ya matumizi mengineyo, kiasi cha shilingi bilioni 284.1 zilitumika kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ikiwa ni asilimia 89 ya bajeti ya mwaka ya shilingi bilioni 317.4, na hivyo kunufaisha jumla ya wanafunzi 93,176. Kadhalika, Serikali ililipa kiasi cha shilingi bilioni 44.0 za madai ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari yaliyohakikiwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matumizi ya maendeleo. Kwa upande wa matumizi ya maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 2,657.2 ziligharamia miradi ya maendeleo ikilinganishwa na makadirio ya mwaka ya kutumia shilingi bilioni 4,924.6. Fedha za ndani zilikuwa shilingi bilioni 1,201.6

ikilinganishwa na makadirio ya mwaka ya shilingi bilioni 1,871.5 sawa na asilimia 64.2. Upungufu huu umetokana na kuchelewa kupatikana kwa wakati kwa mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara. Jumla ya shilingi bilioni 663.8 zaligharamia miradi ya miundombinu, kati ya hizo shilingi bilioni 296 zilitumika kwenye miradi ya umeme na shilingi bilioni 367.8 kwenye miradi ya barabara. Matumizi ya maendeleo yaliyogharamiwa kwa fedha za nje yalikuwa shilingi bilioni 1,450.4 ikilinganishwa na makadirio ya shilingi bilioni 3,054.1 sawa na asilimia 47.

Mheshimiwa Spika, Vitambulisho vya Taifa na Anwani za Makazi. Serikali imeendelea na azma yake ya kutekeleza mradi wa Vitambulisho vya Taifa ambavyo vitasaidia, pamoja na mambo mengine, kurahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na huduma za kifedha. Mradi huu unaenda sambamba na uanzishwaji wa anwani za makazi. Vitambulisho hivyo vitaanza kutolewa katika robo ya kwanza ya mwaka 2012/2013 kwa Zanzibar na Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Sensa ya Watu na Makazi na Utafiti Kuhusu Hali ya Umaskini. Kwa kutambua umuhimu wa Sensa ya Watu na Makazi, Serikali imeendelea kugharamia maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi, ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95. Hadi sasa Serikali imetumia shilingi bilioni 23.6 kugharamia maandalizi ya zoezi la Sensa. Sensa hiyo imepangwa kufanyika tarehe 26 Agosti 2012. Aidha, Serikali iliendelea kugharamia utafiti wa mapato na matumizi katika kaya. Utafiti huu ulianza mwezi Oktoba 2011 na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba 2012 na matokeo yanatarajiwa kutoka mwezi Julai 2013. Utafiti huu utatoa picha halisi ya hali ya umaskini, hususan wa kipato tangu mwaka 2007 hadi mwaka 2012. Hii itasaidia kutambua mwenendo wa umaskini wa kipato na sababu zilizopelekea mwenendo huo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II). Katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Serikali iliendelea kutekeleza MKUKUTA awamu ya pili unaojielekeza katika maeneo ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato, kuboresha maisha na ustawi wa jamii na utawala bora na uwajibikaji sambamba na Melengo ya Maendeleo ya Milenia. Ili kufikia matokeo tarajiwa katika kila eneo, sekta kadhaa huchangia katika utekelezaji kupitia sera, mikakati na mipango ya kisekta. Kwa mantiki hiyo, utekelezaji wa MKUKUTA II unahitaji ushirikiano wa sekta mbalimbali za uchumi katika hatua ya upangaji na utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, MKUKUTA ni mkakati unaoziweka pamoja juhudi za Serikali na wadau mbalimbali katika kupambana na umaskini. Aidha, umaskini ni suala pana linalojumuisha umaskini wa kipato na usio wa kipato. Ni kweli kuwa umaskini wa kipato umekuwa ukipungua kwa kasi ndogo. Hata hivyo, Serikali inachukua hatua mbalimbali za kupunguza umaskini kwa kujenga mazingira bora ili wananchi washiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi, ikiwa ni pamoja na kuwekeza katika elimu, afya, miundombinu na sekta ya fedha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zilizojitokeza, hususan mtikisiko wa uchumi duniani, uchumi uliendelea kukua kwa kiwango cha kuridhisha. Kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2011, kilikuwa asilimia 6.4 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2010. Aidha, pato la wastani la Mtanzania limeongezeka kutoka shilingi 770,464 kwa mwaka 2010 hadi shilingi 869,436 kwa mwaka 2011. Kwa wastani, ongezeko hili limeongeza uwezo wa wananchi kupata huduma bora ikiwa ni pamoja na nyumba bora, simu za mkononi, pikipiki na usafiri wa baiskeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza programu mbalimbali za huduma ya jamii kwa lengo la kuboresha maisha na ustawi wa jamii. Matokeo ya utekelezaji wa programu hizo zinaonesha mabadiliko chanya. Katika sekta ya elimu, viwango vya uandikishaji na kumaliza katika ngazi zote za elimu vinaridhisha. Mfano, kiwango cha uandikishwaji katika elimu ya msingi, kilikuwa asilimia 94 na katika elimu ya sekondari ni asilimia 35 kwa mwaka 2011. Huduma za afya kwa mtoto na mama zinaendelea kuimarika kutokana na utekelezaji wa mpango wa afya ya mtoto na mama. Aidha, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama imeendelea kuimarika kutokana na utekelezaji wa programu ya sekta ya maji iliyoanza mwaka 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika huduma ya utawala bora na uwajibikaji, Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kuimarisha sekta ya sheria kwa kuongeza idadi ya

mahakimu wa Mahakama za mwanzo; kuimarisha mfumo wa sheria na haki za binadamu; kuhamasisha umma kuhusu haki za binadamu na wajibu wa jamii; na kushiriki katika mpango wa nchi za Afrika kujitathmini zenyewe katika masuala ya utawala bora. Aidha, Serikali imeendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha za umma, kwa kuimarisha ofisi za ukaguzi katika Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, niruhusu sasa nizungumze juu ya Sekta ya Fedha. Serikali imefanya mageuzi mbalimbali katika sekta ya fedha ili kuhakikisha kwamba inachangia kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kukuza Pato la Taifa. Mageuzi haya yameleta mafanikio makubwa. Hadi kufika mwezi Aprili mwaka 2012 idadi ya benki imeongezeka na kufikia 49 kutoka benki 43 Aprili mwaka 2011. Kadi za simu za mkononi zinazotumika kutoa huduma za kifedha zimefikia 21,184,808 mwaka 2011 kutoka 10,663,623 mwaka 2010. Aidha, idadi ya Taasisi ndogo ndogo za kifedha zimefikia 150 mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kutoa mikopo ya kilimo kupitia dirisha la kilimo lililopo katika Benki ya Rasilimali Tanzania. Hadi kufikia Machi, 2012 jumla ya mikopo 81 yenye thamani ya shilingi bilioni 22.9 ilitolewa, kati ya mikopo hiyo, 42 ni ya *SACCOS*, 32 ni kwa ajili ya makampuni na 7 kwa Taasisi ndogondogo za fedha (*MFIs*). Mikopo iliyotolewa kwa *MFIs* yaani *Micro Finance Institutions* na *SACCOS* ilitumika kukopesha miradi mingi ya wakulima wadogo wadogo vijijini. Aidha, Serikali imetoa shilingi bilioni 30 kwa ajili ya mtaji wa Benki ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea na utekelezaji wa programu ya mageuzi na maboresho ya ushirika nchini ili kuimarisha vyama vikuu vya ushirika na kuviwezesha kutoa huduma za kifedha kwa wananchi wengi zaidi hususan waliopo vijijini. Mwaka 2011, idadi ya Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (*SACCOS*) iliongezeka na kufikia 5,346 kutoka vyama 5,314 mwaka 2010. Vilevile, idadi ya wanachama iliongezeka kwa asilimia 5.7 na kufikia wanachama 970,655 kutoka wanachama 917,889 iliyokuwepo mwaka 2010. Aidha, Hisa, Akiba na Amana za wanachama ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 236.8 mwaka 2010 hadi shilingi bilioni 399.0 mwaka 2011, hii ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 68.5. Mikopo iliyotolewa kwa wanachama iliongezeka kutoka shilingi bilioni 539.2 mwaka 2010 hadi shilingi bilioni 627.2 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 16.3.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi 2012, mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kwa asilimia 21.9 ikilinganishwa na asilimia 23.3 Machi 2011. Ongezeko hili linaenda sambamba na kuongezeka kwa rasilimali za fedha za ndani kwenye benki pamoja na kupungua kwa ukuaji wa rasilimali za fedha za kigeni kwenye benki. Sehemu kubwa ya mikopo hii ilielekezwa katika shughuli binafsi asilimia 21.9; biashara asilimia 19.9; uzalishaji bidhaa viwandani asilimia 11.9; kilimo asilimia 11.8 na usafiri na mawasiliano asilimia 7.9.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza upatikanaji wa mikopo, Serikali imepata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuanzisha Taasisi ya Kuratibu Taarifa za Wakopaji (*Credit Rerefence Bureau*) na Mfumo wa Kuhifadhi Taarifa za Wakopaji (*Credit Reference Databank*). Mshauri Mwelekezi ameanza zoezi la kuweka mitambo na kutoa mafunzo kwa watumiaji. Aidha, Serikali imeboresha mazingira ya upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu na kati kwa ajili ya nyumba, kilimo na uwekezaji ambapo kanuni za taasisi za fedha za maendeleo ziliandaliwa na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la Machi 2012.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali imeendelea kufanya maboresho katika sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa kufanya tathmini ya uwekezaji wa mifuko, uhai wa mifuko, pamoja na kuandaa mwongozo za uwekezaji wa mifuko hiyo. Aidha, Serikali imefanya marekebisho ya Sheria za Mifuko yote pamoja na Mamlaka ya Usimamiaji wa Shughuli za Mifuko (*SSRA*) ili kuboresha usimamizi wa mifuko hiyo.

Mheshimiwa Spika, ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria mpya ya Ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ya mwaka 2010 ili kutoa fursa kwa sekta binafsi kushiriki katika ujenzi wa miundombinu na kuiendesha kwa lengo la kutoa huduma bora za kijamii na kiuchumi kwa wananchi. Katika mwaka 2011/2012, Serikali imefanya maandalizi ya utekelezaji wa Sera ya Ubia ikiwa ni pamoja na kuanzisha madawati ya *PPP* kwa kila

Wizara na kuandaa miongozo itakayotumika kuchambua na kuidhinisha miradi ya ubia kwa mujibu wa sheria. Aidha, Serikali imeanza hatua za awali kubaini miradi inayoweza kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, dhana ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi inatekelezwa kwa kutumia sheria mbili yaani Sheria ya Ubia ya mwaka 2010 na Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 iliyorekebishwa mwaka 2011. Sababu za kurekebisha Sheria ya Ununuzi wa Umma pamoja na mambo mengine ni kuingiza vifungu vinavyowezesha Taasisi za Serikali kupata wabia makini wa uwekezaji katika miradi ya umma kwa njia zilizo wazi. Aidha, katika mwaka 2012/2013, Serikali itakamilisha Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma ambazo zinazingatia mazingira ya kipekee ya Sheria ya Ubia ambayo inawezesha kupata wabia walio tayari kuwekeza katika miradi husika. Serikali itahakikisha kanuni na taratibu zote za kuidhinisha na kusimamia miradi ya ubia zinazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali itatoa mafunzo ya uelewa wa dhana ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa watumishi wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi za Serikali na Halmashauri zote. Aidha, Serikali itachagua miradi michache ya kuanza nayo ili kupata uzoefu wa uendeshaji wa miradi hiyo. Maeneo tunayotarajia kuanza nayo ni barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege, maji pamoja na ujenzi wa ofisi.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kutumia fursa hii kuziomba Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhamasisha Sekta Binafsi kushiriki katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa kuzingatia taratibu na kanuni zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme juu ya usimamizi wa Deni la Taifa. Katika kutekeleza azma yake ya kuboresha miundombinu ya kimkakati, Serikali imeendelea kukopa kutoka nje na ndani ya nchi ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Hadi mwishoni mwa Machi 2012, Deni la Taifa lilikuwa shilingi bilioni 20,276.6 ikilinganishwa na deni la shilingi bilioni 17,578.9 Machi 2011 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 15.4. Kati ya hizo, shilingi bilioni 15,306.9 zilikuwa ni deni la nje na shilingi bilioni 4,969.7 ni deni la ndani. Kati ya kiasi cha deni la nje, shilingi bilioni 12,342.5 zilikuwa ni deni la umma na kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 2,964.4 ni deni la sekta binafsi. Aidha, hadi kufikia Machi 2012, deni la ndani la Serikali lilifikia shilingi bilioni 4,969.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 4,496.5 mwezi Machi, 2011, hii ni sawa na ongezeko la asilimia 10.5. Sababu kubwa ya kuongezeka kwa deni la taifa ni mikopo mipya kwa ajili ya kugharimia miradi ya maendeleo na utumiaji wa dhamana za muda mfupi za Serikali kwa ajili ya kudhibiti mfumuko wa bei katika uchumi na kushuka kwa thamani ya shilingi kuliongeza deni la nje, hizo ndiyo sababu.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Deni la Taifa linasimamiwa vizuri, mwezi Februari, 2012, Serikali ilifanya Tathmini ya Uhimilivu wa Deni (*Debt Sustainability Analysis*) likijumuisha dhamana zinazotolewa na Serikali kwa Wizara, Mashirika na Taasisi za Umma ambapo matokeo ya tathmini hiyo yanaonesha kuwa Deni la Taifa linahimilika. Tuna vigezo kwa nafasi mbalimbali tutaonyesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa Mashirika ya Umma. Katika kuhakikisha Taasisi, Wakala na Mashirika ya Umma yanatekeleza majukumu yao, Serikali imetoa Waraka Na.1 wa mwaka 2012 unaoelekeza Wizara mama na Bodi za Wakurugenzi kuingia katika mikataba ya utendaji, Waraka huo umeanza kutumika Januari, 2012. Aidha, ukaguzi wa kiutendaji (*Management Audit*) katika Taasisi za Serikali umefanyika kwa baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma kwa kuangalia uzingatiaji wa kanuni, Sheria na miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali ikiwa ni pamoja na uwajibikaji na utawala bora, matumizi ya fedha na taratibu za ajira. Zoezi hili ni endelevu na linalenga kuboresha uendeshaji wa Mashirika na Taasisi za Serikali. Kadhalika, Serikali imefanya uhakiki wa mashirika 170 yaliyobinafsishwa. Kati ya hayo, mashirika 41 yalikutwa yanajiendesha kwa faida, mashirika 66 yanajiendesha kwa hasara na mashirika 63 yalikuwa mufilisi. Kwa yale ambayo yanaendeshwa kwa hasara yatawekwa chini ya mfilisi kwa lengo la kuyachambua na kupendekeza hatua za kuchuliwa. Aidha, kwa yale yaliyokuwa mufilisi hatua za kuyafilisi zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa uniruhusu nizungumzie juu ya bajeti ya mwaka 2012/2013. Bajeti ya mwaka 2012/2013 itazingatia vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2012/2013; Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA II); Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 na program za maboresho katika sekta ya umma. Lengo likiwa ni kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Mheshimiwa Spika, pamoja na miongozo hiyo, bajeti hii inazingatia pia changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2011/2012. Changamoto hizo ni pamoja na upatikanaji wa umeme wa uhakika; kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la Dunia; uhaba wa chakula katika baadhi ya maeneo; kupanda kwa bei za bidhaa na huduma; kutopatikana kwa wakati fedha za kugharamia miradi ya maendeleo kulikosababishwa na masharti magumu na urasimu kwa mikopo ya kibiashara; na kuongezeka kwa malimbikizo ya madeni ya ndani, hususan ya wazabuni, wakandarasi na watumishi. Mambo mengine yaliyozingatiwa ni pamoja na mwenendo wa uchumi wa dunia na makubaliano ya kikanda na kimataifa. Serikali imepanga hatua mbalimbali za kuchukua kukabiliana na changamoto hizo kama nitakavyoeleza hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, shabaha na malengo ya bajeti ya mwaka 2012/2013. Bajeti ya mwaka 2012/2013, imejielekeza katika kufikia shabaha na malengo yafuatayo:-

(i) Kukuza pato halisi la Taifa kwa asilimia 6.8 mwaka 2012 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.4 mwaka 2011;

(ii) Kuimarisha miundombinu ya uchumi, ikijumuisha umeme, barabara, reli na bandari;

(iii) Kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha;

(iv) Kuongezeka kwa mapato ya ndani yatakayofikia uwiano na Pato la Taifa wa asilimia 18 kwa mwaka 2012/2013 kulinganisha na mwelekeo wa asilimia 16.9 mwaka 2011/2012;

(v) Kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei ili urudi kwenye viwango vya tarakimu moja;

(vi) Kuwa na kiwango tengemavu cha ubadilishaji wa fedha kitakachotokana na mwenendo wa soko la fedha;

(vii) Kukua kwa mikopo kwa sekta binafsi kwa kiwango cha asilimia 20 ya Pato la Taifa mwishoni mwa Juni 2013 sambamba na jitihada za kudhibiti mfumuko wa bei;

(viii) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne na nusu;

(ix) Kuimarisha utaratibu wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (*PPP*) ili kupanua fursa za kuchangia utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(x) Kuboresha mazingira ya wafanya biashara wadogo na wa kati;

(xi) Kulinda na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika Sekta za huduma za jamii;

(xii) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji; na

(xiii) Kujenga uwezo wa nchi kukabiliana na misukosuko ya kiuchumi na kifedha pamoja na kushiriki kwa ufanisi katika ushirikiano kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, niruhusu sasa nizungumze juu ya misingi ya bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2012/2013. Ili kufikia malengo yaliyoainishwa hapo juu, misingi ya bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2012/2013 ni hii ifuatayo:-

(i) Kuendelea kuimarika kwa utengamavu wa viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya jamii;

(ii) Kuwepo kwa nishati ya umeme wa uhakika na kuhamasisha matumizi ya gesi asilia;

(iii) Kuimarika kwa utekelezaji wa Sera za Fedha na Bajeti;

(iv) Kuendelea kuimarika kwa mahusiano na Washirika wa Maendeleo;

(v) Kuendelea kutekeleza Sera ya Ugatuaji wa madaraka kwa wananchi;

(vi) Kuendelea kutekeleza maboresho katika sekta ya umma ikiwa ni pamoja na kuendelea kuimarika kwa usimamizi wa fedha za umma; na

(vii) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara pamoja na kuongezeka kwa tija na fursa za uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na azma yake ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuchukua hatua mbalimbali katika maeneo ya mapato yatokanayo na kodi na yasiyotokana na kodi; na kupanua wigo wa makusanyo. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha taratibu za kukusanya mapato pamoja na kupunguza misamaha ya kodi ili kuweza kugharamia kwa kiwango kikubwa matumizi ya kawaida kwa kutumia mapato ya ndani. Sera za mapato zitakazozingatiwa kwenye Bajeti ya mwaka 2012/13 ni pamoja na:-

(i) Kuboresha mifumo ya ukusanyaji na usimamiaji wa mapato yasiyo ya kodi kwa kupitia upya mfumo wa utoaji stakabadhi na leseni, pamoja na kuboresha viwango vya kubakiza maduhuli kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali;

(ii) Kupanua wigo wa kodi kwa kuendelea kurasimisha sekta isiyo rasmi ili iingie kwenye mfumo wa kodi;

(iii) Kuendelea kufanya mapitio ya sheria za Wakala/Taasisi za Umma zinazokusanya maduhuli ili ziweze kuchangia zaidi kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali;

(iv) Kuendelea kufanya mapitio ya sheria mbalimbali zinazotoa misamaha ya kodi kwa lengo la kudhibiti na kupunguza misamaha hiyo;

(v) Kupitia upya mfumo wa ukusanyaji wa kodi ya majengo katika Majiji, Manispaa, Miji, Wilaya na Miji Midogo ili kuuboresha zaidi;

(vi) Kufanya mapitio ya vyanzo vya mapato na mfumo wa ukusanyaji katika Serikali za Mitaa ili kuongeza mapato; na

(vii) Kujenga uwezo wa Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati na Madini, Shirika la Maendeleo la Petroli Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Wakala wa Ukaguzi wa Madini ili kusimamia ukusanyaji wa mapato katika maeneo ya madini, gesi na petroli.

Mheshimiwa Spika, hatua za kuboresha uzalishaji na huduma. Serikali imepokea mapendekezo kutoka kwa wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge kuhusu haja ya kuboresha mazingira ya uzalishaji katika Sekta za Uvuvi, Viwanda, Kilimo, Mifugo na Utalii. Hatua ambazo Serikali imepanga kuchukuwa ni pamoja na:-

(i) Kupitia upya vivutio kwa sekta ya viwanda vya ndani vinavyotumia malighafi za ndani vikiwemo viwanda vya nguo na mafuta ya kula;

(ii) Kutafuta utaratibu mzuri wa kubainisha vipuri vya mashine na mitambo inayosamehewa kodi ili kuondoa usumbufu wanaoupata waagizaji;

(iii) Kupitia upya viwango vya kodi katika sekta ya Kilimo na Uvuvi kwa lengo la kuviwianisha na kupunguzwa;

(iv) Kupitia upya maudhui na viwango vya Tozo ya Kuendeleza Stadi (*Skills Development Levy)* na Leseni ya Magari (*Motor Vehicle Licence*). Kwa kufanya hivyo, Serikali inalenga katika kupanua wigo wa kodi, kuwapunguzia mzigo waajiri na kupanua ajira hapa nchini. Aidha, mapitio ya Leseni za Magari yatazingatia kurejea madhumuni ya kuanzishwa kwa leseni hiyo; na

(v) Kufanya mapitio ya Sheria ya VAT kwa lengo la kuibadili kwa kuzingatia uzoefu wa kimataifa "*Best Practice*".

Mheshimiwa Spika*,* Mamlaka za Serikali za Mitaa zinahimizwa kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuzingatia fursa zilizopo. Aidha, OWM – TAMISEMI kwa kushirikiana na Shirika la Misaada na Utaalamu la Ujerumani – GIZ watakamilisha na kusambaza kwenye Halmashauri mfumo wa kompyuta wa utunzaji kumbukumbu za mali na majengo (*Integrated Property Rating Information Management System - IPRIMS*) ili kuboresha ukusanyaji wa mapato hususan kodi ya majengo. Natoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na viongozi wengine wa ngazi mbalimbali kuweka msukumo utakaowezesha Halmashauri kukusanya kikamilifu kodi ya majengo pamoja na mapato mengine ili kuziongezea uwezo wa kuhudumia wananchi na kuwaletea maendeleo endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia sera za mapato zilizoainishwa hapo juu, Serikali inalenga kukusanya mapato ya ndani (bila kujumuisha Halmashauri) shilingi bilioni 8,714.7 sawa na asilimia 18 ya Pato la Taifa. Kati ya kiwango hicho, mapato ya kodi shilingi bilioni 7,080.1 na mapato yasiyo ya kodi shilingi bilioni 644.6. Mapato yanayotokana na vyanzo vya Halmashauri shilingi bilioni 362.2 sawa na asilimia 0.7 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya ndani. Serikali itaendelea na utaratibu wake wa kukopa katika soko la ndani la fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na kulipia hatifungani za Serikali na dhamana za Serikali za muda mfupi zinazoiva. Katika mwaka 2012/2013, Serikali inakusudia kukopa kiasi cha shilingi bilioni 1,632 kutoka soko la fedha la ndani. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 483.9 sawa na asilimia moja ya Pato la Taifa ni kwa ajili ya kugharimia miradi ya maendeleo na kiasi cha shilingi bilioni 1,148.1 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani za Serikali na dhamana za Serikali za muda mfupi zinazoiva. Kiwango hiki kimezingatia viashiria vya kiuchumi pamoja na kuhakikisha kuwa Taasisi za Fedha zinaendelea kutoa mikopo kwa Sekta binafsi ili kuchochea ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo mipya yenye masharti nafuu. Serikali itaendelea kushirikiana na Washirika wa Maendeleo ili kuhakikisha Misaada na mikopo inapatikana kwa wakati na kuchangia katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Katika bajeti ya mwaka 2012/2013, Serikali inatarajia kupata kiasi cha shilingi bilioni 3,156.7 kutokana na misaada na mikopo yenye masharti nafuu. Kati ya fedha hizo, Misaada na mikopo ya kibajeti ni shilingi bilioni 842, sawa na Dola za Marekani milioni 495. Misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikijumuisha mifuko ya kisekta inatarajiwa kuwa shilingi bilioni 2,314.2.

Mheshimiwa Spika, pamoja na misukosuko ya kiuchumi na majanga ya kiasili iliyozikumba nchi Wahisani, bado zimeendelea kutoa misaada na mikopo kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Napenda kuwatambua washirika wetu wa maendeleo ambao ni: Uingereza, Norway, Canada, Marekani, Uholanzi, Ubelgiji, China, Finland, Ufaransa, Ujerumani, Ireland, Japani, Korea ya Kusini, Denmark, Hispania, Sweden, Uswisi, India, Italia, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika,

Umoja wa Ulaya, *Global Funds,* Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF),* BADEA, Kuwait Fund, Nordic Fund, *Opec Fund, Saudi Fund* na Mashirika ya Umoja wa Mataifa. Tunawashukuru Sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara. Sera ya Serikali ni kutafuta mikopo nafuu kutoka mashirika na nchi wahisani kwa ajili ya kugharamia bajeti yake ya maendeleo. Hata hivyo, kwa kuzingaita mahitaji makubwa ya kuendeleza miradi ya miundombinu kwa mwaka 2012/2013, Serikali inatarajia kupata kutoka nje mikopo yenye masharti ya kibiashara kiasi cha shilingi bilioni 1,254.1 sawa na Dola za Marekani milioni 749. Fedha hizi zitatumika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2012/2013 ikijumuisha mchango wa Serikali (*counterpart fund)* katika ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam, mradi wa maji wa Ruvu chini na ujenzi wa barabara. Uamuzi wa kuendelea kukopa kwa masharti nafuu na ya kibiashara unazingatia uhimilivu wa Deni la Taifa uliopo.

Mheshimiwa Spika, sasa nitazungumzia sera za matumizi. Katika mwaka 2012/2013, sera za matumizi zitazingatia yafuatayo:-

(i) Matumizi yataendelea kuzingatia mapato halisi yanayopatikana;

(ii) Nakisi ya bajeti haitazidi asilimia 5.5 ya Pato la Taifa, ikijumuisha ruzuku;

(iii) Mafungu yataendea kuzingatia viwango vya matumizi vitakavyoidhinishwa na Bunge;

(iv) Maafisa Masuuli wataendelea kuzingatia Sheria ya Fedha na ya Ununuzi wa Umma; na

(v) Serikali inaendelea kukusanya madeni yote kwa lengo la kuyahakiki na kuyapangia utaratibu wa kuyalipa.

Mheshimiwa Spika*,* matumizi ya kawaida. Sera za matumizi ya kawaida kwa mwaka 2012/2013, zinalenga pamoja na mambo mengine katika kugharamia mishahara; madeni ya mikopo ya ndani na nje; uboreshaji wa huduma za kiuchumi na maendeleo ya jamii; mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu; mitihani ya shule za msingi na sekondari; ununuzi na usambazaji wa dawa; mahitaji ya Tume ya Kuratibu Mabadiliko ya Katiba; matengenezo ya mali ya Serikali; ununuzi wa chakula cha hifadhi; mahitaji ya kawaida kwenye miradi iliyokamilika; pamoja na kuendelea kulipa madai mbalimbali ya watumishi na wazabuni.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu, kilimo kisichokuwa na tija na ukosefu wa ajira, Serikali imetenga fedha katika maeneo yafuatayo: Shilingi bilioni 30 kwa ajili ya Benki ya Rasilimali; shilingi bilioni 40 kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo na hivyo kufikisha mtaji wa shilingi bilioni 100. Aidha, shilingi bilioni 7.5 zimetengwa kwa ajili ya kurejesha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa sheria, ambapo katika awamu ya kwanza vijana 5,000 wanatarajiwa kujiunga. Vilevile, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 70.7 katika maeneo mapya ikiwa ni Mikoa, Wilaya na Halmashauri kugharamia matumizi ya kawaida na maendeleo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matumizi ya maendeleo. Katika hotuba ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2011 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2012/13, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, aliainisha miradi ya kitaifa ya kimkakati pamoja na miradi katika maeneo muhimu ya ukuaji wa uchumi. Bajeti hii itazingatia vipaumbele hivyo:-

(i) Mheshimiwa Spika, kwanza ni miundombinu. Umeme - mkazo utawekwa katika upatikanaji wa umeme wa kuhakika kwa kuongeza uzalishaji, usafirishaji na usambazaji ambapo jumla shilingi bilioni 498.9 zimetengwa kwa ajili hiyo. Aidha, Serikali itatekeleza mradi wa ujenzi wa Bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam kwa mkopo kutoka Benki ya Exim ya China wenye

thamani ya Dola za Marekani milioni 1,225.3 utakaosimamiwa na *TPDC*. Mpaka sasa tuko katika hatua ya mwisho ya kushughulikia mkataba.

(ii) Usafirishaji na uchukuzi – uimarishaji wa reli ya kati ikijumuisha ukarabati wa injini na mabehewa ya treni. Kwa upande wa barabara, miradi inayopewa kipaumbele ni pamoja na barabara zenye kufungua fursa za kiuchumi. Katika usafiri wa anga na majini, miradi itakayotekelezwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege na uendelezaji wa gati ya Ziwa Tanganyika. Jumla ya shilingi bilioni 1,382.9 zimetengwa katika eneo hili.

(iii) Maji safi na salama - kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini. Kiasi cha shilingi bilioni 568.8 kimetengwa.

(iv) Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) – kuimarisha mawasiliano kwa kutumia TEHAMA ili kuboresha upatikanaji wa huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa taarifa za masoko ya ndani na nje ya nchi; ukusanyaji wa mapato; huduma za afya; elimu; huduma za kifedha; na kadhalika. Jumla ya shilingi bilioni 4 zimetengwa katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, pili, kilimo, uvuvi na ufugaji. Kwa kushirikiana na sekta binafsi, Serikali itawekeza katika kilimo cha mpunga na miwa katika mabonde makuu ya Wami, Ruvu, Kilombero na Malagarasi pamoja na kuongeza tija na thamani, kubadilisha mfumo wa kilimo na kukuza kilimo cha misitu. Hii ni pamoja na kuendeleza shughuli za ufugaji na uvuvi ili ziwe na tija kwa kuboresha mazingira ya uwekezaji; kwa kufanya hivyo kutapunguza umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Spika, katika vitabu haionyeshi lakini tumetenga shilingi bilioni 262.2 kwa ajili ya *sub-sector* hii ya kilimo, uvuvi na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula pamoja na kuhakikisha usalama wa chakula, Serikali itaimarisha utekelezaji wa dhana ya Kilimo Kwanza kwa kuhakikisha kwamba nguzo zake zote zinaendelea kuzingatiwa; kuhakikisha kwamba walengwa wanapata pembejeo kwa wakati; Maafisa ugani kutakiwa kuwa na mashamba yao ya mfano (mashamba darasa) ili kuwaelimisha wakulima kilimo cha kisasa; kuongeza msukumo kwenye kilimo cha umwagiliaji ili wakulima waweze kufanya shughuli zao za kilimo katika misimu yote badala ya kutegemea mvua; Kuimarisha masoko ya mazao kupitia Bodi ya Mazao Mchanganyiko ambayo imeshaanza shughuli zake; na Mikoa kutakiwa kuendelea kutenga ardhi na vijiji kutakiwa kupima na kurasimisha ardhi kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na wa nje. Kiasi cha shilingi bilioni 192.2 kimetengwa katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, tatu, maendeleo ya viwanda, Serikali inakusudia kuendeleza viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana nchini; viwanda vinavyoongeza thamani ya madini; viwanda vikubwa vya saruji; na viwanda vya eletroniki na TEHAMA pamoja na kuboresha mazingira ya biashara na kutenga maeneo maalum ya uwekezaji mijini na vijijini na kukuza ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Hatua hii inaenda sambamba na kuboresha na kuimarisha viwanda vidogo vidogo nchini. Jumla ya shilingi bilioni 128.4 zimetengwa katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, nne, maendeleo ya rasilimali watu na huduma za jamii. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali imepanga kuboresha viwango vya elimu katika ngazi zote hususan katika maeneo ya utafiti, ufundi stadi, afya; sayansi na ujuzi maalum kuhusu madini, gesi, urani, chuma na mafuta; hatua hii inajumuisha ukarabati wa maabara na upatikanaji wa vifaa vya maabara. Shilingi bilioni 84.1 zimetengwa katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, tano, utalii. Serikali itaendelea kuboresha huduma zitolewazo katika eneo hili ikiwa ni pamoja na kutangaza utalii na kuboresha mazingira ya kitalii na kutoa mafunzo ya utalii, kuainisha maeneo mapya ya utalii na kuboresha vyuo vya utalii.

Mheshimiwa Spika, huduma za fedha. Serikali itaendelea kuimarisha huduma za kifedha hususan mifumo ya kuweka akiba na kukopa kama vile *SACCOS, VICOBA* na benki za kijamii ili

kuwawezesha wananchi kupata mitaji kwa ajili ya biashara na uzalishaji. Kiasi cha shilingi bilioni 2.6 zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha mtaji wa Benki ya Wanawake, Mradi wa *SELF* na Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Aidha, Wizara ya Fedha itaendelea kusimamia maendeleo ya Taasisi za fedha zinazojihusisha na utoaji wa mikopo kwa wajasiriamali. Ili kufanikisha hili kitengo kilichopo cha maendeleo ya sekta ya fedha kitahuishwa na kuwa idara kamili.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa fedha za umma. Serikali itaendelea kutekeleza awamu ya nne ya Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma na kuhakikisha kwamba Sheria ya Fedha za Umma na Sheria ya Ununuzi wa Umma zinafuatwa kikamilifu ili kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma. Maeneo yanayozingatiwa kwenye programu hiyo ni pamoja na: kuendelea kuboresha mtandao wa malipo *(IFMS)* ili kuimarisha udhibiti wa matumizi ya fedha za umma kwa Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa; utoaji wa mafunzo ya ulipaji kwa mfumo wa malipo wa kibenki kwa watumishi wa Ofisi za Bunge, Sekretarieti za Mikoa, Idara ya Ushirika, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na Ofisi za Hazina ndogo Mikoa yote. Aidha, Serikali itaendelea kutoa mafunzo ya kuandaa hesabu kwa kutumia viwango vya uhasibu vya kimataifa ili kuongeza uwazi katika matumizi ya fedha za Umma; kuijengea uwezo Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali katika kuhakikisha kanuni na taratibu za matumizi ya fedha za umma zinazingatiwa ipasavyo; na kujenga uwezo wa Serikali Kuu, Mikoa na Halmashauri katika eneo la uandaaji wa mipango na bajeti, ukusanyaji wa mapato, usimamizi wa rasilimali, uboreshaji wa mawasiliano na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha utaratibu wa kupeleka fedha kwenye Halmashauri na kutoa taarifa mapema kuhusu matumizi ya fedha zilizopelekwa. Aidha, fedha zote zitakazovuka mwaka bila kutumika zitatolewa taarifa kwenye vikao vya Kamati za Kudumu na Baraza la Madiwani ili kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali itaendelea na zoezi la uhakiki wa watumishi kwenye Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote ili kuondoa watumishi wasiostahili kwenye orodha ya malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali. Aidha, mamlaka za ajira na maafisa masuuli wanaelekezwa kusitisha malipo kwa watumishi walioacha au kuachishwa kazi, kustaafu, kufariki au likizo bila malipo ili kuzuia upotevu wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika***,*** Serikali itaendelea kutilia mkazo wa ukaguzi wa mapato na matumizi ya fedha za umma katika Wizara, Taasisi, Wakala, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuthibitisha endapo fedha zinazopangwa kukusanywa zinapatikana na pia fedha zinazotumwa kutoka Hazina zinafika na kutekeleza shughuli zilizoidhinishwa. Serikali itaboresha mifumo ya udhibiti na usimamizi wa fedha za umma zinazokusanywa au kupelekwa kwenye Mikoa na Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa Mashirika ya Umma. Katika kukabliana na changamoto za usimamizi wa Mashirika ya Umma, Serikali inaendelea kuimarisha Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kufanya mapitio ya Sheria za Msajili wa Hazina ambazo ni "*Treasury Registrar Ordinance"* ya mwaka 1958 na *"Treasury Registrar Powers and Functions"* Sura 370 ya mwaka 2000 kama ilivyorekebishwa mwaka 2010 ili kuwa na Sheria moja. Lengo la hatua hiyo ni kuimarisha ofisi kwa kuipa nguvu zaidi za kisheria kuweza kusimamia ipasavyo utendaji wa Mashirika ya Umma pamoja na Taasisi ili kuongeza tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kukabiliana na mfumuko wa bei**.** Uchumi wetu unakabiliana na changamoto nyingi ikiwemo mfumuko wa bei ambao kwa wastani umeshuka kutoka asilimia 19.8 mwezi Desemba 2011 hadi asilimia 18.7 mwezi Aprili 2012. Kichocheo kikubwa cha mfumuko wa bei ni kupanda kwa bei za umeme, mafuta na vyakula hususan mchele na sukari. Kwa mfano kwa mwezi Aprili 2012, chakula kimechangia asilimia 24.7 wakati umeme na mafuta vimechangia kwa asilimia 24.9. Mfumuko wa bei ambao haujumuishi chakula na nishati bado uko kwenye tarakimu moja ambayo ni asilimia 8.8. Hivyo, jitihada za Serikali zitaelekezwa katika kukabiliana na kupanda kwa bei ya bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, hatua za haraka ambazo Serikali itachukua ni pamoja na kutoa vibali vya uagizaji wa sukari na mchele kutoka nje na kuendelea kuimarisha Hifadhi ya Chakula ya Taifa.

Aidha, Serikali itawekeza katika kilimo cha mpunga na miwa katika mabonde makuu ya Kilombero, Wami, Kagera na Malagarasi pamoja na miradi ya kilimo cha umwagiliaji. Hatua nyingine ni pamoja na kuendelea kuimarisha miundombinu ya usafirishaji na masoko; kuimarisha mfumo wa masoko kwenye maeneo yanayozalisha chakula kwa wingi hususan Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na mipakani. Kwa upande wa nishati ya umeme, Serikali itaendeleza vyanzo mbadala vya umeme kama vile umeme wa gesi, nguvu za jua, upepo, miwa ili kupunguza matumizi ya mafuta kama chanzo cha nishati.

Mheshimiwa Spika, kupanua fursa za ajira. Ili kuongeza ajira hasa kwa vijana, Serikali itaendelea kupanua huduma za fedha ikiwa ni pamoja na kuanzisha Benki ya Kilimo na kuongeza mitaji kwa Benki za Rasilimali, Wanawake, Posta na Twiga Bancorp. Hatua nyingine zitakazochukuliwa na kuchangia ongezeko la ajira ni pamoja na kujenga miundombinu ya barabara, umeme, kilimo na mawasiliano. Aidha, sekta binafsi itahamasishwa kutumia fursa zinazotolewa na Benki na Maendeleo ya Afrika kupitia Dirisha la kuendeleza sekta binafsi. Kadhalika, Serikali itaajiri watumishi 71,756 katika sekta za elimu, afya, kilimo na kada nyingine.

Mheshimiwa Spika, maboresho ya mfumo wa kodi, ada, tozo na hatua nyingine za mapato. Katika miaka ya hivi karibuni, Serikali imefanya maboresho katika mfumo wa kodi kwa nia ya kupanua wigo wa kodi na kuongeza mapato ya ndani. Maboresho yaliyofanywa ni pamoja na marekebisho ya sheria za kodi, kanuni na taratibu za usimamiaji wa kodi. Aidha, hatua hizi zimechangia katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi. Hata hivyo kuna changamoto katika kuhuisha mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa bajeti hatua kwa hatua. Kwa kuzingatia hali hiyo Serikali itaendelea kuchukua hatua zenye kuboresha sera za kodi na usimamiaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika**,** ili kuendeleza mafanikio yaliyopatikana kwenye mfumo wa kodi, napendekeza kufanya maboresho katika sheria mbalimbali za kodi kama ifuatavyo:-

(a) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148;

(b) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332;

(c) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147;

(d) Sheria ya Ushuru wa Mauzo Nje, Sura 196;

(e) Sheria ya Kodi ya Michezo ya Kubahatisha *(Gaming Act),* Sura, 41;

(f) Sheria ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura, 124;

(g) Sheria ya Ushuru wa Viwanja vya Ndege, Sura, 365;

(h) Misamaha ya Kodi ya magari kupitia sheria za kodi na matangazo ya Serikali (*GNs*);

(i) Marekebisho mengine katika baadhi ya sheria za kodi na sheria za Usimamizi wa Fedha; na

(j) Marekebisho ya Ada na Tozo Mbalimbali za Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea.

(k) Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika*,* Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148. Napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 kama ifuatavyo: -

(i) Kuanzisha kiwango kipya *(VAT Rate)* cha asilimia 10 cha Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa baadhi ya watu, taasisi na mashirika yanayopata unafuu wa kodi hiyo *(special*

*relief).* Kwa mantiki hiyo, wale waliokuwa hawalipi kodi hiyo kuanzia sasa watalipa asilimia 10. Hatua hii itazihusu Kampuni binafsi, watu binafsi na Kampuni zitakazopewa vyeti vya Kituo cha Uwekezaji Tanzania isipokuwa zile zenye vyeti hivyo kwa sasa. Aidha, itahusu pia Mashirika yasiyo ya Kiserikali isipokuwa yale yaliyopewa msamaha wa kodi pale yanapotoa huduma ya chakula, dawa baridi na vifaa kama vile sabuni ambavyo vinatolewa msaada kwenye vituo mahsusi vya kulelea watoto yatima na shule; *(Makofi)*

(ii) Kurekebisha kifungu cha 19 cha Jedwali la Pili la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kuongeza Mashine za Elektroniki za kutoa Stakabadhi za Kodi *(Electronic Fiscal Devices - "EFDs")* katika orodha ya vifaa vinavyopata msamaha wa kodi hiyo. Lengo ni kuwawezesha walipa kodi kupata vifaa hivi kwa gharama nafuu na kuhamasisha matumizi yake kwa kuwa ni muhimu katika kutoa stakabadhi za mauzo ya bidhaa na huduma;

(iii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa vifaa vitakavyotumika kwa ajili ya gesi iliyoshindiliwa na gesi ya mabomba *(Compressed Natural Gas and Piped Natural Gas).* Msamaha wa kodi unatolewa ili kuhamasisha matumizi ya gesi katika magari, kupikia, nyumbani, taasisi na viwandani. Aidha, Shirika la Maendeleo ya Petroli *(TPDC)* litawajibika kuhakiki vifaa hivyo ili kuhakikisha kwamba vitatumika kujenga miundombinu ya gesi.

Mheshimiwa Spika**,** mitambo na vifaa vya kujenga miundombinu ya gesi asili vinavyoombewa msamaha wa kodi ni kama ifuatavyo:-

(i) *CNG vehicles conversion kits* – vifaa vinavyoongezewa kwenye magari yaweze kutembea kwa kutumia nishati ya gesi asili;

(ii) *High pressure vessels (CNG and LPG cylinders)* – mitungi maalumu ya kutunzia gesi asili iliyoshindiliwa na gesi ya LPG;

(iii) *Natural Gas Compression plants equipments* – vifaa kwa ajili ya mitambo ya kushindilia gesi asili;

(iv) *Natural gas pipes (Transportation and Distribution pipes*) – mabomba maalum ya kusafirishia na kusambazia gesi asili;

(v) *CNG storage cascades* – mitungi maalum ya pamoja ya kusafirishia na kuhifadhia gesi asili iliyoshindiliwa;

(vi) *CNG transportation trailers* - magari na matela ya kusafirishia gesi asili iliyoshindiliwa;

(vii) *Natural gas metering equipments* – mita za kupimia kiasi cha gesi asili;

(viii) *Pipeline fittings and valves* – vifaa vya kuunganishia mabomba na kuruhusu/kuzuia gesi kupita;

(ix) *CNG Refueling/filling equipment* – vifaa vya kujazia gesi asili kwenye magari;

(x) *PNG/CNG accessories* – vifaa vidogo vidogo vinavyotumika katika ujenzi wa mabomba ya gesi asili na katika mitambo ya kushindilia gesi asili;

(xi) *Gas Receiving Unit* – vifaa vya kupokelea gesi ya mabomba;

(xii) *Condensate Stabilizer* – vifaa vya mifumo ya kuimarisha uhifadhi wa *condensate*;

(xiii) *Flare Gas System* – vifaa kwa ajili ya mifumo ya kuunguza gesi kwa ajili ya usalama;

(xiv) *Air & Nitrogen System* – vifaa vya mifumo ya hewa na ya *Nitrogen*;

(xv) *Condensate Tanks and Loading Facility* – matanki ya kuhifadhia *condensate* na vifaa vya kupakilia;

(xvi) *System piping on piperack* – mifumo ya kubeba mabomba ya gesi asili;

(xvii) *Instrumentation* – vifaa vya umeme na udhibiti kwenye mifumo ya gesi asili; na

(xviii) Majiko yaliyotengenezwa mahsusi kwa ajili ya matumizi ya gesi pekee.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi katika Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa pamoja zitaongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 22,565.1

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332. Napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kama ifuatavyo:-

(i) Kuweka kiwango cha chini cha mapato ghafi ya wafanyabiashara wadogo cha shilingi 3,000,000 kisichotozwa kodi na kurekebisha matabaka (*bands*) ya walipa kodi. Lengo la hatua hii ni kulinda mapato halisi ya Serikali na kuhakikisha kwamba wenye mapato ya chini ya kiwango cha kutozwa kodi cha shilingi 3,000,000 hawatozwi kodi chini ya mfumo wa Kukadiria kodi Walipa kodi wadogo "*Presumptive Scheme*" kama ilivyo kwenye mapato yatokanayo na ajira. Hivi sasa Wafanyabiashara wenye kipato hicho wanatozwa Sh. 35,000.

Viwango vya sasa na vinavyopendekezwa ni kama ifuatavyo:-

**Viwango vya sasa**

| | Thamani ya Mauzo | Kodi kwa wasiokuwa na kumbukumbu za mauzo | Kodi kwa wenye kumbukumbu za mauzo |
|---|---|---|---|
| (i) | Kwa mauzo yasiyozidi Shs. 3,000,000/= | Shs. 35,000/= | 1.1% ya mauzo |
| (ii) | Kwa mauzo yanayozidi Shs. 3,000,000/= na yasiyozidi Shs. 7,000,000/= | Shs. 95,000/= | Shs. 33,000/= + 1.3% ya mauzo yanayozidi Shs. 3,000,000/= |
| (iii) | Kwa mauzo yanayozidi Shs. 7,000,000/= na yasiyozidi Shs. 14,000,000/= | Shs. 291,000/= | Shs. 85,000/= + 2.5% ya mauzo yanayozidi 7,000,000/= |
| (iv) | Kwa mauzo yanayozidi Shs. 14,000,000/= na yasiyozidi Shs. 20,000,000/= | Shs. 520,000/= | Shs. 260,000/= + 3.3% ya mauzo yanayozidi Shs. 14,000,000/= |

**Viwango vinavyopendekezwa**

| | Thamani ya Mauzo | Kodi kwa wasiokuwa na kumbukumbu za mauzo | Kodi kwa wenye kumbukumbu za mauzo |
|---|---|---|---|
| (i) | Kwa mauzo yasiyozidi Shs. 3,000,000/= | Asilimia sifuri (0%) | Asilimia sifuri (0%) |
| (ii) | Kwa mauzo yanayozidi Shs 3,000,000/= na yasiyozidi Shs 7,500,000/= | Shs. 100,000/= | 2% ya mauzo yanayozidi Shs 3,000,000/= |
| (iii) | Kwa mauzo yanayozidi Shs 7,500,000/= na yasiyozidi Shs 11,500,000/= | Shs. 212,000/= | Shs. 90,000/= plus 2.5% ya mauzo yanayozidi Shs 7,500,000/= |
| (iv) | Kwa mauzo yanayozidi Shs 11,500,000/= na yasiyozidi Shs 16,000,000/= | Shs. 364,000/= | Shs. 190,000/= + 3.0% ya mauzo yanayozidi Shs 11,500,000/= |
| (v) | Kwa mauzo yanayozidi Shs 16,000,000/= na yasiyozidi Shs 20,000,000/= | Shs. 575,000/= | Shs. 325,000/= + 3.5% ya mauzo yanayozidi Shs 16,000,000/= |

(ii) Kutoza Kodi ya Zuio ya asilimia 10 kwenye mapato yatokanayo na riba inayotolewa na mabenki kwa wafanyabiashara ambao si wakaazi (*non-residents*). Lengo ni kuweka usawa kwa walipa kodi wote. *(Makofi)*

(iii) Kufanya marekebisho ya kifungu cha 54 (2) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ili kufuta msamaha wa Kodi ya Mapato kwa makampuni yenye hisa zipatazo asilimia 25 au zaidi. Lengo la marekebisho haya ni kuleta usawa kwa walipa kodi wanapopata gawio.

(iv) Kuanzisha kodi itokanayo na uuzaji wa rasilimali ya uwekezaji (*capital gains tax*) kwenye uuzaji wa hisa za kampuni za ndani unaofanywa na Kampuni mama zilizo ya nje ya nchi. (*Makofi*)

(v) Kuongeza kima cha chini cha kutozwa kodi (*threshold)* kwenye mapato ya ajira kutoka shilingi 135,000 hadi 170,000. Hatua hii itaongeza kipato kwa mfanyakazi.

(vi) Kutoa msamaha wa Kodi ya Mapato kwa soko la Hisa la Dar es Salaam *(Dar es salaam Stock Exchange*). Lengo ni kulifanya soko hilo kukua.

(vii) Kusamehe Kodi ya Mapato (kwa wenye leseni) yatokanayo na michezo ya kubahatisha iliyokwishalipiwa kodi chini ya Sheria ya Kodi ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41. Lengo la hatua hii ni kuepusha wenye leseni za biashara ya michezo ya kubahatisha kulipa kodi mara mbili.

(viii) Kusamehe Kodi ya Zuio kwenye riba ya mikopo inayotozwa na mabenki ya nje kwa wawekezaji wanaowekeza kwenye sekta na shughuli muhimu katika mkakati wa kukuza uchumi *(Strategic Investors).* Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wawekezaji hao wanapopata mikopo kutoka kwenye mabenki ya nje ya nchi na hivyo kuhamasisha uwekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi za Kodi ya Mapato zitaongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 105,672.3

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147. Napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 kama ifuatavyo:-

(i) Kufuta Ushuru wa bidhaa uliokuwa unatozwa kwenye mafuta mazito ya kuendeshea mitambo. Hivi sasa mafuta hayo yanatozwa ushuru wa bidhaa wa shilingi 40 kwa lita. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uzalishaji katika viwanda hapa nchini. Aidha, hatua hii itaongeza uzalishaji na kuleta ushindani sawa kwa wenye viwanda katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* kwa kuwa nchi nyingine hivi sasa hazitozi ushuru kwenye bidhaa hiyo, yaani zile nchi za Afrika Mashariki tunazoshirikiana pamoja.

(ii) Mheshimiwa Spika, kumekuwa na kilio cha muda mrefu cha wasanii kudurufiwa kazi zao za sanaa na kukosa maslahi kwa kazi wanazofanya. Ili kutatua tatizo hili, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato itaanza kurasimisha biashara ya bidhaa za muziki na filamu kwa nia ya kuhakikisha kwamba uasili wake unatambulika na hivyo kuzuia vitendo vya kudurufu kazi za sanaa *(piracy of artists work)* hali ambayo inadumaza ukuaji wa sanaa na vipaji vya wananchi wetu hapa nchini. Aidha, Mamlaka ya Mapato itaweka stampu kwenye bidhaa hizo ili uuzaji wa kazi hizo uwe rasmi na kuwawezesha wasanii kupata kipato stahili kutokana na kazi zao. Vilevile hatua hii itaiingizia Serikali mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa yanahitajika maandalizi ya kutosha ikiwa ni pamoja na kurekebisha sheria na kanuni mbalimbali, utekelezaji wa hatua hii utaanza rasmi tarehe 1 Januari, 2013.

(iii) Kufuta msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa magari kwa wote waliokuwa wananufaika na msamaha huo isipokuwa kwa miradi inayotekelezwa kwa misaada ya wafadhili yenye msamaha wa kodi kwenye mkataba, mashirika ya dini, Balozi, Ofisi za Balozi, Wanabalozi na Wawakilishi wa mashirika ya kimataifa *(Diplomats and Diplomatic Missions).* Aidha, haitahusu Kampuni za Madini zenye mikataba yenye kutoa misamaha. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Rudia.

**WAZIRI WA FEDHA:** Nirudie?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**WAZIRI WA FEDHA:** Narudia hicho kipengele cha tatu, kufuta msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa magari kwa wote waliokuwa wananufaika na msamaha huo, isipokuwa kwa miradi inayotekelezwa kwa misaada ya wafadhili yenye msamaha wa kodi kwenye mkataba, mashirika ya dini, Balozi, Ofisi za Balozi, Wanabalozi na Wawawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa yaani *Diplomats and Diplomatic Missions*. Aidha, haitahusu kampuni za Madini zenye mikataba yenye kutoa misamaha.

**MBUNGE FULANI:** *How*?

*(Hapa Wabunge walinong'ona kuashiria kutoelewa kilichokuwa kikielezwa na Waziri wa Fedha)*

**SPIKA**: Mtapata muda wa kusoma na kuelewa.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naendelea.

(iv) Ili kulinda viwanda vya hapa nchini vinavyotengeneza maji ya matunda (juisi) dhidi ya ushindani usio haki wa bidhaa hiyo kutoka nje, maji ya matunda kutoka nje yatatozwa ushuru wa bidhaa wa shilingi 83 kwa lita, ambapo yanayozalishwa hapa nchini yatatozwa ushuru wa bidhaa wa shilingi nane (8) tu kwa lita. (*Makofi*)

(v) Kurejea msamaha wa ushuru wa mafuta ya petroli (*fuel levy)* uliotolewa mwaka 2011/2012 kwenye mafuta yanayotumika kuendesha meli, na vifaa vingine vinavyotumika katika utafiti wa mafuta na gesi ili usomeke kama Ushuru wa Bidhaa *(Excise Duty)* kwenye mafuta ya Petroli.

(vi) Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Ushuru wa Bidhaa unaotozwa kwenye pombe, vinywaji baridi, sigara, na mvinyo kama ifuatavyo:-

(a) Vinywaji baridi kutoka shilingi 69 kwa lita hadi shilingi 83 kwa lita ikiwa ni nyongeza ya shilingi 14;

(b) Mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango kinachozidi asilimia 75 kutoka shilingi 420 kwa lita hadi shilingi 145 kwa lita, ikiwa ni punguzo la shilingi 275;

(c) Mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25, kutoka shilingi 1,345 kwa lita hadi shilingi 1,614 kwa lita, ikiwa ni nyongeza ya shilingi 269;

(d) Vinywaji vikali, kutoka shilingi 1,993 kwa lita hadi shilingi 2,392 kwa lita, ikiwa ni nyongeza ya shilingi 399;

(e) Bia inayotengenezwa na nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa, kutoka shilingi 248 kwa lita hadi shilingi 310 kwa lita, ikiwa ni nyongeza ya shilingi 62 kwa lita; na … *(Makofi*)

(f) Bia nyingine zote, kutoka shilingi 420 kwa lita hadi shilingi 525 kwa lita, ikiwa ni nyongeza ya shilingi 105 sawa na shilingi 52.5 kwa chupa yenye ujazo wa nusu lita.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya viwango vya Ushuru wa Bidhaa kwenye sigara ni kama ifuatavyo: -

(a) Sigara zisizo na kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 6,820 hadi shilingi 8,210 kwa sigara elfu moja. Ongezeko hili ni sawa na nyongeza ya shilingi 1,390 kwa sigara elfu moja au shilingi 1.4 kwa sigara moja;

(b) Sigara zenye kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 16,114 hadi shilingi 19,410 kwa sigara elfu moja, ikiwa ni nyongeza ya shilingi 3,296 au shilingi 3.3 kwa sigara moja;

(c) Sigara nyingine zenye sifa tofauti na (a) na (b) kutoka shilingi 29,264 hadi shilingi 35,117 kwa sigara elfu moja, ikiwa ni nyongeza ya shilingi 5,853 sawa na shilingi 5.8 kwa sigara moja;

(d) Tumbaku ambayo iko tayari kutengeneza sigara *(cut filler)* kutoka shilingi 14,780 hadi shilingi 17,736 kwa kilo, ikiwa ni nyongeza ya

shilingi 2,956 kwa kilo; na

(e) Ushuru wa "*Cigar*" unabaki kuwa asilimia 30. (*Kicheko*)

(vii) Kutoza Ushuru wa bidhaa kwenye Gesi asilia inayotumika viwandani kwa kiwango cha Shilingi 0.35 kwa kila futi ya ujazo (Shs 0.35 *per cubic feet).*

(viii) Kuongeza Ushuru wa bidhaa kwenye muda wa maongezi (*airtime*) kwenye simu za mkononi kutoka asilimia 10 kwenda asilimia 12. Lengo la hatua hii ni kuwianisha ushuru wa bidhaa unaotozwa kwa huduma hii katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa wakati huu ambapo tupo kwenye Soko la Pamoja. Wenzetu wote Afrika Mashariki kwa makubaliano ya Soko la Pamoja tulikubaliana ushuru unaofanana. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatua hizi katika Ushuru wa Bidhaa kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 144,054.9.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Mauzo Nje, Sura 196. Napendekeza kuongeza kiwango cha ushuru wa mauzo nje *(export levy)* kwenye bidhaa za ngozi ghafi zinazosafirishwa kwenda nje ya nchi kutoka asilimia 40 za sasa au Shilingi 400 kwa kilo moja hadi asilimia 90 au Shilingi 900 kwa kilo moja kutegemea kiwango kipi ni kikubwa. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha usindikaji wa ngozi hapa nchini na kuongeza thamani ya bidhaa za ngozi. Aidha, hatua hii itachangia katika kukuza ajira viwandani na kuongeza mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 26,431.8.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Michezo ya Kubahatisha *(Gaming Act),* Sura 40. Napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Michezo ya Kubahatisha *(Gaming Act),* Sura 40; kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza tozo la *Gaming Tax* kwa *casino* kutoka asilimia 13 ya mapato ghafi ya mchezo wa kubahatisha *(Gross Gaming Revenue)* hadi asilimia 15;

(ii) Kutoza tozo kwenye michezo ya Utabiri wa Matokeo ya Michezo (*Sports Betting)* kwa asilimia 6 ya *"total stakes*";

(iii) Kutoza tozo la *Gaming Tax* kwa kiwango cha asilimia 43 kwenye michezo ya "*SMS Lotteries";*

(iv) Kutoza tozo la *Gaming Tax* kwa kiwango cha asilimia 15 kwa michezo ya *Internet Casino*.

(v) Kuweka kipengele katika Sheria ya Kodi ya Michezo ya kubahatisha kinachotamka kwamba "*gaming tax shall be conclusive tax". (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 6,360.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme juu ya Sheria ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura 124. Napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura 124 kwa kuanzisha utaratibu wa kumiliki usajili wa namba za magari zenye utambulisho wa taarifa za mtu binafsi kwenye gari lake kwa ada ya shilingi 5,000,000 kwa miaka mitatu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie hili, kuna mtu anapenda gari lake lionyeshe jina analotaka yeye au jina lake lakini tunataka kupata fedha. Kwa nafasi hii tuwape ruksa na wao watupe fedha. Mtu yeyote atakayependa kufanya hivyo atulipe shilingi milioni 5,000,000 lakini hiyo itadumu kwa miaka mitatu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 50 lakini kikubwa zaidi watu watahamasika na watafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Viwanja vya Ndege, Sura 365. Napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Viwanja vya Ndege, Sura 365 kwa kuongeza tozo ya huduma za viwanja vya ndege *(Airport Service Charges)* kutoka kiwango cha sasa cha Dola za Kimarekani 30 hadi Dola 40 kwa safari za nje na kutoka Shilingi za Tanzania 5,000 hadi Shilingi 10,000 kwa safari za ndani. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 11,597.7.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme juu ya misamaha ya kodi ya magari kupitia Sheria za Kodi na Matangazo ya Serikali *(GNs)*. Napendekeza kufanya marekebisho kwenye sheria husika za kodi na matangazo ya Serikali yanayotoa msamaha wa kodi kwenye magari kwa walengwa mbalimbali ili kuweka ukomo wa umri wa miaka nane (8) kwa magari hayo badala ya miaka 10, magari kuukuu. Aidha, magari yenye umri wa zaidi ya miaka nane (8) yatatozwa Ushuru wa bidhaa wa asilimia 20. Lengo la hatua hii ni kupunguza wimbi la uagizaji wa magari chakavu na kulinda mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Marekebisho mengine katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria za Usimamizi wa Fedha. Napendekeza kufanya marekebisho mengine madogo madogo yasiyo ya kisera katika Sheria mbalimbali za kodi ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki, Sura 231 ili kwanza, kuweka kinga dhidi ya mali zinazomilikiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki ikiwemo nyumba, akiba, fedha na akaunti za benki dhidi ya mashauri ya kisheria, maamuzi ya kimahakama na utaifishaji.

Pili, kuipa hadhi ya mdai benki hii kama ilivyo kwa Taasisi ya Fedha ya Kimataifa (*IMF*), Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika ili kuiwezesha kupewa upendeleo endapo yatatokea matatizo yoyote katika soko la fedha.

Tatu, kumpa mamlaka Waziri wa Fedha kutekeleza maamuzi ya Baraza la uongozi (*Governing Board)* la *EADB* kwa kurekebisha Jedwali la Sheria hii kupitia Tangazo la Serikali na baadaye kuwasilisha taarifa Bungeni.

Nne, kutoa tafsiri ya mali za benki ili kutoa ufafanuzi kwamba mali za benki ni pamoja na nyumba za benki, akiba za fedha zilizokasimiwa kwa *EADB* kwa ajili ya utendaji wake.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya ada na tozo mbalimbali za Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea. Napendekeza kufanya marekebisho ya viwango vya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea ili kuvihuisha kulingana na hali halisi ya ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ya mwaka 2004. Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya Kikao cha maandalizi ya Bajeti *(Pre-Budget Consultations of EAC Ministers for Finance)* mnamo tarehe 18 Mei 2012 jijini Kampala, Uganda. Kikao hicho kilipendekeza marekebisho ya viwango vya Ushuru wa Pamoja wa Forodha *(EAC-Common External Tariff "CET")* na Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC-Customs Management Act, 2004)* kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013. Mapendekezo hayo yanalenga katika kuboresha Sekta za Viwanda, Usafirishaji, Afya, Nishati, Mifugo, Mawasiliano na Habari.

Mheshimiwa Spika, maeneo yanayopendekezwa kufanyiwa marekebisho kwenye viwango vya Ushuru wa Pamoja wa Forodha ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijasoma naomba kueleza kwamba Afrika Mashariki tuna makubaliano ya kuwa na kodi zinazofanana, kwa hiyo, hizi hapa zinaletwa kwa ajili ya idhini yenu.

(i) Kutoza ushuru wa asilimia sifuri (0%) badala ya asilimia 35 kwenye ngano inayotambuliwa katika *HS Code* 1001.90.20 na *HS Code* 1001.90.90 kwa kipindi cha mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uingizaji wa bidhaa hii nchini kwa vile uzalishaji wa ndani bado ni wa chini kuweza kutosheleza mahitaji.

(ii) Kuongeza Ushuru wa Forodha kwenye *galvanized wire* kutoka asilimia sifuri (0%) hadi asilimia 10 inayotambuliwa katika *HS Code 7217.20.00*. Hatua hii inalenga katika kuwianisha viwango vya utozaji wa Ushuru wa Forodha kwa vile bidhaa hii inatengenezwa kutokana na *hot rolled steel wire rods* zinazotambuliwa katika *HS Code 7213.20.00* ambayo inatozwa ushuru wa asilimia 10.

(iii) Kutenganishwa kwa bidhaa zinazotambulika katika *HS Code* 2106.90.91 ili kutenganisha virutubisho vya chakula na madini *(Food Supplements and Mineral Premix)* vinavyotumika katika kutengeneza chakula cha watoto wachanga na kuzitoza Ushuru wa Forodha wa asilimia sifuri (0%). Hatua hii inalenga katika kuwezesha watoto wachanga na wagonjwa kuweza kupata vyakula vyenye virutubisho kwa bei nafuu na kuimarisha afya zao.

(iv) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia sifuri kwenye ving'amuzi *(Set Top Boxes)* vinavyotambuliwa katika *HS Code 8528.71.00* ili kuwezesha mabadiliko ya kutoka katika teknolojia ya analogi na kwenda katika teknolojia ya digitali, mtakumbuka sasa hivi ni asilimia 25, tunataka iwe zero. Hatua hii inatekeleza makubaliano ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba ifikapo Desemba 2015 ziwe zimetoka kwenye mfumo wa utangazaji wa analogi kwenda digitali.

(v) Kupunguza Ushuru wa Forodha kwenye umeme (*HS Code* 2716.00.00) kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri (0%). Hatua hii inalenga katika kupunguza gharama ya umeme unaonunuliwa kutoka nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na hivyo kupunguza gharama za uzalishaji katika nchi hizo. (*Makofi*)

(vi) Kupunguza Ushuru wa Forodha kwenye glasi za ndani *(inner glass)* za chupa za chai (*thermos*) zinozotambuliwa katika *HS Code* 7020.00.90 kutoka asilimia 25 hadi asilimia sifuri ili kutoa unafuu na kuchochea ukuaji wa viwanda vya kuunganisha chupa za chai katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuwa bidhaa hiyo haipatikani katika Jumuiya.

(vii) Kutenganisha programu (*software*) inayotambulika katika *HS Code* 8523.80.00 ili kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia sifuri (0%). Lengo ni kuhamasisha ukuaji wa Sekta ya Mawasiliano na hivyo kuongeza mchango wake katika Pato la Taifa.

(viii) Kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha *(duty remission)* kwenye malighafi ya kutengeneza sabuni *(Palm Sterini, RBD)* inayotambuliwa katika *HS Code 1511.90.40* kwa kipindi cha mwaka moja. Hatua hii inalenga katika kuvipa unafuu viwanda vidogo vya kutengeneza sabuni hapa nchini na kuviwezesha kumudu ushindani katika bidhaa hiyo inapoingizwa kutoka nje.

(ix) Kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha *(duty remission)* kwa malighafi ya kutengeneza sabuni inayojulikana kama *LABSA* inayotambuliwa katika *HS Code 3402.11.00; HS Code 3402.12.00* na H*S Code 3402.19.00* kwa kipindi cha mwaka mmoja. Hatua hii inalenga katika kuimarisha uzalishaji na kukuza viwanda vidogo vya sabuni nchini.

(x) Kupunguza Ushuru wa Forodha kwenye bidhaa inayojulikana kama *cathodes* inayotambuliwa katika *HS Code 7403.11.00* kutoka asilimia 10 hadi sifuri (0%). Hivi sasa bidhaa hii inatozwa ushuru wa asilimia 10 ambapo shaba iliyotengenezwa kwa ukamilifu *(refined alloys/refined copper)* hutozwa ushuru wa asilimia (0%), ambapo ni

kinyume na matakwa ya Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004. Lengo la hatua hii ni kuwianisha ushuru wa malighafi inayotumika kuzalisha bidhaa hii ili iendane na kanuni/taratibu za kutoza ushuru zinazozingatia viwango vya usindikaji.

(xi) Kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 badala ya asilimia 35 kwenye saruji inayotambuliwa katika *HS Code* 2523.90.00 kwa kipindi cha mwaka mmoja.

(xii) Kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha *(duty remission)* kwa wazalishaji wanaotumia mafuta ya kutengeneza vilainishi *(castor oil and its fraction)* inayotambuliwa katika *HS Code* 1515.30.00. Hatua hii imezingatia kwamba bidhaa hii ni malighafi inayotumika katika kutengeneza vilainishi.

(xiii) Kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye vyuma vinavyowekwa kwenye kingo za barabara vijulikanavyo kama *road guard rails* kwa kutenganisha *HS Code 7308.90.90.* Lengo ni kutoa unafuu katika ujenzi wa miundombinu ya barabara zetu. Aidha, hatua hii inazingatia kwamba bidhaa hii haizalishwi kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa Fedha wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya marekebisho kwenye Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC-Customs Management Act, 2004)* kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya marekebisho katika Kifungu 30(b) cha Sehemu B ya Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye mitambo (*machinery*) na vipuri vyake vinavyotumika kwenye uchimbaji wa madini. Msamaha huu hautahusisha vipuri vya magari vitakavyoagizwa na makampuni yanayojihusisha na uchimbaji wa madini.

(ii) Kufanya marekebisho katika aya ya 22 (a) ya Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuongeza *"refrigerated trailers"* katika bidhaa zinazopata msamaha wa Ushuru wa Forodha. Hatua hii inalenga katika kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye magari ya trela yenye majokofu ili kuimarisha biashara ya usambazaji bidhaa kama vile nyama, maziwa n.k.

(iii) Kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye malighafi zinazotumika katika kutengeneza vifaa vya kufanyia uchunguzi wa magonjwa *(medical diagnostic kits)* kwa kuwa vifaa hivyo hutozwa asilimia sifuri (0%) vinapoagizwa kutoka nje. Aidha, lengo pia ni kuhamasisha uzalishaji wa bidhaa hiyo katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

(iv) Kufanya marekebisho katika Jedwali la Tano, B kwenye aya ya 15 ili kuongeza vifaa vinavyotumika katika ufugaji na kurina asali na kuvipa msamaha wa ushuru wa forodha vinapoagizwa nje na wafugaji wa nyuki. Lengo ni kuhamasisha na kuchochea ukuaji wa sekta ya ufugaji wa nyuki hapa nchini. *(Makofi*)

(v) Kuendelea kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye migahawa ya Majeshi ya Ulinzi kwa kipindi cha mwaka mmoja ujao.

(vi) Kufanya marekebisho katika Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 ili kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha *(duty remission)* kwa wazalishaji wa vyakula vinavyotengenezwa mahsusi kwa lishe ya watoto wenye utapia mlo na watu wanaoishi na virusi vya ukimwi. Hatua hii inalenga katika kuwawezesha kupata vyakula hivyo kwa gharama nafuu na kuboresha afya zao.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine ninayotarajia kufanya kwenye Ushuru wa Forodha ni kama ifuatavyo:-

(i) Kufuta msamaha wa Ushuru wa Forodha kwa magari yenye ujazo wa cc 3000. Hatua hii haitahusu miradi inayotekelezwa kwa misaada ya wafadhili yenye msamaha wa kodi kwenye mikataba, mabalozi na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa *(Diplomats and Diplomatic missions).*

(ii) Kupunguza msamaha wa kodi uliokuwa unatolewa kwenye bidhaa zinazotambulika kama "*deemed capital goods"* kutoka asilimia 100 hadi asilimia 90. Kwa mantiki hiyo, mwekezaji atatakiwa kulipa asilimia 10 ya kodi zote zinazotozwa kwenye bidhaa husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatua hizi kwa pamoja zinatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 12,805.

Mheshimiwa Spika, hatua zote za mapato kwa ujumla zimezingatia azma ya Serikali ya kukuza uchumi na kuongeza mapato ili hatimaye kupunguza utegemezi wa bajeti kutoka kwa wahisani. Aidha, ili kutekeleza azma hiyo, hatua za mapato zinalenga katika kupunguza misamaha ya kodi hatua kwa hatua ili kufikia kiwango cha asilimia 1 ya Pato la Taifa kama ilivyo katika nchi nyingine Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, tarehe ya kuanza Kutekeleza hatua mpya za kodi. Hatua hizi za kodi zinazopendekezwa zitaanza kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2012, isipokuwa pale ilipoelezwa vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, sura ya bajeti kwa mwaka 2012/2013. Kwa kuzingatia sera za uchumi pamoja na misingi na sera za bajeti, Serikali inatarajia kukusanya shilingi bilioni 15,119.6. Kati ya mapato hayo, Serikali inalenga kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya jumla ya shilingi bilioni 8,714.8 sawa na asilimia 18 ya Pato la Taifa. Aidha, mapato kutokana na vyanzo vya Halmashauri ni shilingi bilioni 362.2 sawa na asilimia 0.7 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, washirika wa maendeleo wanatarajiwa kuendelea kutusaidia mwakani kwa kutupatia misaada na mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 3,156.7. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 842.5 ni misaada na mikopo ya kibajeti na shilingi bilioni 2,314.2 ni mikopo na misaada kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ikijumuisha *Basket Funds* na fedha za *Millenium Challenge Account (MCA - T).*

Mheshimiwa Spika, Serikali inategemea kukopa kiasi cha shilingi bilioni 2,886.1 kutoka vyanzo vya ndani na nje kuziba pengo la mapato. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1,148.1 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali za muda mfupi zinazoiva, shilingi bilioni 483.9 ambayo ni asilimia moja ya Pato la Taifa na shilingi bilioni 1,254.1 ni mikopo yenye masharti ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 15,119.6 katika mwaka 2012/2013 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Jumla ya shilingi bilioni 10,591.8 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha shilingi bilioni 3,781.1 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Serikali, Taasisi na Wakala za Serikali na shilingi bilioni 2,745.1 kwa ajili ya Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 4,527.8 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 2,213.6 kitagharamiwa kwa fedha za ndani na shilingi bilioni 2,314.2 kitagharamiwa kwa fedha za nje (misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo ikijumuisha miradi ya MCA (T) na *basket fund).*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mfumo wa bajeti kama ulivyoelezwa hapo juu, sura ya bajeti kwa mwaka 2012/2013 inakuwa kama ifuatavyo:-

| | Mapato | | Shilingi Milioni |
|---|---|---|---|
| **A.** | **Mapato ya Ndani** | | **8,714,671** |
| | (i) Mapato ya Kodi (TRA) | 8,070,088 | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | (ii) Mapato yasiyo ya Kodi | | 644,583 | |
| **B.** | **Mapato ya Halmashauri** | | | **362,206** |
| **C.** | **Mikopo na Misaada ya Kibajeti** | | | **842,487** |
| **D.** | **Mikopo na Misaada ya Miradi ya Maendeleo ikijumuisha MCA (T)** | | | **2,314,231** |
| **E.** | **Mikopo ya Ndani** | | | **1,631,957** |
| **F.** | **Mikopo yenye Masharti ya Kibiashara** | | | **1,254,092** |
| | **JUMLA YA MAPATO YOTE** | | | **15,119,644** |
| | **Matumizi** | | | |
| **G.** | **Matumizi ya Kawaida** | | | **10,591,805** |
| | (i) Deni la Taifa | | 2,745,056 | |
| | (ii) Mishahara | | 3,781,100 | |
| | (iii) Matumizi Mengineyo | | 4,065,649 | |
| | Wizara | 3,311,399 | | |
| | Mikoa | 49,701 | | |
| | Halmashauri | 704,549 | | |
| **H.** | **Matumizi ya Maendeleo** | | | **4,527,839** |
| | (i) Fedha za Ndani | | 2,213,608 | |
| | (ii) Fedha za Nje | | 2,314,231 | |
| | **JUMLA YA MATUMIZI YOTE** | | | **15,119,644** |

Mheshimiwa Spika, mambo yaliyozingatiwa wakati wa mgao wa fedha kwa bajeti ya mwaka 2012/13 ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kuweka mafungu yote katika kiwango cha mgao wa fedha kinacholingana na matarajio ya matumizi ya mafungu husika kwa mwaka 2011/2012;

(ii) Kuyatengea fedha matumizi yasiyoepukika kama vile posho za kisheria, "*ration allowance*", n.k.

(iii) Maeneo mapya ya utawala;

(iv) Fedha zinazotolewa kwa Wizara zenye utaratibu wa kubakiza (*retention*); na

*(v)* Maeneo ya vipaumbele (*strategic* na *non-strategic).*

Mheshimiwa Spika, bajeti ninayoiwasilisha ina uwiano wa asilimia 70 kwa matumizi ya kawaida na asilimia 30 kwa matumizi ya maendeleo. Viwango hivyo vya uwiano vimezingatia ukweli kwamba makisio ya matumizi ya maendeleo kwa fedha za ndani ya Shilingi 1,871.5 bilioni na makisio ya matumizi ya maendeleo kwa fedha za nje ya Shilingi 3,054.1 bilioni yenye jumla ya Shilingi 4,925.6 kwa mwaka 2011/2012 hayatafikiwa. Hivyo, inatarajiwa kwamba hali halisi ya

matumizi ya maendeleo itakuwa Shilingi 2,983 bilioni ambayo ni karibu ya asilimia 22 yaani kwa mwaka huu unaoishia mwezi huu, uwekezaji wetu katika miradi ya maendeleo umefikia asilimia 22. Kwa hali hiyo, tunapopanga kuelekea mbele kwa kipindi kilichoishia Aprili, 2012 matumizi ya maendeleo kwa fedha za ndani yalifikia shilingi 1,201.6 bilioni na matumizi ya maendeleo kwa fedha za nje ni shilingi 1,450.4 bilioni. Sababu za kutofikiwa kwa malengo hayo ya matumizi nimezieleza hapo awali ikiwa ni pamoja na kutopatikana kwa fedha za mikopo ya kibiashara na kuchelewa kwa fedha za misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo kutoka kwa wahisani. Aidha, uwiano huo umezingatia maeneo niliyoyataja hapo juu ambayo ni matumizi muhimu.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, Serikali kupitia bajeti hii imejipanga kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2012/2013 ambao unaelekeza uwekezaji wa rasilimali za Taifa kwenye maeneo machache ya kipaumbele kwa lengo la kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi na kupunguza umaskini. Serikali itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kwa kuwekeza zaidi katika maeneo ya kipaumbele. Aidha, kila mwananchi anapaswa kushiriki kikamilifu katika kutumia fursa zinazojitokeza kwa kutoa huduma na kuzalisha mali ili kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, kufanikiwa kwa Bajeti ya Mwaka 2012/2013 kunahitaji nidhamu ya hali ya juu kwa kila Wizara, Idara, Mikoa, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za umma. Matumizi yasiyokuwa na tija na ambayo si muhimu ni vyema yakaepukwa. Sekta binafsi ina uwezo mkubwa wa kuchangia katika uchumi. Hivyo, ni muhimu kila Wizara, Idara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa fursa kwa sekta binafsi ili waweze kuchangia kikamilifu katika kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Bunge la Bajeti mwaka huu unafanyika miezi michache kabla ya zoezi muhimu la Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika tarehe 26 Agosti 2012. Kauli mbiu ya sensa ya mwaka huu ni ''Sensa kwa Maendeleo Jiandae Kuhesabiwa''. Napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na viongozi wengine katika ngazi zote kuhamasisha wananchi kushiriki katika zoezi hili ambalo matokeo yake yatawezesha kupata takwimu muhimu zitakazowezesha Serikali kupanga mipango kwa ajili ya maendeleo ya wananchi kwa usahihi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru wapiga kura wangu wote wa Jimbo la Kalenga kwa kunichagua kuwa Mbunge wao na kwa ushirikiano wanaonipatia. Napenda kuwaahidi kuwa nitaendelea kushirikiana nao kuliletea maendeleo Jimbo letu la Kalenga. Mwisho namshukuru mke wangu mpendwa pamoja na familia kwa kuwa msaada kwangu katika kutekeleza majukumu haya mapya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Tafadhali, mwongozo wa Spika hata watu hawaja- *conclude*? Miongozo wakati wa siku ya bajeti huwa haitolewi, siku ya bajeti hamtoi miongozo, mmesikiliza waliyosema, sasa muache tuendelee na kazi yetu.

Waheshimiwa Wabunge hoja hii imeungwa mkono, sasa nitawahoji.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyokuwa tumetangaza awali kwamba kitabu hiki cha hotuba ya Waziri kuna hii *addendum*, mtakaposoma msisahau kusoma hii *addendum* kwa sababu mkisahau hii *addendum* mtasoma kitu kingine, kwa hiyo, mtakapokuwa mnasoma msisahau.

Pili, vitabu *Volume* I, *Financial and Revenue Estimates* vitakuwa kwenye *pigeon holes*, mimi ninacho hiki, kwa hiyo mtavikuta kwnye *pigeon holes*.

Tatu, naomba nitangaze kuwepo kwa wageni wetu waliokuja kutusindikiza katika kusikiliza bajeti hii. Kwa sababu ya wingi wa wageni, mtanisamehe, nitataja kwa makundi tu maana nikiwataja mmoja mmoja hapa tutatumia saa moja. Kwa hiyo, Waheshimiwa wageni wetu pamoja na Waheshimiwa Wabunge, naomba mridhike kwamba tutawataja kwa kupitia makundi yao.

Kwanza kabisa kama mnavyoona mara zote Mabalozi wanakaa kwenye *Speaker's gallery* lakini kwa leo kwa sababu Mabalozi waliokuja ni wengi imebidi tuwape nafasi ile pale. Kwa hiyo, tuna Waheshimiwa Mabalozi wanaowakilisha nchi zao hapa nchini, *they are seated over that place and we welcome you and we are grateful that you have been able to come and participate with us in this activity. Thank you very much.* (*Makofi*)

Tuna Waheshimiwa Majaji na viongozi wa Mahakama na wao sijui wamekaa wapi, naomba wasimame, ahsante karibu sana, nafikiri ni Jaji Mkazi hapa, ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, sijui wenyewe wako wapi, ahsante sana. Tunawapa pongezi na karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna Makatibu Wakuu pamoja na Makamishna kutoka Wizara zote za Serikali huko waliko, ahsante. Wako huku nyuma huku, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tuna Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Wakuu wa Wilaya za Dodoma na Waheshimiwa Madiwani hapo walipo, ahsante sana. Hawa ni wenyeji wetu wa Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Kuna Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa hapa nchini, hawa ni *International Organisation Representatives, wherever they are, can they raise?* Nafikiri walisimama pamoja na wale wageni wengine*. (Makofi)*

Tuna wawakilishi kutoka *General Budget Support Development Partners,* hawa nadhani ndiyo walewale tena waliokuwa wametajwa. *(Makofi)*

Tuna Mheshimiwa Msekwa, Spika Mstaafu, tunamuona pale, ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna Viongozi wa Vyama vya Siasa ambao wamealikwa, tulimuona asubuhi Mheshimiwa Professor Lipumba. *(Makofi)*

Waheshimiwa wengine sikuwaona lakini Mheshimiwa Mbatia alikuwa hodari sana kuja sasa yuko ndani ya *House*, ameiga hatua nyingine*. (Kicheko/Makofi)*

Kuna Wabunge wastaafu popote walipo pale, wasimame. *Okay*, ahsante, karibuni sana, tunaomba muendelee kuchangamka tu. *(Makofi)*

Tuna Wakuu wa Vyombo vya Fedha nchini, Mashirika ya Umma, Mifuko ya Jamii na taasisi mbalimbali za umma, popote walipo wasimame, *okay*, ahsante sana. Tunawatakia kheri zaidi katika utekelezaji wa bajeti hii. *(Makofi)*

Kuna wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, ahsanteni sana, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Tuna Viongozi wa Dini wa Mkoa, kokote walipo, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tuna viongozi wa Kitaifa wa Chama cha Wafanyakazi *TUGHE*, hawa wako wapi? Yupo pale mmoja na wengine wapo pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna Maafisa kutoka Wizara ya Fedha na Wizara zote za Serikali, nadhani wale waliosimama wakati ule. *(Makofi)*

Pia tuna Waandishi wa Habari, hebu simameni na nyie. Ahsante sana. Ingawa tunao kila siku lakini tunawashukuru kwa kazi ambayo wanaendelea nayo. *(Makofi)*

Ahsanteni sana na wageni wengine ambao sikuwataja lakini wote mnakaribishwa. Kama nilivyosema, Bunge ni mahali ambapo wote mnakaribishwa hata kama hamjatambulishwa, kama unakosa kuingia humu ndani ni sababu ya nafasi tu.

Pia nimemwona *CAG* na Mheshimiwa Kitilya mwenye kukusanya mapato *TRA*. *(Makofi)*

Naona watu wangu walisahau watu muhimu sana hapa na wengine ni *Governor* wa Benki nafikiri, sina majina yao, nafikiri ni Mheshimiwa *Governor* na wasaidizi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, alisema mke wake mpendwa, yupo?

**MJUMBE FULANI:** Hayupo!

**SPIKA:** Haya basi, amesikia salamu zetu.

Kamishna wa Bajeti yuko wapi? Mheshimiwa Mwamnyange, mama Mwamnyange naona atakuwa na wenzie kule, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa kama nilivyosema, upo uwezekano kwamba wengine hatukuwataja si kwa makusudi, nadhani labda taarifa zilikuja *late* ndiyo maana hawakutajwa lakini nawashukuru sana wote kwa kuja kushirikiana na sisi. Wanasema shughuli ni watu na watu ni sisi wenyewe, mngekuwa hampo, tungekuwa kama wanyonge, ahsanteni sana kwa kuja. *(Makofi)*

Ninayo matangazo mawili mengine, moja Kaimu Katibu wa Kamati ya Waheshimiwa Wabunge wa CCM, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati ya Wabunge wa CCM kuwa kesho tarehe 15, saa nne asubuhi kutakuwa na kikao kitakachofanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa. Tulitangaza kwamba ingekuwa saa tisa, tukasema saa tano, sasa naona imekuja *officially* saa nne katika ukumbi wa Msekwa.

Halafu, nilitangaza lakini wengi hamkuwepo, kwamba tarehe 16 kesho kutwa kutakuwa na uzinduzi wa Awamu ya Nne ya Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma yaani *The Public Financial Management Reform Program.* Ni huu mradi ambao unahusisha Kamati ya *Public Accounts Committee,* Kamati ya *LAAC*, Kamati ya *POAC* na Kamati ya Uchumi na Fedha ambao ulikuwa unafadhiliwa na *Development Partners* umeingia Awamu yake ya Nne. Tulikuwa na Awamu ya Kwanza, tukawa na Awamu ya Pili na Tatu ndiyo wamemalizia juzi na wanaingia Awamu ya Nne. Kadiri tulivyosaidiwa na mradi huu, ndiyo mnaona kuchangamka kwa taarifa za Kamati yangu na Kamati za *CAG*, kwa kweli imetokana sana na kazi ya mradi huu. Kwa sababu wameimarisha ofisi ya *CAG*, wameimarisha Wabunge na mambo mengine. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tutakuwa na huu uzinduzi tarehe 16, saa nne asubuhi katika ukumbi wa Msekwa. Kwa hiyo, mnaombwa Waheshimiwa Wabunge msikose kwa sababu ni mradi unaotuimarisha sisi wenyewe.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge naomba niwashukuru sana kwa jioni hii na tumpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na watu wote walioshughulika kuandaa bajeti hii na kama mlivyoona ilikuwa sio kazi rahisi, tumegombana mpaka karibu dakika za mwisho na kama tulivyoahidi, tutajipanga tuangalie mfumo ulio bora zaidi wa kufanya bajeti iwe shirikishi zaidi kuliko ilivyokuwa sasa. Lakini tunawapongeza sana kwa hatua hiyo kwa sababu Waziri mwenyewe ndiyo mara yake ya kwanza kuwasilisha hotuba. Kwa hiyo, si kitu rahisi, uone tu vinaelea lakini ni vigumu sana.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge, naomba kuahirisha kikao hiki cha Bunge mpaka Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 12. 41 jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Jumatatu, Tarehe 18 Juni, 2012, Saa Tatu Asubuhi)*